# HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

# VIONGOZI WAKUU WA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

| | |
|---|---|
|  |  |
| Mhe. Inocent L.Bashungwa (Mb.),<br>*Waziri wa Viwanda na Biashara* | Mhe. Mhandisi<br>Stella M. Manyanya (Mb.),<br>*Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara* |
|  |  |
| Prof. Riziki S. Shemdoe<br>*Katibu Mkuu* | Bw. Ludovick J. Nduhiye<br>*Naibu Katibu Mkuu* |

## YALIYOMO


***1. UTANGULIZI ........................................................1***

***2. MCHANGO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KATIKA UCHUMI..............................7***

**2.1. Sekta ya Viwanda. ..............................................7**

**2.2. Sekta ya Biashara................................................8**

***3. MAFANIKIO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KATIKA AWAMU YA TANO.............8***

**3.1. Mafanikio katika Sekta ya Viwanda................10**

**3.2. Mafanikio ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ...................................................16**

**3.3. Mafanikio katika Sekta ya Biashara ...............19**

**3.4. Mafanikio ya Sekta ya Masoko .........................23**

***4. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020................................29***

**4.1. Bajeti Iliyoidhinishwa na Kupokelewa kwa Mwaka 2019/2020 ............................................29**

**4.2. Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti kwa Mwaka 2019/2020 ............................................30**

*4.2.1.* Sekta ya Viwanda ......................................................30

*4.2.2.* Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo .......64

*4.2.3.* Sekta ya Biashara......................................................73

*4.2.4.* Sekta ya Masoko .......................................................91

*4.2.5.* *Maendeleo ya Rasilimali Watu na Utoaji Huduma*.........................................................................132

*4.2.6.* *Ukaguzi wa Ndani*....................................................134

*4.2.7.* *Ununuzi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha*.........135

*4.2.8. Mawasiliano Serikalini*......136
*4.2.9. Huduma za Sheria*......136
*4.2.10. TEHAMA na Takwimu*......137

***5. MWELEKEO NA VIPAUMBELE VYA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA......138***

**5.1. Mwelekeo wa Sekta ya Viwanda na Biashara......138**

**5.2. Vipaumbele kwa Bajeti ya Mwaka 2020/2021......153**

***6. MALENGO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA 2020/2021......154***

**6.1. Malengo ya Makuu ya Wizara......154**
*6.1.1. Sekta ya Viwanda*......155
*6.1.2. Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo*......156
*6.1.3. Sekta ya Biashara*......157
*6.1.4. Sekta ya Masoko*......159
*6.1.5. Maendeleo ya Rasilimali Watu*......160
*6.1.6. TEHAMA na TAKWIMU*......163
*6.1.7. Ununuzi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha*......163

**6.2. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021......164**
*6.2.1.* Taasisi za Kuendeleza Uwekezaji......164
*6.2.2. Taasisi za Utafiti, Maendeleo ya Teknolojia na Mafunzo*......166
*6.2.3. Taasisi za Ushindani na Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa na Huduma*......172

***7. MAKADIRIO YA MAKUSANYO NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021......181***

**7.1. Makusanyo ya Serikali......181**

**7.2. Maombi ya Fedha** .............................................. 182

***8. SHUKRANI*** ............................................................ ***182***

***9. HITIMISHO*** .......................................................... ***183***

***10. MAOMBI RASMI YA FEDHA*** .............................. ***184***

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACP | African, Caribbean and Pacific |
| ACT | Agriculture Council of Tanzania |
| AfCFTA | African Continental Free Trade Area |
| AGOA | African Growth and Opportunity Act |
| ALAF | Alluminium Africa |
| AMCOS | Agriculture Marketing Cooperative Society |
| AMGC | African Minerals and Geosciences Centre |
| ASDP | Agricultural Sector Development Programme |
| B0T | Bank of Tanzania |
| BRELA | Business Registration and Licencing Agency |
| B2B | Business to Business |
| CAMARTEC | Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology |
| CBOs | Community Based Organisation |
| CBT | Cashewnut Board of Tanzania |
| CET | Common External Tariff |
| CFC | Common Fund for Commodities |
| CGS | Credit Guarantee Scheme |
| COCs | Certificate of Conformity |
| COMESA | Common Market for Eastern and Southern Africa |
| CORECU | Coastal Regional Co-operative Union |

| | |
|---|---|
| COSOTA | Copyright Society of Tanzania |
| COSOZA | Copyright Society of Zanzibar |
| COVID -19 | Corona Virus Disease of 19 |
| CPB | Cereals and other Produce Board |
| CRDB | Commercial Rural Development Bank |
| CTI | Confederation of Tanzania Industries |
| DANIDA | Danish International Development Agency |
| DITF | Dar es Salaam International Trade Fair |
| DRC | Democratic Republic of Congo |
| EAC | East African Community |
| EGA | e Government Authority |
| EATV | East Africa Television |
| EIF | Enhanced Integrated Framework |
| EPZ | Export Processing Zone |
| EPZA | Export Processing Zone Authority |
| EU | European Union |
| FAO | Food Agriculture Organization |
| FBOs | Faith Based Organisation |
| FCC | Fair Competition Commission |
| FCT | Fair Competition Tribunal |
| FSDT | Financial Sector Deepening Trust |
| FTA | Free Trade Area |
| GCLA | Government Chemistry Laboratory Authority |
| GePG | Government Electronic Payment Gateway |
| GIZ | Germany Development Agency |
| GN | Government Notes |

| | |
|---|---|
| GPSA | Government Procurement Services Agency |
| GST | Geological Survey of Tanzania |
| ICDs | Inland Container Deport |
| ICT | Information and Communication Technology |
| IFAD | International Fund for Agriculture Development |
| IPs | Implementing Partners |
| ITC | International Trade Centre |
| ITDA | Intrasit Tanzania Drivers Association |
| ITV | Independent Television |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| JKT | Jeshi la Kujenga Taifa |
| KCU | Kagera Co-operative Union |
| KDCU | Karagwe District Co-operative Union |
| KOICA | Korea International Cooperation Agency |
| LGAs | Local Government Authorities |
| LIC | Local Investment Climate |
| MIVARF | Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Finance |
| MAMCU | Mtwara- Masasi Cooperative Union |
| MSD | Medical Store Department |
| MSY | Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza |
| MSMEs | Micro Small and Medium Enterprises |
| MWAMTUKA | Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya |

| | |
|---|---|
| | Tathmini ya Utendaji Kazi |
| NBP | National Business Portal |
| NCU | Ngara Cooperative Union |
| NDC | National Development Corporation |
| NEDF | National Entrepreneurship Development Fund |
| NFRA | National Food Reserve Authority |
| NHIF | National Health Insurance Fund |
| NIC | National Insurance Cooperation |
| NMB | National Microfinance Bank |
| NPCC | National Pharmaceutical Coordination Committee |
| NTBs | Non Tariff Barriers |
| OAS | Online Application System |
| OC | Other Charges |
| ODOP | One District One Product |
| ORS | Online Registration System |
| OSBP | One Stop Border Post |
| OSHA | Occupational Safety and Health Authority |
| PPRA | Public Procurement Regulatory Authority |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund |
| QUALIMIS | Quality Management System |
| RAS | Regional Administrative Secretary |
| REA | Rural Energy Agency |
| RoO | Rule of Origin |
| SADC | Southern African Development Community |
| SEZ | Special Economic Zone |

| | |
|---|---|
| SIDO | Small Industries Development Organization |
| SIDA | Swedish International Development Cooperation |
| SIDP | Sustainable Industrial Development Policy |
| SMEs | Small and Medium Enterprises |
| SPS | Sanitary and Phytosanitary |
| SUA | Sokoine University of Agriculture |
| TAA | Tanzania Airport Authority |
| TACACU | Tanga Cashew Co-operative Union |
| TADB | Tanzania Agricultural Development Bank |
| TAMCU | Tunduru Agricultural Co-operative Union |
| TAMISEMI | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANECU | Tandahimba and Newala Cooperative Union |
| TANePS | Tanzania Electronic Procurement System |
| TANESCO | Tanzania Electricity Supply Company Limited |
| TANROADS | Tanzania National Roads Agency |
| TANTRADE | Tanzania Trade Development Authority |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards |
| TBT | Technical Barriers to Trade |
| TCCIA | Tanzania Chambers of Commerce, Industry and Agriculture |

| | |
|---|---|
| TCB | Tanzania Coffee Board |
| TCDC | Tanzania Cooperative Development Commission |
| TDBP | Tanzania Domestic Biogas Programme |
| TDC | Technology Development Centre |
| TDU | Textile Development Unit |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TEMDO | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation |
| TFDA | Tanzania Food and Drug Authority |
| TIC | Tanzania Investment Center |
| TIRDO | Tanzania Industrial Research Development Organisation |
| TMDA | Tanzania Medicine and Medical Devices Authority |
| TMEA | Trade Mark East Africa |
| TMX | Tanzania Menchantile Exchange |
| TNBC | Tanzania National Business Council |
| TPCs | Training Cum Production Centre |
| TPMA | Tanzania Pharmaceutical Manufacturing Association |
| TPSF | Tanzania Private Sector Foundation |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TRF | Trade Related Facility |
| UAE | United Arab Emirates |
| UKIMWI | UPUNGUFU WA KINGA MWILINI |

| | |
|---|---|
| UNCTAD | United Nations Conference on Trade and Development |
| UNDP | United Nations Development Program |
| UNIDO | United Nations Industrial Development Organisation |
| USAID | United States Agency for International Development |
| USD | United State Dollars |
| VAT | Value Added Tax |
| VVU | Virusi Vya UKIMWI |
| WCF | Workers Compensation Fund |
| WFP | World Food Programme |
| WMA | Weights and Measures Agency |
| WRRB | Warehouse Receipt Regulatory Board |
| WTO | World Trade Organization |
| WIPO | World Intellectual Property Organization |

## DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

### Dira

Kuwa na msingi shindani wa viwanda, mazingira bora ya uwekezaji na ukuaji wa biashara unaowezesha kukua kwa uchumi shirikishi na endelevu.

### Dhima

Kujenga msingi shindani na endelevu wa viwanda wenye kuwezesha biashara ulimwenguni kwa kuzingatia faida za mahala tulipo kijiografia na rasilimali zilizopo nchini kupitia sera, mikakati na mipango kwa mageuzi shirikishi ya viwanda.

### Majukumu

Wizara ya Viwanda na Biashara ina dhamana ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na mikakati inayoongoza maendeleo ya Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Majukumu mahsusi ya kisekta ni kama yafuatavyo:-

i) Kuandaa, kuratibu na kupitia sera na mikakati ya sekta za Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo;
ii) Kufuatilia na kuperemba utendaji katika Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na taasisi

zinazowezesha maendeleo ya viwanda na biashara;

iii) Kubuni na kuandaa programu za kuendeleza sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji, Masoko, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na taasisi zinazowezesha maendeleo ya viwanda na biashara;

iv) Kukusanya, kuchambua, kusambaza na kutathmini taarifa za sekta za Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo;

v) Kukuza na kuhamasisha biashara ya ndani na nje na kuboresha upatikanaji wa huduma za kuendeleza biashara;

vi) Kuimarisha ufanisi wa utendaji wa wafanyakazi wa Wizara na Taasisi zake;

vii) Kusimamia utekelezaji wa sheria zinazosimamia viwanda na biashara;

viii) Kuimarisha utafiti wa maendeleo ya Sekta ya Viwanda;

ix) Kusimamia utendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara;

x) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa Sekta Binafsi; na

xi) Kutafuta fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania.

# 1. **UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika*;** Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu 44 (Viwanda) na Fungu 60 (Biashara) tarehe 24 na 25 Machi, 2020 Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mipango na Bajeti kwa Mwaka 2019/2020. Aidha, naliomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2020/2021.

2. ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa kuzingatia na kutambua kuwa hii ni Hotuba yangu ya Kwanza ya Bajeti nikiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na kwa kuwa hiki ni kikao cha mwisho cha Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fadhili zake kwa mja wake na kwa kunijalia afya na baraka katika majukumu niliyokasimiwa. Kwa namna ya pekee niruhusu nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kuwa Waziri na kunipa majukumu yanayobeba ajenda kuu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya ujenzi wa

uchumi wa viwanda. Nampongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya SADC na namna anavyoshughulikia masuala ya biashara katika nchi za SADC na EAC ikiwa ni pamoja na kuomba kufutiwa madeni kwa nchi za Afrika katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugionjwa wa COVID – 19. Nampongeza pia kwa namna anavyotuongoza kwa ujasiri na misingi imara, yenye kusheheni uzalendo na mapenzi kwa nchi yetu. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; pamoja na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi; Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; kwa jinsi walivyojizatiti na kusimamia ipasavyo misingi ya utaifa wetu na hususan kwa kuwahakikishia Watanzania kuwa Tanzania ni mahala salama na penye fursa za uhakika za kujiletea maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

3. ***Mheshimiwa Spika;*** Napenda kuchukua nafasi hii, kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa umakini wenu katika kuliongoza na kulisimamia Bunge letu. Pia, naipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Viwanda, Biashara na Mazingira, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mbunge wa Jimbo la Mvomero, Makamu wake Mheshimiwa Kanali Mstaafu Ali Khamis Masoud, Mbunge wa Jimbo la Mfenesini na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati. Ushauri na maelekezo yao yamekuwa chachu muhimu sana katika mageuzi ya kifikra na kiutendaji ya Wizara na hivyo kuchochea kasi ya maendeleo ya viwanda na biashara nchini.

4. ***Mheshimiwa Spika*;** Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wapya kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Kwa namna ya pekee, niwashukuru watangulizi wangu Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Jimbo la Sikonge aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja mtangulizi wake Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu. Nikiri kuwa misingi waliyoiweka imeendelea kuwa chachu muhimu katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara nchini.

5. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2019/2020, Bunge liliondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini,

Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar; Mheshimiwa Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard Mganga Ndasa, aliyekuwa Mbunge wa Sumve; na Mheshimiwa Balozi Augustine Mahiga aliyekuwa Mbunge wa Kuteuliwa na Waziri wa Katiba na Sheria. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia zao na wote walioguswa na misiba hiyo. Vilevile, naomba kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliopata misiba ya kufiwa na wazazi, watoto au wanafamilia wa karibu. Pia, natoa pole kwa Watanzania waliokumbwa na kadhia ya majanga mbalimbali kama vile ajali za majini, barabarani na majanga mengine yanayofanana na hayo.

6. ***Mheshimiwa Spika;*** Naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi; hususan Baraza la Taifa la Biashara (Tanzania National Business Council – TNBC ); Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (Tanzania Private Sector Foundation – TPSF); Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (Confederation of Tanzania Industries – CTI); Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (Tanzania Chambers of Commerce, Industry and Agriculture – TCCIA); na Baraza la Kilimo Tanzania (Agriculture Council of Tanzania – ACT) kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda

Vidogo na Biashara Ndogo. Tunaendelea kuwategemea kama nguzo na mihimili muhimu ya kushirikiana katika kutekeleza kwa vitendo sera na mipango ya kisekta katika kuendeleza viwanda na biashara na kuchochea ukuaji wa uchumi wetu kwa ujumla.

7. ***Mheshimiwa Spika;*** Hotuba hii ya Bajeti ninayoiwasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Naibu Waziri Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Jimbo la Nyasa; Katibu Mkuu, Prof. Riziki Silas Shemdoe; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ludovick James Nduhiye; Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa kujituma na kuonesha daima utayari wa kuboresha mbinu na mikakati ya kisekta kwa vitendo.

8. ***Mheshimiwa Spika;*** Nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Karagwe kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na ya Jimbo. Nawapongeza kwa namna wanavyojibidiisha katika kujiletea maendeleo. Aidha, ninawaahidi kwamba nitaendelea kutetea maslahi yenu hapa Bungeni na hata nje ya Bunge ili kuhakikisha Jimbo linaendelea kushamiri na kuleta matokeo ya mtu mmoja

mmoja, Jimbo na hatimaye kuongeza mchango wake kwa Taifa kwa ujumla. Kipekee namshukuru sana mke wangu mpendwa Jennifer Bashungwa, watoto na familia yangu kwa ujumla kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ya kitaifa.

9. ***Mheshimiwa Spika;*** Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuomba ushiriki wa dhati wa kila Mtanzania katika kupambana na usambaaji wa virusi vya CORONA vinavyosababisha ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID-19) ili kulinda nguvukazi ya Taifa letu. Maendeleo ya viwanda na biashara na ufungamanishi wa uchumi kwa ujumla wake unahitaji kushirikisha rasilimali zenye ubora ikiwemo nguvukazi yenye afya. Hivyo, nawaomba sana Watanzania wote kuwa kila mmoja, kila familia na jumuiya zote nchini kutambua kuwa usalama wetu hutegemea jitihada ya kila mmoja kujilinda na kumlinda mwenzake. Kwa kufanya hivyo, tunatoa uhakika kwa Watanzania wote kuwa wanufaika wa uhakika wa matunda ya jitihada za ujenzi wa uchumi wa viwanda unaojengwa kwa nguvu zote.

10. ***Mheshimiwa Spika;*** Baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa nijielekeze katika kuelezea Mchango wa Sekta ya Viwanda na Biashara ukifuatiwa na Mafanikio Makuu ya

Sekta; Mapitio ya Bajeti na Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2019/2020; Mwelekeo wa Sekta ya Viwanda na Biashara; na kisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka 2020/2021.

## 2. MCHANGO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KATIKA UCHUMI

### 2.1. *Sekta ya Viwanda.*

11.***Mheshimiwa Spika;*** Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kwa mwaka 2019 ulikuwa asilimia 8.5 ikilinganishwa na asilimia 8.05 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 0.45. Mchango huo ni matokeo ya kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji viwandani katika kipindi hicho (Kiambatisho Na.1). Vilevile, Kasi ya ukuaji wa thamani ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani kwa mwaka 2019 ilikuwa ni Shilingi Trilioni 10.2 ikilinganishwa na Shilingi Trilioni 9.6 mwaka 2018, sawa na kasi ya ukuaji wa asilimia 5.8 (Kiambatisho Na. 2). Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

12.***Mheshimiwa Spika;*** Mchango wa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo katika Pato la Taifa ni asilimia 35 na Sekta hii imeajiri zaidi ya Watanzania milioni tisa ikiwa ni ya pili katika sekta za kiuchumi katika kutoa ajira ikiifuatia Sekta ya Kilimo.

### 2.2. *Sekta ya Biashara*

13. ***Mheshimiwa Spika;*** Shughuli za Biashara ya jumla na rejareja zimechangia asilimia 8.8 kwenye Pato la Taifa kwa mwaka 2019 ikiwa ni moja kati ya sekta tatu zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa.

## 3. MAFANIKIO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KATIKA AWAMU YA TANO

14. ***Mheshimiwa Spika;*** Ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini ni jukumu jumuisha na shirikishi linalohusisha sekta mbalimbali za uchumi ambazo zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Hivyo, sekta hizo hutekeleza mipango jumuishi katika kujenga uchumi wa viwanda kwa kutumia rasilimali za fedha za Bajeti ya Serikali kwa kujenga miundombinu ya msingi na wezeshi ikiwemo miundombinu ya barabara, maji, umeme na mawasiliano. Aidha, sekta za huduma huchangia katika kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na nguvukazi yenye afya, bora na ujuzi unaohitajika. Pia uwepo wa ulinzi na usalama wa mali na watu hutoa uhakika wa mazingira ya wananchi kujishughulisha katika uzalishaji wa mazao, bidhaa na huduma. Hivi, tunapoangalia mafanikio ya utekelezaji wa Bajeti

ya Sekta ya Viwanda na Biashara na hususan katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, hatuna budi kuangalia kwa ujumla na mapana yake namna Bajeti ya Serikali inavyogharamia mipango ya sekta nyingine ambazo zinajielekeza katika kuchangia utekelezaji wa azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.

15. ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa ujumla wake, Sekta ya Viwanda na Biashara imefanikiwa: Kuongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali muhimu nchini ikiwemo sukari, mafuta ya kula, bidhaa za chuma, saruji na marumaru na hivyo kwa kiasi kikubwa kukidhi mahitaji ya ndani ya nchi; Kuvutia ujenzi wa viwanda vipya nchini na ufufuaji wa viwanda vilivyobinafsishwa; Kuongeza maeneo ya kufanyia kazi wajasiriamali na kuboreshwa kwa maeneo ya uwekezaji; Kuendelea kuimarika mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji kupitia utekelezaji wa *BLUEPRINT*; na Kuimarika kwa taasisi za utafiti na maendeleo ya teknolojia kwa kuboresha maabara zake na utoaji huduma. Pia, Sekta imefanikiwa Kuimarisha udhibiti wa bidhaa na huduma nchini; Kuongezeka uwezo na ujuzi wa rasilimali watu; Kuongezeka kwa uwekezaji na mapato katika viwanda; Kuendelea kujitosheleza katika baadhi ya bidhaa nchini ambazo zilikuwa zikiagizwa kwa wingi kutoka nje; Kuendelea kutoa elimu kwa wajasiriamali; Kuzalishwa kwa teknolojia mbalimbali za kuongeza thamani

mazao hususan za kutumika vijijini zikiwemo za kusindika alizeti, nafaka, matunda; Kuanza kutoa leseni za biashara (Kundi A na B) kwa njia ya kielektroniki na Kutoa mikopo kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa NEDF na kuutunisha. Vilevile, imefanikiwa kuendelea kulinda viwanda na biashara za ndani; Kuimarisha masoko ya mipakani; Kukamilisha baadhi ya majadiliano na kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa ili kupata na kutumia fursa za masoko hayo; Kuendelea kuunganisha wakulima na fursa za masoko; na Kuendelea kutoa taarifa za masoko ya mazao ya chakula, biashara na bidhaa mbalimbali. Aidha, taasisi za sekta zimeweza kutoa gawio lake Serikalini na pia kuchangia katika Bajeti ya Serikali.

### 3.1. Mafanikio katika Sekta ya Viwanda

16. ***Mheshimiwa Spika;*** Sekta ya Viwanda nchini ni miongoni mwa nguzo muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali iliweka nguvu kubwa katika kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2015/16-2020/21 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 – 2020. Utekelezaji huo umehamasisha na kuchochea ujenzi wa uchumi

wa viwanda ili kufikia malengo ya maendeleo ya muda mrefu kama yalivyoanishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Ili kuhakikisha Sekta hiyo inachangia na kuleta tija katika uchumi wa Taifa, juhudi za makusudi zimeendelea kuchukuliwa katika uongezaji thamani wa malighafi za ndani hususan katika Sekta za Kilimo, Uvuvi, Mifugo, Maliasili na Madini. Hatua hizo zinasaidia kuchangia upatikanaji wa ajira; kuongeza uzalishaji na mauzo ya bidhaa ndani na nje ya nchi; na hivyo kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni katika uchumi.

17. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi hicho, msisitizo umewekwa katika ujenzi wa viwanda vipya na kuimarisha viwanda vilivyopo. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na juhudi hizo ni pamoja na uendelezaji na uanzishwaji wa viwanda vya marumaru, saruji, chuma, vinywaji, na matunda, nyama, maziwa, nguo na mavazi, bidhaa za plastiki na ngozi. Kwa muhtasari, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano ni kama ifuatavyo:-

### *i) Uongezaji Thamani wa Mazao*

18. ***Mheshimiwa Spika;*** Kutokana na uhamasishaji unaofanywa na Serikali, uongezaji thamani wa mazao ambayo malighafi zake zinazalishwa kwa wingi nchini umeendelea kuongezeka ambako kumechochewa na kuendelea kwa ujenzi wa viwanda nchini. Kwa mfano, viwanda 8 vya kusindika maziwa vyenye kusindika maziwa vimeongeza uwezo wake kutoka lita 167,620 kwa siku hadi kufikia lita 194,335 kwa siku. Vilevile, viwanda 17 vya nyama vilivyojengwa vimewezesha kuongeza usindikaji wa mazao ya mifugo ambapo zimewezesha Tanzania kuwa na jumla ya viwanda 145 vya usindikaji wa mazao ya mifugo. Viwanda hivyo vinajumuisha viwanda 33 vya nyama, viwanda 99 vya maziwa na viwanda 13 vya kusindika ngozi. Pia, Serikali imewezesha ujenzi wa viwanda vitatu vya kusindika matunda na mbogamboga. Viwanda hivyo ni Kiwanda cha *Elven Agri*, *Sayona Fruits Limited* na *Dabaga*. Aidha, Serikali imewezesha ujenzi wa viwanda vinne vya kusindika vyakula vya *Dar Worth Company Limited* kinachozalisha sembe, dona na unga wa lishe; *Uniliver* cha kusindika Chai; *Murzah Wilmar Rice Millers* cha kusindika Mpunga; na *Mahashree Agroprocessing Tanzania Limited* cha kufungasha mazao jamii ya kunde hususan mbaazi.

### *ii) Ujenzi wa Viwanda Vipya*

19. ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali inaendelea kuhamasisha uendelezaji na ujenzi wa viwanda nchini. Kutokana na jitihada hizo, jumla ya viwanda vipya 8,477 vimeanzishwa nchini kati ya mwaka 2015 hadi 2019. Viwanda hivyo vipya vinajumuisha viwanda 201 vikubwa, 460 vya kati, 3,406 vidogo; na 4,410 vidogo sana. Mfano wa viwanda katika Sekta ya Ujenzi ni *Kilimanjaro Cement, Fujian Hexingwang Industry Co. Ltd* na *KEDA Ceramic ltd*; Sekta ya Dawa na Vifaa Tiba ni *Kairuki Pharmaceautical Industry* na *Zesta Pharmaceautical Industry*); Sekta ya Chakula na Vinywaji ni *21st Century Food processing Industry na Sayona Fruits Ltd*; na Sekta ya Vifaa vya Umeme ni *Inhemeter Co. Ltd* na *Europe Inc. Industry*.

### *iii) Ajira katika Sekta ya Uzalishaji*

20. ***Mheshimiwa Spika;*** Ajira katika Sekta za Uzalishaji zimeongezeka kutoka ajira 254,786 mwaka 2015 hadi kufikia ajira 306,180 mwaka 2018, ikiwa ni ongezeko la asilimia 20.2. Ongezeko hilo lilitokana na ujenzi wa viwanda vipya na upanuzi wa viwanda vilivyopo ikiwemo; Kiwanda cha *Goodwill Ceramic Ltd, KEDA* (Twyford), *Sayona Fruits Ltd* (Chalinze), *Sayona Drinks Ltd* (Mwanza), *Kiluwa Steel Ltd* (Mlandizi),

*Fujian Hexing Wang Industry Co. Ltd* (Mkuranga), *Global Packaging Ltd* (Kibaha), *Europe Inc. Co. Ltd* (Dar es Salaam), na *Azam Fruits Processing Ltd* (Mkuranga). Inatarajiwa kuwa, kwa mwenendo huo viwanda hivyo vitazalisha takribani ajira 370,478 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2020.

### *iv) Kujitosheleza kwa Mahitaji ya Ndani kwa Baadhi ya Bidhaa za Viwandani*

21. ***Mheshimiwa Spika;*** Nchi imejitosheleza katika baadhi ya bidhaa muhimu zinazozalishwa nchini zikiwemo: saruji, marumaru, nondo, mabati na vifaa vya umeme. Matokeo hayo yamefikiwa kutokana na jitihada za Wizara za kuhamasisha wawekezaji kujenga viwanda vipya pamoja na upanuzi wa viwanda vya zamani. Kwa mfano, upanuzi wa viwanda vya saruji vya Tanga *Cement* Ltd na Mbeya *Cement* Ltd na kuanza kwa uzalishaji wa viwanda vipya kikiwemo Kiwanda cha *Kilimanjaro Cement* Ltd cha mjini Tanga kilichoanza kazi mwaka 2017 umewezesha kuongezeka kwa uwezo wa uzalishaji saruji (installed production capacity) hadi kufikia tani milioni 9.1 kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na tani milioni 4.7 mwaka 2015. Uzalishaji halisi (actual production capacity) ni tani milioni 7.4 ambapo mahitaji halisi nchini ni tani milioni 4.8. Hii inamaanisha kuwa viwanda hivyo vinazalisha ziada ya tani milioni 2.6

ambazo huuzwa nje ya nchi zikiwemo Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, DRC Congo na Msumbiji.

22. ***Mheshimiwa Spika;*** Kutokana na jitihada za Serikali za kuhamasisha uwekezaji wa viwanda, ujenzi wa viwanda vikubwa viwili vya marumaru vya *Goodwill (T) Ceramic Co. Ltd* na *KEDA (T) Ceramic Co. Ltd* vimeanzishwa. Kiwanda cha *Goodwill (T) Ceramic Co. Ltd* kina uwezo uliosimikwa wa mita za mraba milioni 18 kwa sasa uzalishaji halisi ni mita za mraba Milioni 14.4, na Kiwanda cha *KEDA* uwezo wa uzalishaji ni mita za mraba 28.8 na uzalishaji halisi ni mita za mraba milioni 18.

23. ***Mheshimiwa Spika;*** Uzalishaji wa bidhaa za chuma umeendelea kutosheleza mahitaji ya ndani na umesaidia katika upatikanaji wa malighafi za ujenzi wa miundombinu wezeshi ya viwanda nchini. Viwanda vikubwa vitatu vya chuma vya *Kiluwa Steel* (chenye uwezo wa kuzalisha tani 12,000 kwa mwaka), *Lodhia Steel Industry* chenye uwezo wa kuzalisha tani 3,700 na *Lake Steel and Allied Products Ltd* ambavyo vimeongeza idadi ya viwanda vya chuma nchini na kufikia 25 ni kielelezo cha mafanikio. Kati ya hivyo, viwanda 16 vinazalisha nondo na vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,082,700 kwa mwaka, wakati mahitaji ya nondo nchini kwa mwaka ni tani 295,000.

***v) Uendelezaji Maeneo Maalum ya Uwekezaji***

24. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ, imefanya tafiti tatu zenye dhana ya kufanya tathmini ya tija inayopatikana kutokana na kampuni zilizowekeza chini ya EPZA katika uchumi wa nchi. Matokeo ya tafiti hizo yameonesha uwepo wa tija katika uwekezaji wa maeneo ya SEZ. Kwa mfano, shughuli za uzalishaji zinazotokana na uwekezaji uliofanyika ndani ya BWM-SEZ zimewezesha kupatikana Dola za Marekani 127,641,683 kutokana na mauzo ya nje ya nchi; Matumizi ya wawekezaji ya Dola za Marekani 63,730,000 kwa malipo ya wafanyakazi wa ndani, malighafi, umeme, maji na gharama nyingine za kuendesha biashara; Kodi na Tozo mbalimbali zilizolipwa kupitia TRA za Dola za Marekani 7,497,100.34; na Ajira za moja kwa moja viwandani zipatazo 3,000. Tafiti na tathmini hizo zitaendelea kufanyika kwa nia ya kuboresha ufanisi wa Mamlaka na kukuza mchango wake kwa Taifa.

## 3.2. Mafanikio ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

***i) Kutoa Ajira kwa Watanzania Wengi***

25. ***Mheshimiwa Spika;*** Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imetoa ajira kwa wingi kwa Watanzania ambapo kwa sasa imeajiri

zaidi ya Watanzania milioni nane. Ajira hizo zimewezesha wahusika kujiongezea vipato na kutatua changamoto zao za kijamii na kiuchumi. Pia, imeweza kuongeza chachu katika azma ya ujenzi wa viwanda nchini ambapo takribani asilimia 99 ya viwanda vyote nchini vipo chini ya sekta hiyo. Hivyo, Sekta hiyo ni fungamanisho kubwa katika uchumi wa nchi kwa kuwa inahusisha sekta zote za uchumi. Vilevile, imebeba dhamana ya nchi ya kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo 2025, hasa ikizingatiwa kuwa inashirikisha Watanzania wengi katika shughuli za kiuchumi. Aidha, Viwanda vingi vilivyoanzishwa vimekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza thamani ya malighafi za Tanzania hususan zitokanazo na mazao ya kilimo.

### ***ii) Mitaji kwa Wajasiriamali Wadogo***

26. ***Mheshimiwa Spika;*** Kupitia Sekta hiyo, Wizara imefanikiwa kuchochea uanzishwaji wa shughuli za kiuchumi kwa kutumia mikopo inayotolewa na SIDO chini ya Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi (NEDF). Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi Machi 2020, mtaji wa Mfuko wa NEDF umeongezeka kwa Shilingi Bilioni 2.22 kutoka Shilingi Bilioni 6.429 Machi 2016 hadi Bilioni 8.65. Ongezeko hilo limetokana na riba inayopatikana kutokana na fedha inayojizungusha (Revolving Fund)

kupitia mikopo hiyo. Aidha, jumla ya wajasiriamali 17,654 wakiwemo wanawake 8,933 na wanaume 8,721 walipatiwa mikopo iliyowezesha jumla ya ajira 47,180 kupatikana.

27.***Mheshimiwa Spika;*** Mwezi Februari, 2020 yalisainiwa makubaliano kati ya SIDO, VETA, Azania Bank, NSSF na NEEC ya kuanzisha program ya kutoa mikopo kwa wajasiriamali waliohudumiwa na SIDO na wahitimu wa VETA kupitia Benki ya Azania. Makubaliano hayo yaliyofanyika chini ya uratibu wa Baraza la Uwezeshaji yanatoa nafasi kwa SIDO na VETA kuwapeleka wajasiriamali na wahitimu Benki ya Azania kuomba mikopo ya viwanda ya kuanzia Shilingi Milioni 8 hadi Milioni 500. Fedha zitakazokopeshwa kiasi cha Shilingi Bilioni 5 zimetolewa na NSSF kwa mkopeshaji ambaye ni Benki ya Azania. Program hiyo itaitwa SANVN kuwakilisha taasisi za SIDO, VETA, AZANIA BANK, NSSF na NEEC. Mwezi Aprili, 2020 vikao vya wataalam vilikamilisha Rasimu ya Mwongozo ya Utekelezaji wa Program (SANVN Viwanda Scheme – Lending Manual) na linasubiri uidhinishwe na kusambazwa ndipo utekelezaji wa program uanze.

### *iii) Maeneo ya Shughuli za Uzalishaji kwa Wajasiriamali*

28. ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imefanikiwa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wajasiriamali kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Suala hilo limewezesha ujenzi wa majengo ya viwanda (Industrial Shades) 12 katika Mitaa ya Viwanda ya SIDO iliyopo mikoa ya Dodoma (3), Manyara (3), Kagera (1), Mtwara (1) na Geita (4). Jumla ya viwanda 29 vimeweza kusimikwa katika majengo hayo ambapo ajira 648 zimezalishwa. Aidha, Serikali imefanikisha kusogeza karibu huduma za kusaidia na kuhamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kujenga ofisi nne za SIDO katika mikoa mipya ya Simiyu, Katavi na Geita.

## 3.3. Mafanikio katika Sekta ya Biashara

29. ***Mheshimiwa Spika;*** Sekta ya Biashara ni nguzo muhimu katika kuwezesha upatikanaji wa fursa za biashara na masoko kwa bidhaa za Tanzania za kilimo na viwandani kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi. Biashara ni chanzo muhimu cha mapato ya Serikali na huwezesha kutawanya faida zinazopatikana kutokana na shughuli za uzalishaji. Hivyo, biashara hizo huchangia katika kuinua vipato vya wazalishaji

na wafanyabiashara na kuchagiza uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha kuanzia 2015 hadi 2019, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Sera na Mikakati ya biashara na masoko kwa kufanya mapitio ya Sera, Sheria na Taratibu mbalimbali ili ziendane na mahitaji ya Sekta kwa kipindi kilichopo na kijacho. Juhudi hizo ni pamoja na kuendelea kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara nchini, kuendelea kujenga miundombinu ya masoko; na kutafuta fursa nafuu za biashara kupitia majadiliano ya biashara baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa.

30. ***Mheshimiwa Spika*** Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na Kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Dkt. John Pombe Magufuli katika kipindi chake cha Uenyekiti wa SADC kwa kusimamia na kutetea lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha kuu za majadiliano. Kupitia jitihada zake, Mikutano ya SADC sasa inatumia lugha 4 za Kiingereza, Kireno, Kifaransa na Kiswahili. Kwetu sisi hiyo ni hatua kubwa na yenye manufaa kwa nchi katika Mtangamano huo wa Kikanda. Wizara itashirikiana na wadau wengi kuendelea kuuza Lugha ya Kiswahili kama bidhaa duniani kote.

### *i) Mauzo ya Bidhaa na Huduma katika Masoko ya Nje*

31. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha miaka mitano, Sekta ya Biashara imefanikisha kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma kwenye masoko ya kikanda yanayotoa fursa za upendeleo maalum (preferential market access). Tanzania imekuwa na urari chanya wa mauzo ya bidhaa kwenda kwenye masoko ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Mfano, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka mwaka 2015 hadi mwaka 2018, Tanzania imekuwa na urari chanya wa mauzo ya bidhaa kwa wastani wa Dola za Marekani Milioni 288.04. Thamani ya bidhaa zilizoingizwa kutoka nchi za EAC ilishuka kutoka Dola za Marekani Milioni 322.80 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani Milioni 302.93 mwaka 2018. Kukua kwa Sekta ya viwanda nchini kumesababisha kupungua kwa uingizwaji wa bidhaa kutoka EAC na SADC. Matokeo hayo, yametokana na Tanzania kujitosheleza na kuzalisha kwa ushindani bidhaa za saruji, marumaru, vyandarua, baadhi ya bidhaa za chuma kama vile nondo na mabati, mabomba ya plastiki, unga wa ngano na nafaka ikiwemo mahindi na mchele. Aidha, bidhaa zingine zilizouzwa zaidi katika Jumuiya hizo ni pamoja na chai, kahawa, sigara, madawa, vifaa tiba na madini ya *Tanzanite*.

### ii) Biashara katika Masoko ya Nje

32. ***Mheshimiwa Spika;*** Sekta ya Biashara imefanikisha kuendelea kuimarisha mahusiano ya kibiashara na nchi za Umoja wa Ulaya na zile zilizo nje ya Umoja huo. Miongoni mwa nchi hizo ambazo Tanzania imeendelea kujiimarisha kibiashara ni pamoja na nchi za Uswisi, Denmark, Uingereza, Uholanzi, Sweden na Ujerumani. Kwa mfano, mauzo ya Tanzania nchini Uswisi yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 153,933 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani Milioni 257,166 mwaka 2018. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni maua, mapambo, kahawa, chai, viungo, mafuta ya wanyama na mbegu, pamba na madini na vito vya thamani. Aidha, mauzo ya Tanzania yameendelea kuimarika kwenda kwenye nchi nyingine zinazotoa upendeleo maalum wa biashara ikiwemo India, China, Japan, Uturuki na Marekani. Mfano kuongezeka kwa mauzo kwenda nchini India kutoka Dola za Marekani Milioni 20,547 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani Milioni 42,421 mwaka 2018. Bidhaa zilizouzwa zaidi ni kahawa, pamba, chai, tumbaku, samaki na bidhaa za baharini, nguo na mavazi, bidhaa za mikono (handcrafts), na ngozi na bidhaa za ngozi.

### 3.4. Mafanikio ya Sekta ya Masoko

#### *i) Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini*

33. ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imefanikiwa kuendelea na uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini kwa kuandaa na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara Nchini (Blueprint for Regulatory Reform to improve Business Environment). Mpango huo umewezesha maboresho ya tozo 173 ambapo kati ya tozo hizo, tozo 163 zimefutwa na tozo kero 10 zimepunguzwa kiwango. Kati ya tozo zilizofutwa, 114 ni za Sekta ya Kilimo na Mifugo, 5 za OSHA, 44 za TBS, GCLA,Utalii, Maji, Uvuvi na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa-TFDA. Aidha, tozo zilizopunguzwa ni za Mamlaka za Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA). Mpango huo umewezesha kuhamisha jukumu la usimamizi wa masuala ya chakula kutoka iliyokuwa TFDA kwenda TBS, ili kuondoa muingiliano wa majukumu. Maboresho hayo yamesaidia kuondoa urasimu na kupunguza gharama za kufanya biashara. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na kufutwa kwa tozo ni pamoja na ongezeko la usajili wa usalama mahali pa kazi (workplace) 16,457 zilizosajiliwa kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na mahala pa kazi 11,963 zilizosajiliwa kwa mwaka 2018. Aidha, Serikali

inaendelea na maandalizi ya kutunga Sheria ya Uwezeshaji Biashara ya mwaka 2020 (Business Facilitation Act, 2020), ili kuipa nguvu ya kisheria misingi ya maboresho iliyobainishwa katika *Blueprint*. Rasimu ya Waraka wa Sheria hiyo imekwishawasilishwa kwenye ngazi za maamuzi Serikalini.

### *ii)Kudhibiti Upotevu wa Mazao baada ya Mavuno*

34. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Bodi ya Stakabadhi za Ghala imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kujenga miundombinu ya masoko ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ghala katika maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka 2019/2020, ghala zifuatazo zimejengwa na zinatumika kuhifadhi mazao ya kilimo yakiwemo korosho, ufuta, dengu, kakao, mbaazi na choroko. Ghala zilizojengwa zinapatikana katika Wilaya ya Ruangwa Mkoa wa Lindi linalomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Wilaya ya Tunduru Mkoa wa Ruvuma linalomilikiwa na Chama cha Ushirika cha Umoja Amcos Tunduru na Wilaya ya Kondoa Mkoa wa Dodoma linalomilikiwa na Chama cha Ushirika Pabu, Wilaya ya Babati Mkoa wa Manyara linalomilikiwa na Chama cha Ushirika Rivaku. Kutokana na hatua hizo, Serikali imefanikisha kupunguza upotevu wa mazao baada ya

uzalishaji (post harvest loss), kuongeza uhai wa muda wa matumizi wa bidhaa za kilimo (shelf life) na kuweka mfumo wenye uwazi na rahisi kwa wanunuzi.

35. ***Mheshimiwa Spika***; Msimu wa mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Stakabadhi za Ghala inayosimamia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala imesajili jumla ya ghala 51 zenye ujazo wa kati ya Mita za Ujazo 300 hadi 10,000. Jumla ya Kilo 240,218,696 zilihifadhiwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Mikoa ya Ruvuma, Pwani, Lindi, Mtwara, Manyara, Mbeya, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Songwe, Kilimanjaro na Dodoma ***(Kiambatisho Na. 3).*** Juhudi hizo zimesaidia kuongezeka mauzo ya bidhaa kutokana na kukamilika kwa Mfumo wa Mauzo ya Bidhaa kwa Njia ya Kielektroniki wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX). Jumla ya tani 519.89 zimeuzwa kupitia Mfumo huo. Kati ya hizo, tani 431.481 ziliuzwa Wilayani Kondoa, Mkoa wa Dodoma wakati tani 88.41 ziliuzwa Wilaya ya Babati Mkoa wa Manyara. Aidha, Bodi inatarajia kuongeza mazao ya pamba, mahindi, choroko, kahawa, dengu na mbaazi katika Soko la Bidhaa Tanzania (TMX).

### ***iii) Kuimarisha Mifumo ya Uzalishaji na Masoko***

36. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali likiwemo Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Bodi ya Kahawa, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Vyama vya Ushirika imefanikisha kuweka mifumo madhubuti ya uzalishaji na upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo. Vyama vya Ushirika vilivyoshirikishwa ni pamoja na vyama vya Ushirika vya: Kagera (KCU); Karagwe (KDCU); na Ngara (NCU). Aidha, wadau hao wamesaidia kuongeza uwazi na ushindani wa soko ambao umeendelea kuimarisha bei za mazao na kuleta manufaa kwa wakulima.

### ***iv) Vituo vya Mipakani***

37. ***Mheshimiwa Spika;*** Tanzania imeendelea kutumia fursa yake ya kijiografia (strategic geographical location) kupanua wigo wa fursa za biashara na masoko kati ya Tanzania na nchi jirani. Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali imewezesha kuanzishwa kwa vituo 8. Vituo hivyo ni-: Holili/Taveta (Tanzania na Kenya); Sirari/Isebania (Tanzania na Kenya); Namanga/Namanga (Tanzania na Kenya); Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi); Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda); Mutukula/Mtukula (Tanzania na Uganda);

Horohoro/Lungalunga (Tanzania na Kenya); na Kituo cha Tunduma/Nakonde (Tanzania na Zambia). Aidha, kituo kimoja kipya cha Kasumulo/Songwe (Tanzania na Malawi) kipo katika hatua ya ujenzi ambapo kikikamilika kitahudumia mpaka kati ya Tanzania na Malawi.

### *vi) Mfumo wa Usajili wa Shughuli za Biashara kwa Njia ya Mtandao*

38. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanikisha kuongezeka kwa uanzishwaji na ufanyaji biashara nchini kutokana na kurahisisishwa kwa taratibu za kusajili biashara nchini. Hatua ambazo Serikali imechukua ni kuboresha na kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Usajili wa Majina ya Biashara, Makampuni, Alama za Biashara na Huduma, Hataza, Leseni za Viwanda na Leseni za Biashara kwa njia ya mtandao (Online Registration System-ORS) kupitia tovuti ya BRELA (*www.brela.go.tz),* na Dirisha la Taifa la Biashara (National Business Portal - NBP). Hadi kufikia Machi, 2020, Wakala imesajili Makampuni 7,549, Majina ya Biashara 12,627, Alama za Biashara na Huduma 1,970, Hataza 55, Leseni za Viwanda 200 na Leseni za Biashara 9,927.

### *v) Kuhuisha Soko la Biashara ya Zao la Tumbaku*

39. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanikiwa kuhuisha soko la zao la Sekta ya Tumbaku baada ya Serikali kufikia muafaka na wanunuzi wakuu wa zao hilo kuhusiana na madai ya ukiukwaji wa taratibu za ushindani. Hadi sasa kampuni ya *JTI Leaf Services Limited* katika Mpango wake wa ununuzi imethibitisha kununua tumbaku yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 12.6 kwa mwaka 2019/2020, Dola za Marekani milioni 14.1 kwa mwaka 2020/2021, Dola za Marekani milioni 15 kwa mwaka 2021/2022 na Dola za Marekani milioni 15.5 kwa mwaka 2022/2023. Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeendelea kufanyia kazi jumla ya mashauri tisa (9) yanayohusu makubaliano yanayofifisha ushindani (5), miunganiko ya kampuni yaliyofanyika bila kutoa taarifa kwa Tume (2), makubaliano ya siri (1) na matumizi mabaya ya nguvu (abuse of dominance) (1). Katika mashauri yanahusu makubaliano yanayofifisha ushindani (Anti-Competitive Agreements) kutoka katika sekta ndogo ya Tumbaku, Tume imeendelea kufanya majadiliano na mmoja wa watuhumiwa aliyeomba kumalizika kwa shauri lake kwa njia ya suluhu (settlement proceeding). Aidha, Tume inaendelea kufanya uchambuzi wa utetezi wa kimaandishi wa watuhumiwa katika mashauri

yaliyobaki katika mashauri yanayohusu matumizi mabaya ya nguvu za soko (Abuse of Dominance) kutoka katika Sekta Ndogo za Kufukiza (fumigation) na Sekta ya Saruji, Tume imeandaa rasimu ya maamuzi ya awali (provisional findings) kwa shauri kutoka Sekta Ndogo ya Kufukiza. Tume inaendelea kufanya uchunguzi kwa shauri kutoka Sekta Ndogo ya Saruji.

## 4. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020

### 4.1. *Bajeti Iliyoidhinishwa na Kupokelewa kwa Mwaka 2019/2020*

40. ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa ujumla Sekta ya Viwanda ni Mtambuka ambapo utekelezaji wake hutegemea sekta nyingine za uzalishaji wa malighafi kama Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Pia, Sekta zinazosimamia upatikanaji wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda kama vile Sekta za: Ujenzi; Nishati; Maji; na Usafirishaji. Kutokana na umuhimu wa Sekta hizo katika kuendeleza na kukuza Sekta ya Viwanda Nchini, Serikali katika kipindi cha miaka mitano imewekeza rasilimali nyingi katika sekta hizo ikiwa ni jitihada za kuweka msingi bora wa kuendeleza Sekta ya Viwanda nchini.

41. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2019/2020, Wizara (Fungu 44 & 60) iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shilingi 100,384,738,648. Kati ya hizo, Shilingi 51,500,000,000 ni za Matumizi ya Maendeleo na Shilingi 48,884,738,648 za Matumizi ya Kawaida. Aidha, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya Shilingi 14,300,000 (inayojumuisha Fungu 44 Shilingi 5,300,000 na Fungu 60 Shilingi 9,000,000) kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2020, Wizara haikufanikiwa kukusanya kiasi chochote kutoka vyanzo hivyo. Pia, hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 33,812,276,737.40 ambazo ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Wizara haikupata fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

## ***4.2. Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti kwa Mwaka 2019/2020***

### ***4.2.1.*** **Sekta ya Viwanda**

#### ***i) Usajili wa Viwanda Vipya***

42. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2019/2020, jumla miradi mipya 303 imesajiliwa. Kati ya hiyo, miradi 95 ilisajiliwa chini ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), leseni za viwanda 177 (vikubwa 138 na vidogo 39) zilitolewa na

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) pamoja na viwanda 25 vilivyopewa leseni za muda vimepewa leseni za kudumu na miradi sita (6) ilisajiliwa chini ya Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa kwa Mauzo ya Nje (EPZA).

### *ii) Ulinzi wa Viwanda vya Ndani*

43. ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kuvilinda viwanda vya ndani kwa kuhakikisha vinapata malighafi ya kutosha kwa kutoza ushuru mkubwa, kuweka katazo kwa baadhi ya malighafi kwenda nje ya nchi na kutoa vibali maalum kwa baadhi ya bidhaa. Kwa mfano, Serikali imeweka:- Ushuru mkubwa kwenye malighafi ya ngozi, korosho, mafuta ghafi ya kula na mchuzi wa zabibu; Katazo kwa baadhi ya malighafi kwenda nje ya nchi kama vile chuma chakavu (steel scrap metal); na vibali maalum kwa maziwa ya mtindi, sukari na *clinker*. Lengo la jitihada hizo ni kuhamasisha uwekezaji kwenye Sekta ya Viwanda vinavyozalisha ajira nyingi katika mnyororo mzima wa thamani. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority-TRA), na vyombo vya ulinzi na usalama vinahakikisha kuwa bidhaa zinazoingia nchini zinalipa ushuru stahiki ili kuwa na ushindani ulio wa haki sokoni. Hii ni

pamoja na kuimarisha ulinzi wa mipaka yetu ili kuhakikisha kuwa hakuna bidhaa zinazopita njia za panya.

44. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Taasisi zake, imekuwa ikichukua hatua kadhaa katika kulinda viwanda na wafanyabiashara nchini. Kwanza, kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingizwa nchini zinakidhi viwango vya ubora. Bidhaa ambazo hazikidhi viwango hurudishwa au kuteketezwa kulingana na taratibu za kisheria. Pili, kulinda alama na nembo za bidhaa dhidi ya wafanyabiashara wadanganyifu wanaogushi au kutumia bila ridhaa ya mmiliki. FCC, kupitia Sheria ya Ushindani 2003, wanazuia mienendo na vitendo vinavyofifisha ushindani katika soko na hivyo, kuwapa wenye viwanda na Sekta Binafsi kwa ujumla imani ya kuwekeza na kufanya biashara zao bila kuathirika na wafanyabiashara wadanganyifu. Tatu, kutoza kodi kwenye bidhaa zinazoingizwa nchini katika kiwango cha asilimia 10 kwa bidhaa ghafi na asilimia 25 kwa bidhaa zilizo tayari kutumiwa na mlaji. Aidha, viwango hivi vinaweza kutozwa kwa asilimia zaidi ya 25 kulingana na umuhimu wa bidhaa husika.

### ***iii) Uendelezaji wa Viwanda Vilivyo binafsishwa***

45. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kufuatilia viwanda vilivyobinafsishwa, Wizara kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina imekuwa ikifuatilia utendaji kazi katika viwanda vilivyobinafsishwa ambapo kati ya viwanda 156 na Shirika moja vilivyofanyiwa tathmini, viwanda 88 vinafanya kazi na viwanda 68 havifanyi kazi. Kati ya viwanda 68 ambavyo havifanyi kazi, viwanda vitatu vimefanyiwa maboresho ili kuendelea na uzalishaji; viwanda 30 vinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo; ukosefu wa mitaji ya uendeshaji; uchakavu wa mitambo na mashine; uchakavu wa majengo ya viwanda; uvamizi wa maeneo ya viwanda kutoka kwa jamii inayozunguka viwanda; na matumizi ya teknolojia zilizopitwa na wakati. Serikali inaendelea kuvifuatilia viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo vilikuwa havifanyi kazi vizuri na vinahusu mazao ya kimkakati (mfano Kiwanda cha Chai Mponde)ili viweze kuzalisha kwa tija. Aidha, tararibu za kisheria za utwaaji rasmi wa viwanda ambavyo vimetelekezwa bila kuendelezwa kwa muda mrefu zinaendelelea ili viweze kutangazwa tena kwa ajili ya uwekezaji na kuendelea kuzalisha.

### *iv) Uendelezaji wa Viwanda ambavyo Havikubinafsishwa*

46. ***Mheshimiwa Spika***; Viwanda 7 ambavyo havikubinafsishwa kutokana na sababu mbalimbali vimeendelea kuwa mali ya umma chini ya Msajili wa Hazina. Aidha, kati ya viwanda vinne vilivyokabidhiwa kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, viwanda vitatu (3) katika mikoa ya Iringa, Arusha na Dodoma. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea kutafuta wawekezaji wapya wenye nia ya kuwekeza kwa maslahi mapana ya maendeleo ya nchi yetu.

### *v) Uendelezaji wa Viwanda Vinavyomilikiwa na Serikali*

#### *a) Kiwanda cha Viuadudu Kibaha*

47. ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali inamiliki Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kwa asilimia 100 kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC). Kiwanda hicho kina uwezo wa kutengeneza lita milioni 6 za dawa ya viuadudu aina ya *Bactivec* na *Griselef* kwa mwaka. Hadi sasa, Kiwanda kimetengeneza lita 677,000 za viuadudu kwa ajili ya kuua viluilui wa aina mbalimbali za mbu hususan wanaoeneza Malaria. Kiwanda hicho ni mahsusi kwa ajili ya kuunga mkono jitihada za kupambana na ugonjwa wa Malaria nchini. Aidha, Kiwanda

kimefanya mauzo ya dawa za viuadudu kwa soko la ndani na nje ambapo, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kupitia Halmashauri mbalimbali nchini zimekuwa zikinunua dawa kutoka kiwandani kwa nyakati tofauti. Vilevile, nchi za SADC mfano, Angola zimenunua lita 106,000. Hivyo, jumla ya mauzo ya ndani na nje ni takribani lita 500,000. Hata hivyo, Kiwanda kinaendelea na uzalishaji wa dawa kadri ya mahitaji yanavyojitokeza. Hivi karibuni kiwanda kimeingia mkataba wa kuuza Lita 45,785.67 za viuadudu nchini Kenya, zenye thamani ya Dola za Marekani 231,619.44. Sambamba na hilo, NDC kwa kushirikiana na wadau mbalimbali linaendelea kukisaidia Kiwanda kukamilisha taratibu za usajili wa dawa ya kibaiolojia kwa ajili ya kuua wadudu waharibifu kwenye zao la pamba ili kupanua wigo wa kibiashara.

### *b) Mradi wa Matrekta Aina ya URSUS*

48. ***Mheshimiwa Spika;*** NDC imeendelea kuunganisha matrekta aina ya URSUS na zana zake na ujenzi wa kiwanda kipya cha kuunganisha matrekta katika eneo la TAMCO Kibaha. Hadi kufikia Machi, 2020 jumla ya matrekta 822 yalikuwa yamepokelewa kutoka nchini Poland na kuunganishwa. Kati ya hayo, matrekta 724, majembe ya kulimia 511 na majembe ya kusawazisha 233 yalikuwa yameuzwa katika mikoa mbalimbali nchini. Hivi

sasa, ujenzi wa jengo jipya la kiwanda umekamilika na kazi inayotarajiwa kufanyika ni ufungaji wa mitambo mara baada ya kutolewa bandarini.

### *vi) Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji*

49. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ imeendelea kusimamia uendelezaji wa eneo la *Kurasini Trade and Logistic Centre* ambapo imefanikiwa kupata Hati Miliki ya eneo la Mradi mwezi Desemba, 2019. EPZA imepokea mahitaji (specifications) kutoka Bodi ya Chai (TBT), Bodi ya Kahawa (TCB), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) kwa ajili ya uwekezaji ambao utakidhi uendeshaji wa shughuli za kuchakata, kufungasha na kuhifadhi mazao ya kilimo kwa ajili ya mauzo kwenda nchi za nje. Usimamizi wa uendelezaji wa Mradi utaendelea kufanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

50. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ imekua ikihamasisha ushiriki wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uendelezaji wa Maeneo ya SEZ ili kuiwezesha Mikoa husika kutumia Maeneo ya SEZ kama chanzo cha mapato na mbinu mojawapo ya

kuchochea shughuli za kiuchumi katika mikoa husika. Katika Mkakati huo, Mikoa imekua ikihamasishwa kushiriki katika kutenga, kumiliki na kuendeleza maeneo ya SEZ kupitia mafunzo ya uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi yanayotolewa na EPZA. Hadi sasa, mafanikio yamepatikana katika mikoa ya Arusha, Geita, Mwanza, Kigoma na Songwe ambayo imekwisha pokea mafunzo na imetenga maeneo yatakayoendelezwa kama Maeneo Maalum ya Kiuchumi.

51. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ imeendelea na juhudi za kusimamia maendeleo ya SEZ. Mara baada ya eneo kuwa limeendelezwa, shughuli kubwa ya usimamizi inahusisha jukumu la kuhamasisha uwekezaji katika maeneo ya SEZ ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Uhamasishaji huo umechochea na kuvutia uwekezaji na usajili wa leseni za uwekezaji ambapo katika kipindi cha mwaka 2019/2020 EPZA imesajili kampuni sita. Ongezeko hilo limewezesha jumla ya uwekezaji uliopo katika viwanda vilivyo chini ya EPZA kuongezeka kutoka viwanda 163 hadi viwanda 169 vikichangia ongezeko la mtaji unaokadiriwa kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.353 hadi Dola za Marekani Bilioni 2.379. Mauzo ya nje yanakadiriwa kuongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.247 hadi takriban Dola za

Marekani Bilioni 2.266 na fursa za ajira za moja kwa moja kutoka 56,442 hadi 57,342.

### ***vii) Kutoa Huduma za Kitaalam Viwandani***

52. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TIRDO imeendelea kuwa Mshauri Elekezi katika mradi wa ujenzi wa kiwanda kikubwa cha *Karanga Leather Industries* kilichopo Moshi cha kuzalisha bidhaa za ngozi kama vile; viatu, mikanda, soli za viatu, mikoba, mabegi na mipira ya ngozi pamoja na kuongeza thamani katika ngozi kwa ajili ya uuzwaji nje ya nchi. Kiwanda hicho cha ubia kati ya PSSSF na Jeshi la Magereza kitakuwa na uwezo wa kuzalisha jozi za viatu 2,800 kwa siku kwa mwaka wa kwanza hadi kufikia jozi 8,000 kwa siku baada ya miaka mitano. Katika awamu ya kwanza ujenzi wa Kiwanda umefikia asilimia 94. Pia, TIRDO imeendelea kuwa Mshauri Elekezi katika ujenzi wa kiwanda cha vifaa tiba kutokana na zao la pamba kitakachojengwa katika Mmkoa wa Simiyu kwa uwekezaji wa NHIF na WCF.

53. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TIRDO imefanikiwa kuhakiki ubora wa sampuli za bidhaa mbalimbali za chakula na maji zipatazo 174 kutoka viwandani, wajasiriamali na kampuni mbalimbali hapa nchini. Viwanda hivyo ni pamoja na *Masasi Food Industries, Kilimanjaro Natureripe, Darsh Company, Njombe Vegetable*

*processing facility*. Taasisi za kiserikali kama Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) pia wameweza kuhudumiwa na maabara hiyo. Vilevile, wazalishaji wa bidhaa za mifugo kama vile *Kiliagro & Livestock Products* na *Rulenge Agricultural Products Co Ltd* wameweza kuhakikiwa bidhaa zao za nyama ya kuku na nguruwe kwa ajili ya kupata uhakika wa ubora. Aidha, TIRDO imefanikiwa kutoa mafunzo ya uzalishaji chumvi yenye ubora unaokidhi viwango vya ubora vya nchi yetu na vya kimataifa kwa wazalishaji wa chumvi wa jumuiya ya uzalishaji na mashamba ya chumvi Wawi- Pemba.

54. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TIRDO, imefanikiwa kutoa huduma za ukaguzi wa mazingira ili kupunguza uharibifu wa mazingira katika viwanda vinavyozalisha bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na upimaji wa kiwango cha uchafuzi wa hewa, maji, udongo na kubaini kelele hatarishi. Viwanda na taasisi zilizopata huduma hizo ni pamoja na *Kilimanjaro Biochem Ltd, Serengeti Breweries Ltd, Huatan Investment,* na TANESCO (Mtwara Gas Power Plant pamoja na Kinyerezi Gas Power Plant). Vilevile, Viwanja vya Ndege vya Arusha na Bukoba vilinufaika na huduma hizo.

55. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuendelea kuvisaidia viwanda na mamlaka za maji kupunguza gharama za uendeshaji kupitia ufanisi wa matumizi ya nishati ya umeme, Wizara kupitia TIRDO imetoa ushauri kupitia tathmini za matumizi ya nishati. Kwa mfano, Mamlaka ya Maji Safi na Taka ya Tanga walipatiwa huduma hiyo. Aidha, majadiliano yanaendelea na Mamlaka ya Maji Safi na Taka ya Chalinze ili kuwapatia huduma hiyo.

### *viii) Uendelezaji wa Teknolojia na Utafiti*

56. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TIRDO imebuni na kutengeneza mashine kwa ajili ya kiwanda cha mfano cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua kilo 300 kwa saa. Hadi sasa, tayari mashine imekamilika kwa asilimia 88. Lengo la Serikali ni kuhakikisha inabangua kiasi kikubwa cha korosho hapa nchini ili kutoa ajira nyingi kwa wananchi na kuhakikisha malighafi zinaongezewa thamani kabla ya kuuzwa nje ya nchi. Vilevile, TIRDO imebuni na kutengeneza mashine kwa ajili ya kiwanda cha mfano cha kuchakata mawese ambapo hadi sasa kazi zilizofanyika kama ifuatavyo: Kufanya tathmini ya malighafi iliyopo Mkoa wa Kigoma, kubaini ubora wa mawese yanayozalishwa, kubaini teknolojia inayotumika kwa sasa na teknolojia mpya inayohitajika na kununua mashine moja ya mfano kwa ajili ya

kuifanyia utafiti utakaowezesha kuanza kutengeneza hapa nchini. TIRDO pia inatekeleza mradi wa ubunifu na usambazaji wa vitofali lishe vya kuzalishia uyoga wenye virutubisho (mushroom substrate blocks).

57. ***Mheshimiwa Spika;*** Kituo cha CAMARTEC kimeendelea kushirikiana na *Intermech Engineering* katika utafiti na ubunifu wa kipandio kinachovutwa na trekta la magurudumu mawili (power tiller). Katika ushirikiano huo, CAMARTEC imefanya majaribio ya kipandio hicho na kuainisha maeneo yanayohitaji kufanyiwa maboresho. Hadi sasa, CAMARTEC inaendelea kuandaa mpango wa kufanya majaribio na maboresho ya teknolojia nyingine. Pia, CAMARTEC imefanikiwa kubuni na kuunda sampuli kifani (Prototypes) na uzalishaji wa mashine kwa ajili ya wateja. Mashine zilizotengenezwa ni Mashine ya kupura na kupepeta alizeti (3); Mashine ya kupukuchua mahindi (2); Mashine ya kupandia (11); Mashine ya kukata majani ya kulisha mifugo iendeshwayo kwa umeme (5); Mashine za kupura mazao mchanganyiko (3); Mashine ya kusaga karanga (1); na Mashine za kufyatua matofali ya udongo saruji.

58. ***Mheshimiwa Spika;*** Kituo cha CAMARTEC kimekamilisha Mradi wa ujenzi wa mtambo wa biogesi wenye mita za ujazo 45

katika Shule ya Genezareth iliyoko Kinyamwenda Singida. Mradi huo unakusudiwa kuzalisha nishati safi ya kupikia, mbolea hai kwa matumizi ya kuotesha mazao shambani kwa ajili ya matumizi ya shule na pia kusaidia kutibu taka zinazozalishwa chooni. Aidha, Kituo kimekamilisha zoezi la uhakiki wa mitambo ya biogesi iliyoripotiwa kujengwa wakati wa utekelezaji wa Programu ya Uenezi wa mitambo ya Biogesi kwa Ngazi ya Kaya Tanzania (TDBP). Zoezi linahusisha mitambo iliyojengwa chini ya Programu ikiwa ni mtekelezaji na pia Watekelezaji Wenza (IPs) wengine watano (5). Katika mwaka 2019/2020, jumla ya mitambo 259 ya TDBP na mitambo 817 ya watekelezaji wenza wa TDBP ilikuwa imehakikiwa.

59. ***Mheshimiwa Spika;*** Kituo cha CAMARTEC kimekamilisha awamu ya tatu ya mafunzo ya ujasiriamali katika Biogesi kwa wanawake vijana 100 wa jamii za kifugaji kutoka Wilayani Ngorongoro. Mafunzo hayo yamejumuisha Biashara katika Sekta ya Biogesi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mitambo ya biogesi na matumizi ya mbolea hai (bioslurry) inayotoka kwenye mtambo wa biogesi. Pia, Kituo kilitoa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima kuhusu teknolojia za kukata na kufunga majani ya malisho ya mifugo zinavyofanya kazi katika Halmashauri ya Meru Wilaya ya Arumeru. Aidha, wakulima zaidi ya 15 wa Mbozi, Mkoani

Songwe walielimishwa namna ya kutumia kipandio (Planter) kikubwa cha mazao mbalimbali kinachovutwa na trekta.

60. ***Mheshimiwa Spika;*** Kituo cha CAMARTEC kimefanya ukarabati wa mitambo ya biogesi iliyojengwa chini ya ufadhili wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika Shule ya St. Bakanja Wilayani Buhigwe, Kigoma na Shule ya Queen of Apostles Wilayani Ushirombo, Mkoani Geita umefanyika na mitambo inafanya kazi vizuri. Aidha, Kituo kimefanya tathimini ya kazi ya marekebisho ya mitambo ya biogesi na mifumo yake yanayohitajika kufanyika kwenye Mradi wa REA kwa maeneo ya Kambi ya JKT Mlale Songea- Ruvuma na Gereza la Namajani lililoko Masasi – Mtwara na kuwasilisha taarifa REA kwa hatua stahiki.

61. ***Mheshimiwa Spika****;* Wizara kupitia TEMDO imeweza kusanifu uundaji wa mtambo wa kuchakata na kukausha muhogo ambapo mpaka sasa asilimia 40 ya utengenezaji na uundaji wa mashine imekamilika.

### ***ix) Uendelezaji wa Miradi ya Kimkakati na ya Kielelezo***

62. Mheshimiwa Spika; Mradi wa Eneo Maalum la Kiuchumi Bagamoyo (Bagamoyo Special Economic Zone Project) ni mradi wa

kielelezo wa Taifa kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2nd FYDP). Kimkakati, mradi unaojumuisha uendelezaji wa eneo la Bandari (Sea Port) kwenye eneo la Hekta 800 na Uendelezaji wa Eneo Maalum la Viwanda (Portside Industrial Zone) kwenye eneo la Hekta 9000. Mradi wa Eneo Maalum la Viwanda litaendelezwa kwa kuhusisha uendelezaji wa eneo la viwanda na uendelezaji wa Kituo cha kisasa cha Technolojia (High Technology Park).

63. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika eneo la Viwanda, Mamlaka ya EPZA imetoa leseni kwa jumla ya Makampuni kumi na moja ili kufanya uwekezaji. Hadi kufikia mwezi Februari 2020, makampuni mawili (Africa Dragon Enterprises Limited na Phiss Tannery Limited) yameanza uzalishaji na makampuni mengine yapo kwenye hatua mbalimbali za uendelezaji. Mchango unaotarajiwa kutokana na makampuni hayo ni kuwekeza mtaji unaokadiriwa kuwa na thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 67.34, ajira za moja kwa moja 1,651 na mauzo ya nje yanakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani milioni 78.56 kwa mwaka. Aidha, Kampuni moja kati ya mawili yaliyoanza uzalishaji (African Dragon Limited), imeshachangia kodi ya Shilingi bilioni 9.86 katika kipindi cha miaka mitatu (2017 – 2019).

64. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika eneo la mradi wa Kituo cha kisasa cha Technolojia (High Technology Park) kwenye eneo la Bagamoyo SEZ, Mamlaka ya EPZ imeingia mkataba wa ushirikiano na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kuendeleza mradi huu katika eneo la hekta 175. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya EPZ inashirikiana na Serikali ya Korea Kusini kupitia program ya 'KSP- Knowledge Sharing Program', inayoratibiwa na Korea Exim Bank yenye lengo la kufadhili uendelezaji wa miundombinu ya mradi.

65. ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa msingi huo, Mradi wa Bagamoyo SEZ unaendelea kutekelezwa katika maeneo ya Eneo Maalum la Viwanda (Portside Industrial Zone) na Kituo cha kisasa cha Technolojia (High Technology Park). Aidha, kuhusu eneo la Bandari (Sea Port), Wawekezaji waliojitokeza wa Kampuni ya Merchants Port Holdings Company Limited (CMPort) ya China na Mfuko wa Hifadhi ya Hazina wa Serikali ya Oman - State General Reserve Fund-SGRF, walishaanza majadiliano na kukubaliana katika baadhi ya masuala. Hata hivyo, kuna masula kadhaa ambayo Serikali imeweka msimamo wake na unahitaji maamuzi ya mwekezaji ili majadiliano yaweze kuendelea.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imejielekeza katika kutekeleza Mradi wa chuma cha Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma. Aidha, tafiti mbalimbali zilibainisha aina ya madini ya chuma (Magnetite Iron Ore) katika mwamba wa Liganga yanahitaji teknolojia maalum ya kuchenjua chuma na mchanganyiko wa madini mengine yakiwepo Vanadium na Titanium ambayo yana thamani kubwa. Mwaka 2010, mwekezaji Sichuan Hangda Group Ltd alipatikana na kuingia Mkataba wa Ubia na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC). Serikali inaangalia njia bora ya kuwezesha mradi huo kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kurejea mikataba ya uwekezaji kwa kuzingatia Sheria Na. 5 ya Mamlaka ya Nchi ya Uangalizi wa Utajiri wa Asili ya mwaka 2017 na Sheria Na. 6 ya Mamlaka ya Nchi juu ya Majadiliano ya Mikataba yenye Masharti hasi ili uwekezaji huo uwe na maslahi mapana kwa nchi.

67. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia TIRDO inaendelea kufanya "Techno Economic Study" katika Mradi wa Magadi Soda Engaruka. Lengo la utafiti huo ni kubainisha kiasi cha mahitaji ya magadi nchini, thamani ya uwekezaji utakaofanyika na faida za mradi huo kwa ujumla. Makadirio ya awali ya rasilimali magadi (brine) yameonesha uwepo wa kiasi cha mita za ujazo Bilioni 4.68. Aidha, ilibanika kuwa rasilimali hiyo inajiongeza

kwa kiasi cha mita za ujazo wa milioni 1.9 kwa mwaka. Uhakiki wa rasilimali hii unaendelea sambamba na ukamilishaji wa upembuzi yakinifu wa mradi na athari ya mradi katika mazingira na jamii. Utafiti huo unategemewa kukamilika mwisho mwa mwezi Aprili, 2020.

68. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia NDC imekamilisha upimaji wa eneo la TAMCO. Jumla ya ekari 201.04 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na miundombinu. Kati ya hizo, ekari 43.04 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kutengeneza madawa ya binadamu; Ekari 55 kwa ajili ya viwanda vya kuunganisha magari; Ekari 94 kwa ajili ya viwanda vya nguo na mavazi; na Ekari 9 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika eneo hilo.

### x) Mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda

69. ***Mheshimiwa Spika;*** Mapitio ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (SIDP, 1996-2020) yanaendelea na tayari Wizara imekamilisha Tathmini na mapitio ya Awali ya Sera hiyo. Kwa sasa Wizara ipo katika hatua ya kuchambua wasilisho hilo ili kuwezesha hatua za tathmini za kina na uchambuzi ili hatimaye kumwezesha Mshauri Mwelekezi kukamilisha uandishi wa *Research Background Paper* na hivyoo kuwezesha maandalizi ya rasimu ya Sera

na Mkakati wake. Utaratibu huo unalenga kuleta ufanisi na kuwa na uratibu unaozingatia mfumo wenye mwongozo wa usimamiaji wa utungaji sera Serikalini. Sera hiyo inategemewa kukamilishwa ndani ya mwaka 2020.

### *xi) Utekelezaji wa Mikakati Mbalimbali ya Uendelezaji Viwanda Nchini*

70. ***Mheshimiwa Spika;*** Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi wa mwaka 2016-2020 umejikita katika kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la Ngozi. Katika kutekeleza mkakati huo, Serikali imetoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye malighafi na vifaa vinavyotumika kutengenezea viatu na bidhaa za ngozi vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi. Lengo likiwa ni kupunguza gharama za uzalishaji kwa viwanda vya ngozi na kuvutia uwekezaji. Fursa hiyo imetumiwa na kiwanda cha *Karanga Leather Industries* ambacho hivi karibuni kimeingiza mashine na vifuasi (accessories). Vilevile, Kiwanda cha *ACE leather* Morogoro kimetumia fursa hiyo kuingiza mashine na vifuasi ili kusindika ngozi hadi hatua ya mwisho**.** Mkakati huo pia umehamasisha taasisi za umma na shule kununua bidhaa za ngozi hususan viatu kutoka viwanda vya ndani kulingana na upatikanaji. Kwa sasa maandalizi ya kuhuisha mkakati huo yanaendelea.

71. ***Mheshimiwa Spika;***. Katika kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mafuta ya Alizeti wa mwaka 2016-2020, Wizara kupitia TEMDO imeweza kutengeneza mtambo(prototype) wa kukamua mafuta (Oil refinery Machine). Hadi sasa mtambo huo umefanyiwa majaribio ya mwisho ili kutengenezwa na kuwapa wadau kama vile SIDO watakaoweza kutengeneza mitambo mingi kibiashara (commercialization). Pia, TEMDO imeendelea kutengeneza kwa majaribio teknolojia zilizokwishahakikiwa na kusambaza teknolojia /mashine ya kukamua mbegu za alizeti kwa wajasiriamali (Sunflower seeds pressing machine/Oil expelling machine).

72. ***Mheshimiwa Spika,*** CAMARTEC imeendelea na utaratibu wa kuhaulisha mashine ya kupura na kupepeta alizeti kwa wajasiriamali wadogo. Lengo ni kuwezesha teknolojia hizo kusambazwa kwa wakulima pamoja na kuwezesha upatikanaji wake kirahisi katika maeneo ambayo zao la alizeti linalimwa kwa wingi hapa nchini. Kwa sasa, Wizara imeanza maandalizi ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa mkakati huo ambao unafikia ukomo mwaka 2020.

73. ***Mheshimiwa Spika;*** Mkakati wa Pamba hadi Mavazi wa mwaka 2016-2020 unalenga uongezaji thamani zao la pamba hadi mavazi

unaochochea uanzishwaji wa viwanda vya nguo na mavazi na vinavyotoa huduma (auxiliary industries). Viwanda hivyo ni pamoja na viwanda vya kutengeneza vifungo, lebo na zipu. Hivi sasa, Wizara imeanza hatua za uhuishaji wa Mkakati huo ambao utekelezaji wake unaishia mwezi Juni, 2020. Katika hatua hizo, mwezi Julai, 2019 Wizara ilifanya tathmini ya sekta hiyo na kubaini kuwa inakabiliwa changamoto mbalimbali zikiwemo tija ndogo katika uzalishaji wa pamba nchini, na teknolojia hafifu katika utengenezaji wa bidhaa mwambata zinazoweza kuzalishwa kutokana na uchambuaji wa pamba mbegu. Tathmini hiyo ni msingi wa kufanya marejeo ya Mkakati huo.

### *xii) Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta ya Mawese*

74. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na wataalam kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuendeleza Viwanda (UNIDO) na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) ilifanya uchambuzi wa mnyororo mzima wa zao la mchikichi. Lengo lilikuwa kubaini changamoto zinazokabili zao hilo, kupendekeza suluhisho na kuwezesha kuchangia katika upatikanaji wa mafuta ya kula nchini. Pamoja na uchambuzi huo, Wizara kupitia taasisi zake za utafiti wa viwanda (TIRDO, CAMARTEC, TEMDO) na SIDO zilifanya

uchambuzi zaidi na kuandaa maandiko (concept papers) ya teknolojia rahisi ya kuchakata chikichi.

### ***xiii) Uongezaji Tija na Ufanisi wa Uzalishaji katika Viwanda***

75. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuimarisha uratibu wa shughuli za KAIZEN, Wizara iliandaa na kukamilisha miongozo ya kufundishia na kutoa huduma za KAIZEN kwa ufanisi (*KAIZEN Consultancy Services & KAIZEN Technical Guideline*). Miongozo hiyo inasaidia kudhibiti ubora wa huduma za KAIZEN zinazofikishwa kwa walengwa. Vilevile, Wizara ilikamilisha maandalizi ya Mpango wa Taifa wa kueneza falsafa ya KAIZEN Nchini *(Framework for Quality and Productivity Improvement (KAIZEN) in Manufacturing Sector – FKM, 2020-2030)*. Mbali na kueneza KAIZEN nchini, mpango huo unahamasisha pia kuoanishwa kwa KAIZEN kwenye uendelezaji wa Kongano za Viwanda ili ziweze kuhimili ushindani.

76. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Wizara imeendesha mafunzo ya uongezaji endelevu wa tija na ubora kwa kutumia falsafa ya KAIZEN. Juhudi hizo ziliwezesha kuongeza idadi ya wakufunzi kutoka 91 hadi 130 watakaosaidia kueneza falsafa hiyo viwandani. Lengo ni kuwezesha viwanda vilivyoko nchini na vile vitakavyoanzishwa viwe na ukuaji endelevu. Aidha, zaidi ya viwanda 102 (asilimia 25 Viwanda vikubwa na asilimia 75 ni

viwanda vidogo) katika mikoa 8 vimenufaika na mafunzo kwa vitendo.

77. ***Mheshimiwa Spika:*** Katika mwaka 2019/2020, Wizara ilifanya tathimini ya hali ya utekelezaji wa Mradi wa KAIZEN. Tathmini hiyo ilibaini yafuatayo:- Kubadilika kwa maeneo ya kazi kuwa yenye staha; Kuongezeka kwa ubora na tija kwa bidhaa kwa viwanda vilivyopata mafunzo; Kuokoa muda wa utendaji kazi (lead time reduction); na Kubadilika kwa mtazamo wa watumishi viwandani katika utendaji kazi kuwa mzuri zaidi. Viwanda vilivyofanyiwa mafunzo viliweza kuokoa takribani Shilingi 368,609,000 kwa kutekeleza falsafa ya KAIZEN ipasavyo katika maeneo yao.

78. ***Mheshimiwa Spika:*** Katika kuhamasisha uenezaji wa falsafa ya KAIZEN nchini, Wizara imeendelea kuratibu Mashindano ya KAIZEN Kitaifa na kushiriki Kimataifa. Katika mashindano ya Kimataifa yaliyofanyika nchini Tunisia mwaka 2019, Tanzania ilipata ushindi wa kwanza kati ya Mataifa 16 yaliyoshiriki. Aidha, katika mashindano ya Kitaifa yaliyofanyika mwezi Februari, 2020 Kiwanda cha *Shelly's Pharmaceuticals* kilipata ushindi wa kwanza kwa viwanda vikubwa na kwa upande wa viwanda vidogo, Kiwanda cha *Tanzania Brush Products Ltd* kilipata ushindi wa kwanza. Navipongeza viwanda hivyo kwa ushindi walioupata, ambapo kupitia ushindi huo

vitaiwakilisha Tanzania kwenye mashindano ya KAIZEN Barani Afrika yatakayofanyika nchini Afrika Kusini mwezi Septemba, 2020. Juhudi hizo zimeipatia Tanzania fursa ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya KAIZEN Barani Afrika kwa mwaka 2021 yatakayohusisha zaidi ya nchi 16. Mashindano hayo yatakuwa ni fursa ya kuvutia wawekezaji, kutangaza vivutio vya utalii na hatimaye kuchangia ukuaji wa uchumi.

### *xiv) Hali ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani*

#### *a) Uzalishaji wa Sukari*

79. ***Mheshimwa Spika;*** Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuwavutia wenye viwanda vya sukari nchini kuwekeza katika kuongeza ukubwa wa mashamba kwa nia ya kuongeza uzalishaji sukari nchini. Hadi sasa, Kiwanda cha *Kagera Sugar* kina mpango wa kuongeza kilimo cha Miwa hekari 14,000 katika shamba la Kitengule ambapo kiwanda kitaongeza uzalishaji wa Sukari kutoka Tani 80,000 za sasa hadi kufikia Tani 180,000 katika kipindi cha miaka 5 ijayo. Vilevile, Kiwanda cha *Mtibwa Sugar* hivi sasa kinaendelea na ujenzi wa mabwawa ambapo utakapokamilika kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 100,000 kutoka 30,000 zinazozalishwa sasa. Aidha, Kiwanda cha *Kilombero Sugar* kipo katika majadiliano na Serikali kwa lengo la kuongeza

uwezo wa uzalishaji. Kupitia Mpango huo, Kiwanda kitaongeza uzalishaji wa Sukari kupitia wakulima wadogo '*Outgrower Scheme*', uzalishaji unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia Tani 265,000 kutoka 120,000 za sasa kwa kipindi cha miaka 5.

80. ***Mheshimwa Spika;*** ili kuongeza uzalishaji zaidi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza ziada nje ya nchi, Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika miradi mipya ya kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari kwa viwanda vikubwa na vidogo. Miradi hiyo ni pamoja: Bagamoyo ambapo kupitia mradi huo tani 35,000 ya Sukari zitazalishwa; na Mradi wa Mkulazi unatarajia kuzalisha tani 50,000. Wawekezaji wengine ambao wapo kwenye hatua ya kuhaulisha maeneo ya ardhi kama vile *Nkusu Theo* ya Ruvuma na *Ray Sugar* ya Mtwara. Wawekezaji kutoka Mauritius kwa ajili ya mradi wa shamba uliopo Rifiji hivi sasa wako kwenye mazungumzo na Serikali. Aidha, Wizara yangu inaendelea kuhamasisha uchakataji wa miwa na kutengeneza sukari kupitia wajasiriamali wadogo na wa kati. Tayari taasisi ya TEMDO inaendelea na kubuni mtambo rahisi kulingana na mazingira yao ili kuwawezesha wajasiriamali hao kuchakata miwa na kutengeneza sukari kwa teknolojia nafuu. Suala hilo litatia chachu jitihada za kukabiliana na tatizo la sukari nchini na kutoa ajira kwa Watanzania kupitia Sekta ya

Viwanda Vidogo ambayo kitakwimu ndio inatoa ajira nyingi nchini.

81. ***Mheshimiwa Spika;*** Makadirio ya uzalishaji wa sukari kwa msimu wa mwaka 2019/2020 yalikuwa tani 345,296 kwa viwanda vya ndani sawa na asilimia 73.46 ya kiasi cha sukari inayokadiriwa kwa matumizi ya kawaida. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 uzalishaji wa sukari nchini, ulikuwa jumla ya tani 298, 949, wakati mahitaji ya sukari kwa mwaka ni wastani wa tani 635,000. Kati ya mahitaji hayo, tani 470,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na tani 165,000 kwa matumizi ya viwandani. Makadirio hayo yametokana na ukweli kwamba kiasi cha mahitaji ya sukari ya matumizi ya kawaida kwa mwezi ni wastani wa tani 38,000.

### ***b) Uzalishaji Dawa na Vifaa Tiba***

82. ***Mheshimiwa Spika***; Sekta ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba ina jumla ya viwanda 14 ambapo viwanda 12 vinatengeneza dawa za binadamu, viwanda viwili dawa za mifugo na kiwanda kimoja kinatengeneza vifaa tiba. Wizara ilichukua hatua za makusudi ili kuhakikisha Sekta hiyo inaongeza uwekezaji kwenye Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba ikiwa ni sambamba na kuongeza ufanisi wa viwanda vilivyopo ili kufikia asilimia 60 ya uzalishaji wa Dawa na Vifaa Tiba Nchini ifikapo Mwaka 2025. Hatua hizo ni:

Kuunda Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia Sekta ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba (NPCC); na Kuweka vivutio vya uwekezaji kwa lengo la kuhamasisha wawekezaji wa ndani na Nje ya Nchi ***(Kiambatisho Na. 4)***.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuvutia wawekezaji katika sekta hiyo, Serikali imefanya yafuatayo: kuondoa VAT kwa vifungashio vya dawa zinazozalishwa nje na ndani ya nchi; kushusha kodi ya mapato kwa asilimia 30 ambayo imesaidia kuhamasisha uwekezaji mpya na upanuzi wa viwanda, kwa muda wa miaka miwili kwa miradi mipya ya viwanda vya dawa; na Kuweka upendeleo maalum kwa ununuzi wa dawa zinazozalishwa na viwanda vya ndani kupitia MSD.

### *xv) Jitihada za Wizara katika Vita Dhidi ya COVID-19*

84. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kukabiliana na janga la ugonjwa wa Covid-19 unaosababisha homa kali ya mapafu, Mwezi Machi 2020, Wizara ilikutana na wazalishaji wa malighafi ya kutengeneza vitakasa mikono (ethanol) na wazalishaji wa bidhaa hizo. Lengo likiwa ni kujadiliana na wenye viwanda pamoja na wadau wengine namna ya kufanikisha utengenezaji na upatikanaji wa vifaa kinga vya kuzuia usambaaji wa ugonjwa huo. Viwanda hivyo vimeitikia wito

wa kuunga mkono Serikali katika vita dhidi ya ugonjwa huo. Kwa mfano Kiwanda cha *Kilombero Sugar Ltd* kinachomilikiwa kwa ubia na Serikali kilichangia jumla ya lita 30,000 za *Ethanol* kwa ajili ya kutengeneza vitakasa mikono ambapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilipewa lita 20,000 na kiasi kilichobaki zilipewa Taasisi za SIDO na TIRDO. Mwitikio huo, umeweza kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kutengeneza barakoa, vitakasa mikono, sabuni za kunawa mikono na *disinfectants,* ili kuongeza upatikanaji wa bidhaa hizo. Hadi sasa, kuna jumla ya viwanda na taasisi 12 ambazo zinatengeneza vifaa tiba kama Barakoa, Vitakasa mikono na mavazi maalum kwa watoa huduma za afya (**Kiambatisho Na 5)**. Aidha, Viwanda vidogo 55 vya nguo na mavazi pia vimeunga mkono kwa kuanza kutengeneza barakoa kwa kutumia malighafi ya kitambaa. Vivyo hivyo, viwanda vya kutengeneza vitakasa mikono vilivyosajiliwa hadi sasa vimefikia 40.

85. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea kufuatilia maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa katika kikao chake na wadau wa Sekta Ndogo ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba Nchini kilichofanyika Jijini Dar es Salaam mwaka 2018. Katika kutekeleza agizo hilo, wawekezaji 11 wanaendelea na ujenzi wa

viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba na ujenzi umefikia hatua mbalimbali kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 6***. Lengo la Serikali ni kuokoa fedha ambazo zinatumika kuagiza dawa na vifaa tiba hivyo nje ya nchi na hivyo kuendelea kutengeneza ajira hapa nchini. Aidha lengo hilo linakusudia kuhakikisha afya za Watanzania zinakuwa ni suala la kipaombele wakati wote.

86. ***Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, Wizara kupitia TIRDO imeweza kutengeneza mtambo unaotumika kuzalisha bioethanol inayotokana na zao la muhogo ambayo inafaa kutumika kwa matumizi mbalimbali ya hospitali, viwanda vya pombe na majiko. Kutokana na *bioethanol* hiyo, TIRDO imeweza kutengeneza kitakasa mikono (sanitizer) ambacho tayari kinatumika kwa wanajamii kwa matumizi ya kujikinga na kuzuia kuenea kwa maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19). Mpaka sasa, TIRDO imeweza kutengeneza lita 202 za vitakasa mikono na kuwafikia watu mbalimbali kwa ajili ya matumizi.

87. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea na kazi ya ufanyaji tathmini ya mahitaji ya vitakasa mikono nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Mkemia Mkuu wa Serikali, Wazalishaji wa *Ethanol*, TMDA na TPMA. Aidha, kupatikana kwa takwimu halisi

kutasaidia Serikali kufanya maamuzi ya haraka hususan ya kuagiza *Ethanol* ambayo ni malighafi muhimu katika kutengenezea vitakasa mikono.

88. ***Mheshimiwa Spika;*** Napenda kuchukua nafasi hii kutoa onyo kwa wafanyabiashara wanaotumia mazingira ya ugonjwa huo kama fursa ya kujinufaisha badala ya kuunga mkono juhudi za Serikali katika kupambana na Janga hili kuacha mara moja vitendo hivyo. Nawasihi wajielekeze katika kulinda afya za wananchi wetu kwani Serikali haitasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya aina hiyo.

### *i) Jitihada za kuwalinda Wakulima Dhidi ya Mifumo ya Kinyonyaji katika Soko*

89. ***Mheshimiwa Spika;*** Kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali anayoingoza kwa namna alivyosimama imara na kuweka msimamo thabiti dhidi ya mifumo ya kumnyonya mkulima katika mazao mbalimbali na hususan korosho na pamba. Wizara itahakikisha kupitia taasisi zake ikiwemo FCC inasimamia maeneo mengine kuharibu mifumo ya aina hiyo iliyowekwa na wafanyabishara wasio waaminifu kwa lengo la kumnyonya mkulima. Mheshimiwa Rais ni mfano wa kuigwa katika utendaji wetu

hasa katika kuhakikisha haki za wakulima na wananchi wanyonge zinalindwa. Na hii inadhihirisha utayari wake katika kuhamasisha wananchi kufanya kazi kwa kujituma na hivyo kuakisi kauli yake ya “HAPA KAZI TU”.

### ii) Kuendeleza Teknolojia za Uongezaji Thamani Mazao ya Kimkakati

90. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuhakikisha Mazao ya kimkakati yanaongezwa thamani, Wizara kupitia taasisi zake za utafiti imeendelea kubuni teknolojia mbalimbali rafiki ambazo zitatumika katika kuongeza thamani ya Mazao ya Kimkakati yaani, Korosho, Chikichi, Mkonge, Zabibu, Miwa kwa ajili ya kutengeneza sukari, mbegu za mafuta hususan alizeti na karanga na Mazao ya Ngozi. Jitihada hizo zinaenda sambamba na utekelezaji wa Mradi wa ASDP II kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Sekta nyingine za uzalishaji katika kuhakikisha kuwa tunaongeza thamani ya mazao hayo kabla ya kuuzwa ili kuhakikisha mkulima anapata soko la uhakika na bei shindani .

### iii) Teknolojia ya Kupura na Kupepeta Alizeti

91. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Kituo cha CAMARTEC inaendelea na utaratibu wa kuhawilisha teknolojia za mashine ya kupura na

kupepeta alizeti kwa *Makau Engineering* ambaye ni mjasiriamali mdogo. Lengo ni kuwezesha teknolojia hiyo iliyobuniwa na CAMARTEC kuweza kusambazwa kwa wakulima na kuwezesha upatikanaji wa teknolojia hiyo kirahisi kutokana na mahitaji yake katika maeneo ambayo zao la alizeti linalimwa kwa wingi hapa nchini. Hivi sasa wakulima wa zao hilo wanatumia mbinu za kizamani ambazo zinabakisha alizeti nyingi kwenye upuraji. Vilevile, mbinu hizo zinapunguza ubora wa alizeti inayovunwa na kumsababishia mkulima hasara.

### ***iv) Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta ya Mawese***

92. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na wataalam kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuendeleza Viwanda (UNIDO) na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) ilifanya uchambuzi wa mnyororo mzima wa zao la mchikichi. Lengo lilikuwa kubaini changamoto zinazokabili zao hilo, kupendekeza suluhisho na kuwezesha kuchangia katika upatikanaji wa mafuta ya kula nchini. Pamoja na uchambuzi huo, Wizara kupitia taasisi zake za utafiti wa viwanda (TIRDO, CAMARTEC, TEMDO) na SIDO zilifanya uchambuzi zaidi na kuandaa maandiko (concept papers) ya teknolojia rahisi ya kuchakata chikichi.

### v) Upatikanaji wa Teknolojia Rahisi za Kuchakata na Kuongeza Thamani Mazao ya Kimkakati kwa Wajasiriamali Wadogo

93. ***Mheshimiwa Spika***; katika kuhakikisha upatikanaji wa Sukari unakuwa wa uhakika na wakutabirika, Wizara kupitia taasisi ya TEMDO inaendelea kubuni mtambo wa kukamua miwa na kutengeneza Sukari kwa ajili ya wajasiriamali wa kati na wadogo. Tayari baadhi ya wajasiriamali wameonesha nia ya kupata teknolojia hiyo pindi itakapokamilika. Suala hilo litasaidia kwa kiasi kikubwa kukabiliana na upungufu wa Sukari nchini na kuongeza ajira kwa kuwa itahamasisha wananchi wengi kujihusisha na kilimo cha miwa.

#### *Upatikanaji wa Teknolojia Rahisi za Kuchakata Mkonge*

94. **Mheshimiwa Spika**; Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea na jitihada za dhati kufufua zao la Mkonge ambalo lilikuwa moja ya mazao ya biashara yaliyokuwa yanaliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni na kuchangamsha uchumi wa Mikoa ya Tanga na Morogoro. Wizara inaenda na kasi hiyo ili kuhakikisha jitihada hizo zinakuwa na faida kubwa kwa mkulima na Taifa kwa ujumla. Hivyo, Wizara kupitia TEMDO iko katika hatua

ya kukamilisha mashine ndogo (Korona) kwa ajili ya kuchakata mkonge. Lengo ni kuwarahisisishia wajasiriamali wadogo kuchakata Mkonge ili kupata nyuzi. Kukamilika kwa mashine hiyo na kusambazwa kwa wajasiriamali itasaidia wakulima kuuza nyuzi badala ya Mkonge ghafi. Utamaduni tuliozoea wa kuuza malighafi ambayo huuzwa kwa bei ya chini ulisababisha kwa kipindi kirefu kuwakatisha tamaa wakulima na kupunguza uzalishaji na wengine kuacha kabisa kilimo cha Mkonge.

### ***Upatikanaji wa Teknolojia Rahisi za Kuchakata Zabibu***

95. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea kuhakikisha zao la zabibu zinapata soko la uhakika ili kuhamamisha ulimaji wa zao hilo. Katika jitihada hizo Bunge kupitia Sheria ya fedha ya mwaka 2019 ilipunguza baadhi ya tozo katika Mvinyo ili kuleta chachu kwa Kampuni kubwa kununua mchuzi wa Zabibu kwa wazalishaji wadogo na wa kati wa mchuzi. Sambamba na hilo, Wizara kupitia TEMDO imebuni teknolojia ya kukamua mchuzi wa zabibu (Grapes Distemer) ambayo ikikamilika itaongeza kasi ya uongezaji thamani zao hilo na hivyo wakulima wadogo kupata soko la uhakika la zao hilo.

***Uendelezaji na Uongezaji Thamani katika Zao la Ngozi***

96. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TIRDO imefanikiwa kutoa mafunzo kwa wafugaji zaidi ya mia mbili (200) katika Halmashauri za Wilaya za Arumeru, Arusha, Longido na Monduli juu ya namna ya kuongeza thamani katika ngozi (Skin and hide value addition) kwa kutumia teknolojia zilizopo hapa nchini ambazo zilikuwa hazijulikani kwa wafugaji. Mafunzo hayo yamesaidia kuongeza thamani kwenye bidhaa za ngozi pamoja na kuwaongezea kipato wafugaji kupitia bei bora za ngozi.

### *4.2.2.* Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

#### *i) Mapitio ya Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo*

97. ***Mheshimiwa Spika****;* Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kufanya marejeo ya Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003. Kwa sasa, Wizara inakamilisha kufanya tafiti katika maeneo mawili ambayo ni *Rural Industrialization* na *Technology and Innovation*. Baada ya kukamilika kwa tafiti hizo uandishi wa Sera hiyo pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wake utaanza.

Wizara inatarajia kukamilisha Sera ifikapo mwishoni mwa mwaka 2020.

### ii) Upatikanaji wa Huduma za Fedha kwa Wajasiriamali

98. ***Mheshimiwa Spika;*** Upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo ni nyenzo muhimu katika kuanzisha na kuendeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi. Wizara, kupitia SIDO imekuwa ikitoa mikopo kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa Wafanyabishara Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund - NEDF). Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 jumla ya mikopo 2,020 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 3.885 ilitolewa kwa wajasiriamali mbalimbali kote nchini. Kati ya mikopo hiyo, asilimia 51.3 ilitototolewa kwa wanawake na asilimia 48.7 ilitolewa kwa wanaume. Aidha, asilimia 39.2 ya mikopo hiyo ilitolewa maeneo ya vijijini na asilimia 60.2, ilitolewa mijini. Mikopo hiyo imekuwa chachu ya uendelezaji viwanda ambapo jumla ya shilingi Bilioni 1.374 zilizokopeshwa ziliwezesha kuanzishwa kwa viwanda 551 na kuwezesha ajira 6,193 kupatikana.

### iii) Uzalishaji na Usambazaji wa Teknolojia

99. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini,

imewasaidia na kuwaendeleza wajasiriamali 42 wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya kupitia programu ya kiatamizi (Incubation Programme). Wajasiriamali hao hupatiwa huduma mbalimbali kama vile maeneo ya kufanyia kazi, mafunzo, ushauri wa kiufundi pamoja na mitaji ili waweze kukua na kufikia viwango vya kujitegemea sambamba na kuzalisha bidhaa bora zenye kukubalika sokoni.

100. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2019/2020, jumla ya teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya 25 yalihudumiwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Mara, Manyara na Tanga. Teknolojia hizo zilihusu utengenezaji wa sabuni, mafuta ya losheni, utengenezaji wa kemikali za viwandani, usindikaji vyakula, uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi, utengenezaji wa mkaa mbadala (briquettes) na utengenezaji wa zana za kilimo. Bidhaa na zana hizo zimeweza kuingia sokoni na kutumiwa na wananchi kadri ya mahitaji yao. Jitihada za uendelezaji teknolojia imejitokeza pia kwa taasisi zetu kuingia katika uzalishaji wa *sanitizer* kama njia ya kupambana na kujilinda na corona. Kupitia wajasiriamali wake, SIDO imetengeneza mtambo wa kutakasa mwili mzima ambao utafaa sana kuwekwa kwenye maeneo ya maofisi, vivuko, stendi za mabasi, vituo vya mipakani, nk. UNDP kwa

kuona jitihada na nguvu hizo imeonesha *interest* ya kununua kati ya mitambo 50 na 100 ili iweze kutumika kwenye maeneo mbali mbali ya umma.

101. ***Mheshimiwa Spika;*** Karakana zilizoko katika Ofisi za SIDO mikoani ziliweza kutambua au kuzalisha jumla ya teknolojia mpya 272 na kusambaza kwa wajasiriamali. Teknolojia hizo zilihusu ubanguaji wa korosho, usindikaji wa mihogo, ukamuaji wa mafuta ya mawese, usindikaji na ufungashaji wa vyakula mbalimbali, utengenezaji wa sabuni na vitakasa mikono, usindikaji wa ngozi na utengenezaji wa chaki, usindikaji wa asali, mitambo ya kuvunia mpunga, mahindi na mtama, mashine za kuchakata tangawizi, kutengeneza misumari na mashine za kutengeneza vyakula vya mifugo kwa kutaja maeneo machache ya teknolojia hizo. Teknolojia hizo zimeweza kurahisisha kazi kwa wakulima na zile za matumizi ya moja kwa moja zimeingia sokoni na kutumiwa na wananchi.

### *iv) Uendelezaji Maeneo na Majengo ya Uwekezaji wa Wajasiriamali kuendeleza Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo*

102. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia SIDO imeendelea kupanua huduma za upatikanaji wa maeneo ya uzalishaji bidhaa kwa wajasiriamali ambapo mwezi Juni mwaka 2019

Wizara ilipokea Shilingi Bilioni moja toka Bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa ajili ya ujenzi wa majengo viwanda (industrial sheds) katika mikoa ya Kigoma, Mtwara na Ruvuma. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 SIDO imekamilisha upembuzi yakinifu wa majengo matatu pamoja na michoro ya usanifu (architectural drawings) katika mikoa ya Mtwara (2) na Kigoma(1) na kuanza ujenzi. Kwa upande wa Mkoa wa Ruvuma, SIDO wamepata kiwanja cha ekari 19.9 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kwa ajili ya ujenzi wa Mtaa wa Viwanda na Ofisi itakayokuwa na kituo cha mafunzo. Ukamilishaji wa majengo viwanda (industrial sheds) unategemewa kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vipya saba vitakavyotengeneza ajira 76.

### *v) Uendelezaji wa Vituo vya Teknolojia*

103. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia SIDO, inamiliki na kusimamia vituo saba vya uendelezaji teknolojia katika mikoa ya Arusha, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya na Shinyanga. Vituo hivyo vimekuwa vikibuni, kutengeneza na kuendeleza teknolojia mbalimbali kulingana na mahitaji ya wajasiriamali katika maeneo hayo kwa kuzingatia mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja (One District One Product – ODOP) na fursa nyingine zinazojitokeza. Vituo hivyo viliweza

kutengeneza jumla ya mashine 268 na kuziuza kwa wajasiriamali.

104. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia SIDO imeendelea kuboresha vituo hivyo vya teknolojia kwa kufanya ukarabati wa mitambo iliyopo na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwa kutumia dhana ya KAIZEN katika uzalishaji ili kuongeza tija. Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni moja mwezi Juni 2019 kutoka katika bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kufanya maboresho katika vituo vya Lindi, Shinyanga na Kigoma kwa kuvinunulia baadhi ya mitambo ya kisasa. Hadi kufika mwezi Machi 2020, tayari vipimo vya mitambo hiyo(specifications) pamoja na gharama zake zimeainishwa. Kwa sasa shirika limeagiza mashine hizo za kisasa (computerized) kutoka kampuni ya *Jiangsu Longshen Machine Manufacturing Co.Ltd* ya China ambapo tayari malipo ya awali yamefanyika.

### ***vi) Utoaji wa Mafunzo na Huduma za Ushauri wa Kiufundi kwa Wajasiriamali***

105. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kiufundi kupitia SIDO hasa katika maeneo ya uthibiti wa ubora wa bidhaa, michoro ya majengo ya viwanda, ufungaji wa mashine,

ukarabati wa mashine, upangaji wa mashine viwandani (equipment layout) pamoja na uchaguzi wa teknolojia sahihi kulingana na aina ya bidhaa inayozalishwa na mjasiriamali. Katika mwaka 2019/2020 jumla ya wajasiriamali 5,145 walipata ushauri wa kiufundi katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Vilevile, SIDO imeendelea kutoa huduma ya mafunzo mbalimbali kwa wajasiriamali ili kuwawezesha kupata ujuzi wa kubuni, kuanzisha na kuendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kupitia ofisi zake zilizoko mikoani shirika lilitoa mafunzo kwa wajasiriamali 12,589 ambapo mafunzo hayo yalijikita katika stadi mbalimbali.

106. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia SIDO imeendelea kuboresha Vituo vya Mafunzo kwa wajasiriamali (Training Cum Production Centres-TPCs) kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo. Katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Mradi wa "Local Investment Climate" (LIC) imefanya ukarabati wa jengo la mafunzo na ofisi katika TPC ya Dodoma ambayo inajihusisha na utoaji wa mafunzo ya uzalishaji bidhaa za ngozi. Aidha, Kupitia Mradi huo kituo hicho cha mafunzo ya bidhaa za ngozi kimenunuliwa mashine na vifaa vya kisasa vya uzalishaji pamoja na vifaa vya kufundishia. Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa vituo vingine vya mafunzo na

uzalishaji (TPCs) vilivyopo katika ofisi za SIDO mikoani.

### *vii)Kuhamasisha Ujenzi wa Viwanda Vidogo Nchini*

107. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda nchini hususan viwanda vidogo na vya kati ambavyo ni rahisi kuanzishwa kutokana na uwepo wa malighafi za kutosha kwa aina hiyo ya viwanda pamoja na kutohitaji mitaji mikubwa katika uanzishwaji wake. Uhamasishaji huo umekuwa ukifanyika kupitia uongezaji wa mitaji kwa wajasiriamali kwa kuwapa mikopo kupitia Skimu ya Ukopeshaji kwa Wajasiriamali (SME Credit Guarantee Scheme-CGS) inayosimamiwa kwa pamoja kati ya SIDO na CRDB. Aidha, kupitia Mfuko wa NEDF unaosimamiwa na SIDO, wajasiriamali wamekuwa wakipatiwa mikopo kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo katika maeneo ya mijini na vijijini. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi 2020 kupitia mifuko hii, jumla ya viwanda vipya 437 vilianzishwa na kutoa ajira 1,481. Viwanda hivyo ni pamoja na vya kusindika nafaka, korosho, mafuta ya alizeti, asali, kutengeneza bidhaa za ngozi, sabuni, chaki, vyakula vya mifugo, ushonaji na useremala.

108. ***Mheshimiwa Spika;*** Sambamba na utoaji mikopo kwa wajasiriamali, Wizara kupitia SIDO imekuwa ikitoa mafunzo na huduma za kiufundi kwa wenye viwanda pamoja na kuwapatia sehemu za kufanyia kazi baadhi ya wajasiriamali wenye mawazo/ubunifu wa teknolojia mbalimbali za uzalishaji mali kupitia programu ya kiatamizi (incubation programme). Huduma hizi zimehamasisha uanzishaji na uendelezaji wa viwanda pamoja na kuongeza tija katika uzalishaji wa bidhaa zenye ubora.

***viii) Kuimarisha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)***

109. ***Mheshimiwa Spika***; Wizara imeendelea kuimarisha SIDO kwa kutoa fursa za mafunzo kwa wataalamu wake kwa kubadilishana ujuzi katika nyanja mbalimbali zikiwemo za teknolojia**.** Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 wafanyakazi wa SIDO waliweza kwenda China, India na kushirikiana na taasisi za ndani vikiwemo vyuo vikuu vya Mbeya, SUA na Dar es Salaam kwa ajili ya kuongeza ujuzi. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha SIDO hususan katika maeneo ya Vituo vyake vya maendeleo ya Teknolojia (TDCs), Ujenzi na uboreshaji miundombinu katika mitaa ya viwanda ya SIDO na utumiaji wa TEHAMA.

### ***4.2.3.*** **Sekta ya Biashara**

***i) Hali ya majadiliano ya Fursa Mbalimbali za Masoko***

110. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kufanya juhudi mbalimbali ili kuimarisha matumizi ya fursa nafuu za biashara zilizopatikana na kutafuta fursa nyingine kupitia majadiliano ya kibiashara. Lengo ni kuhakikisha bidhaa zinazochakatwa viwandani kwa kutumia malighafi nchini, pamoja na huduma kutoka Tanzania zinapata fursa za uhakika za biashara hususan katika masoko ya nje ya nchi. Sambamba na hilo, Wizara imeendelea kuweka utaratibu madhubuti na shirikishi katika kusimamia na kufuatilia uondoaji wa Vikwazo vya Kibiashara Visivyokuwa vya Kiushuru (NTBs). Hatua hiyo imesaidia kupunguza NTBs kadhaa zilizokuwa zikififisha biashara ya bidhaa na huduma za Tanzania; kuimarisha ushirikiano wa wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi Tanzania Bara na Zanzibar wanaohusika na masuala ya kibiashara kwa kuweka utaratibu wa kufanya kazi kwa pamoja kwa lengo la kufungamanisha shughuli za wadau hao; Kuwajengea uwezo na uelewa wa wadau/ wafanyabiashara kuhusu fursa na namna ya kutumia fursa hizo kupitia ziara, makongamano na shughuli nyingine za kibiashara ndani na nje

ya nchi; na kuibua vyanzo mbadala vya fedha na kiufundi kupitia miradi mbalimbali vinavyosaidia juhudi za Serikali za uendelezaji na uwezeshaji biashara. Baadhi ya matokeo ya juhudi hizo yaliyopatikana kabla ya kujitokeza kwa janga la ugonjwa wa COVID-19, ni kuongeza wigo wa fursa za biashara ya bidhaa na huduma baina ya nchi na nchi (bilateral), Kikanda na Kimataifa. Hali hiyo, imewezesha kuimarika kwa urari wa biashara ya Tanzania katika masoko ya nje, hususan EAC na SADC.

111. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara ilishiriki katika Mkutano wa 36 wa Dharura wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Viwanda, Biashara, Fedha na Uwekezaji la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 09 – 13 Septemba 2019 Jijini Arusha Tanzania. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kupitia na kujadili masuala mbalimbali yanayoihusu Jumuiya hiyo ambayo ni pamoja na:- Uandaaji wa Mkakati wa Utekelezaji na Ukuzaji wa Sekta ya Pamba, Nguo na Mavazi; na Mkakati wa Utekelezaji na Ukuzaji wa Sekta ya Ngozi, Bidhaa za Ngozi na Viatu. Masuala mengine yaliyojadiliwa ni kuhusu taarifa ya Mkakati na Mwongozo wa Sera ya uanzishwaji wa viwanda vya uchenjuaji na uongezaji wa thamani wa madini; na Zoezi la Mapitio ya Wigo wa Pamoja wa Forodha wa EAC(*Comprehensive Review of the EAC CET*).

112. ***Mheshimiwa Spika;*** Kupitia mkutano huo, Mawaziri walipitia taarifa ya maendeleo ya zoezi la Mapitio ya Wigo wa Pamoja wa Forodha wa EAC na kuridhia viwango vipya vya wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha (tariff bands) kuwa nne ambazo ni 0%, 10%, 25% na zaidi ya 25%. Hata hivyo, pendekezo la ukomo wa juu wa zaidi ya 25% ambao uliwasilishwa na nchi wanachama wa kutoza kati ya 30% na 35% haukuweza kuridhiwa hadi tarifa muhimu za uchambuzi zitakapowasilishwa. Hivyo, mkutano huo uliagiza ufanyike uchambuzi zaidi ikiwemo kubainisha bidhaa zinazopendekezwa kutozwa ukomo wa juu wa asilimia 30 na asilimia 35 (product mapping) ili hatimaye uchambuzi huo uwasilishwe kwenye kikao kijacho cha Mawaziri kwa ajili ya kufanya maamuzi ya ukomo wa juu.

113. ***Mheshimiwa Spika;*** Pia, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa ngazi ya juu (EAC High-Level Conference) uliofanyika kuanzia tarehe 25 hadi 27, Septemba 2019 jijini Nairobi, Kenya. Lengo kuu la Mkutano huo, lilikuwa ni kujadili masuala mbalimbali katika Jumuiya Masuala hayo ni pamoja na:- Utekelezaji wa Umoja wa Forodha ndani ya Jumuiya (EAC Customs Union); Majadiliano ya uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (African Continental Free Trade Area - AfCFTA); na Masuala ya Vikwazo vya Kiiashara Visivyokuwa

vya Kiushuru (NTBs). Aidha, Mkutano huo ulitoa fursa kwa Nchi Wanachama kujadili changamoto mbalimbali zinazokwamisha utekelezaji wa masuala muhimu ya biashara ndani ya Jumuiya pamoja na kuweka mikakati endelevu ya kuimarisha biashara miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**ii)** ***Majadiliano ya Kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za Afrika (Africa Continental Free Trade Area – AfCFTA)***

114. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara ilishiriki katika Mkutano wa wataalam kutoka nchi wanachama wa EAC tarehe 26 – 27 Agosti, 2019 jijini Arusha. Miongoni mwa malengo ya Mkutano huo yalikuwa ni:- kupitia na kujadili rasimu ya kwanza ya *tariff offer* ya EAC iliyoandaliwa na nchi wanachama; kujadili msimamo wa pamoja wa EAC kwenye masuala ya Uasili wa Bidhaa na kuandaa rasimu ya jedwali la makubaliano ya Biashara ya Huduma kwenye Sekta tano za kipaumbele ambazo ni: Sekta za Biashara; Utalii; Mawasiliano; Fedha; na Uchukuzi, zilizokubalika kwenye majadiliano ya AfCFTA. Masuala mengine yaliyojadiliwa ni pamoja na: Jedwali la pamoja la ufunguaji wa Biashara ya Bidhaa (EAC Schedules of Tariff Concessions); Msimamo wa Jumuiya katika masuala ambayo majadiliano yake

hayajakamilika hususan vigezo vya Uasili wa Bidhaa (Rules of Origin-RoO); Hali ya majadiliano ya Biashara ya Huduma; Kiwango cha kuanzia kufunguliana biashara ya huduma; Uandaaji wa Jedwali la Pamoja la Biashara ya Huduma la EAC; na Ushirikishwaji wa wadau katika kila hatua za majadiliano.

115. ***Mheshimiwa Spika;*** Majadiliano ya kuelekea katika Eneo Huru la Biashara la Afrika bado yanaendelea na tunaamini kuwa yatakuwa na faida kubwa kwa nchi wanachama, hususan kwa nchi zilizojiandaa vyema katika uzalishaji na hivyo kuhitaji kupata masoko mapya ya kuuzia bidhaa zao pamoja na huduma. Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma na binafsi bado inaendelea kufanya utafiti kuhusu faida na hasara pamoja na kuandaa mikakati madhubuti itakayoifanya nchi kuweza kunufaika na Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika. Baadhi ya Mikakati ambayo Wizara inaifanyia kazi hivi sasa ni pamoja na kufanyia Mapitio Sera ya Taifa ya Biashara, Sera ya Maendeleo ya Viwanda, Sera ya SMEs pamoja Sera nyingine mbali mbali ambazo kwa namna moja au nyingine, zitaweza kuifanya nchi kunufaika na mkataba huo. Kukamilika kwa Sera hizo kutasaidia kuvutia Uanzishaji wa Viwanda vipya, kuongeza ajira nchini pamoja na kulinda viwanda vinavyokua dhidi ya ushindani mkubwa kutoka Nje.

116. ***Mheshimiwa Spika;*** Aidha, Mkutano huo ulikubaliana kutumia vigezo vifuatavyo katika kuboresha rasimu ya mapendekezo ya ufunguaji (tariff offer) :-*Tariff offer* iliyopo kwenye Eneo Huru la Biashara la Utatu (COMESA, EAC-SADC Tripartite FTA); *Tariff offer* zinazotumiwa na nchi wanachama ndani SADC na COMESA; Madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na uingizaji wa bidhaa ndani ya Afrika (threats of AfCFTA imports); Kulinda viwanda vinavyokua; Mapendekezo yaliyopo kwenye maboresho ya CET; na Mwenendo wa biashara ndani ya Jumuiya.

117. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kutekeleza maazimio ya Mkutano huo, Wizara ya Fedha na Mipango, ambayo ina jukumu la kusimamia masuala ya fedha/kodi, imeratibu zoezi la kupitia na kuandaa (tariff offer*)* kwa kushirikiana na wadau nchini. Taarifa hiyo inaendelea kufanyiwa kazi kabla ya kuwasilisha msimamo wa Tanzania katika EAC kuhusu suala hilo.

### iii) *Kukamilisha Majadiliano ya Biashara ya Huduma kwa Sekta Sita za Kipaumbele katika Nchi Wanachama wa SADC*

118. ***Mheshimiwa Spika;*** Nchi Wanachama wa SADC zinaendelea na majadiliano yanayolenga kufunguliana fursa

zaidi za biashara hususan kwenye biashara ya huduma. Majadiliano hayo yanafanyika kwa kuzingatia Itifaki ya Biashara ya Huduma ambayo inahimiza nchi hizo kufunguliana biashara ya huduma. Wizara imeratibu vema majadiliano hayo na kupitia Mkutano wa Kamati ya Baraza la Mawaziri wa Biashara wa SADC uliofanyika Windhoek Namibia tarehe 14 Juni, 2019 Nchi Wanachama zilizoridhia Itifaki hiyo ni saba (7) ambazo ni Afrika Kusini, Botswana, Lesotho, Eswatini, Msumbiji, Mauritius na Shelisheli. Nchi nyingine ikiwemo Tanzania, zimesaini na ziko katika hatua mbalimbali za kuridhia Itifaki hiyo. Itifaki hiyo itaanza utekelezaji wake mara baada ya Akidi ya nchi kumi (10) kutimia. Ufunguaji huo unatarajiwa kuchochea biashara na kukuza biashara ya huduma ili kusaidia katika juhudi za uendelezaji wa viwanda kwa kuongeza uwekezaji wa utoaji huduma na hivyo kuongeza fursa za ajira, ufanishi na uhaulishaji wa teknolojia ili kukuza Pato la Taifa.

119. ***Mheshimiwa Spika;*** Nchi za SADC zimeendelea kuhakikisha biashara inaendelea kufanyika katika kipindi hiki ambacho Nchi hizo na Dunia kwa ujumla zinaendelea na mapambano dhidi janga la COVID-19. Katika kutekeleza hilo, SADC imeandaa muongozo ambao uliidhinishwa na Baraza la Mawaziri wa SADC ambao utawezesha biashara hususan

usafirishaji wa mizigo bila kuwa na masharti magumu ili kuwezesha nchi wanachama kuendelea kupata huduma muhimu wakati huu ambao nchi nyingi zimeweka zuio la watu kuingia au kutoka.

### *iv) Kukamilisha Majadiliano ya Kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC*

120. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeshiriki na kutetea maslahi ya nchi katika majadiliano yanayoendelea ya ufunguaji wa Soko la Biashara kwa nchi za Utatu linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC. Kupitia majadiliano hayo, Mkutano wa Wataalam uliofanyika tarehe 16 - 27 Septemba 2020 Nairobi, Kenya pamoja na mambo mengine, ulipitia na kuidhinisha baadhi ya Vigezo vya Uasili wa Bidhaa kwenye Mafuta ya kula, Saruji, Nguo pamoja na Magari. Vilevile, Mkutano ulipitia rasimu ya Mwongozo (Simplified Trade Regime) unaolenga kusaidia wajasiriamali wadogo kufanya biashara ndani ya nchi za utatu. Utaratibu huo, unalenga kuanza kutumika mara moja kabla ya kukamilisha majadiliano kwenye vigezo vya Uasili wa Bidhaa. Mwongozo unapendekeza bidhaa zenye thamani chini ya Dola za Marekani 2,000 ndizo

ziruhusiwe kuuzwa kwenye soko la Utatu. Hata hivyo, Mkutano uliamua kuwa Mwongozo huo unahitaji maboresho zaidi na hivyo kukielekeza Kikosi Kazi cha Utatu kufanya marekebisho na kukamilisha uchambuzi ili kujiridhisha na ukomo wa thamani ya bidhaa unaopendekezwa.

***v) Kuendeleza Majadiliano ya Biashara kati ya Tanzania na Nchi nyingine***

121. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuendelea kutafuta fursa za biashara katika masoko ya nchi rafiki, Wizara ilishiriki katika Kongamano la Kibiashara kati ya Tanzania na Misri lililofanyika tarehe 10-14 Septemba, 2019 Jijini Dar es Salaam. Lengo la Kongamano hilo lilikuwa ni kutangaza fursa za Biashara kati ya Tanzania na Misri zitakazopelekea kukuza biashara na uwekezaji baina ya nchi hizo mbili na kuendeleza juhudi za kutafuta fursa za masoko kwa bidhaa za ndani zinazozalishwa nchini. Kupitia Kongamano hilo, nchi zote mbili ziliweza kujadili na kuweka mikakati ya kuendeleza fursa za biashara na uwekezaji katika sekta mbalimbali zikiwemo Ujenzi, Madawa, Umeme na Usafirishaji.

### *vi) Mikataba na Itifaki za Biashara*

122. ***Mheshimiwa Spika***; Wizara iliandaa na kuwasilisha Waraka wa kuomba ridhaa ya Serikali kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa *Marrakesh* ulionzisha Shirika la Biashara la Dunia ili kufanya Mkataba wa Uwezeshaji Biashara (Trade Facilitation Agreement) kuwa sehemu rasmi ya mikataba ya WTO. Waraka huo ulipata ridhaa ya Serikali na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 13 Novemba 2019. Tayari Hati ya Kuridhia (Instrument of Ratification) ya Mkataba huo imeshasainiwa na Mamlaka husika na kuwasilishwa Sekretarieti ya WTO kupitia Ubalozi wetu Geneva. Baada ya taratibu za uridhiwaji kukamilika, kinachofuata kwa sasa ni utekelezaji wa Mkataba huo wa Uwezeshaji Biashara.

123. ***Mheshimiwa Spika***; Vilevile, maandalizi muhimu ya awali ya utekelezaji wa Mkataba huo yalifanyika kupitia Kikao cha Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara tarehe 19-22 Novemba 2019, Dar es Salaam. Kupitia Kikao hicho, Kamati iliweza kuandaa rasimu ya taarifa mbambali (notifications) ambazo zinapaswa kuwasilishwa katika Sekretarieti ya WTO kulingana na matakwa ya Mkataba wa Uwezeshaji Biashara wa WTO. Taarifa zilizoandaliwa ni pamoja na Maeneo ya Kundi B

(Category B Measures) pamoja na muda wake wa utekelezaji; Maeneo ya Kundi C ambayo nchi itahitaji msaada wa kiufundi na kifedha katika utekelezaji, na Maeneo ya uwazi (transparency notification). Taarifa hizo ziliwasilishwa kwenye Kikao cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika tarehe 13 Februari 2020 jijini Dodoma. Hatua inayofuata kwa sasa, ni ukamilishaji wa taratibu za uwasilishaji wa taarifa hizo Sekretarieti ya WTO kwa ajili ya hatua zaidi.

### *vii) Mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara*

124. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea na marejeo ya Sera ya Taifa ya Biashara (2003) ambapo rasimu ya Sera, Mkakati wa Utekelezaji na Mkakati wa Mawasiliano pendekezwa vipo tayari. Wizara inaipitia rasimu hiyo ili kuhakikisha kuwa inakidhi na kuakisi mahitaji na hali halisi ya sasa ikiwa ni pamoja na kuendana na mabadiliko mbalimbali yanayoendelea kujitokeza katika ngazi ya kitaifa (national level), kikanda (regional) na kimataifa (multilateral) ili hatimaye ipate ridhaa ya Serikali. Katika ngazi ya kitaifa, msisitizo kwa sasa ni ujenzi wa uchumi wa viwanda na uhamasishaji biashara. Katika ngazi ya kikanda mabadiliko yaliyotokea ni pamoja na uimarishaji wa mtangamano wa kibiashara kupitia utekelezaji wa Itifaki mbalimbali kama vile Itifaki ya Jumuiya ya nchi za Kusini mwa

Afrika (SADC); Itifaki ya Umoja wa Forodha na Itifaki ya Soko la Pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sera hiyo itazingatia kupanuka kwa wigo wa biashara kikanda na katika bara la Afrika, kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Utatu litakalojumuisha kanda za EAC, SADC na COMESA na Eneo Huru la Biashara Afrika

### *viii) Utungaji wa Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Biashara (Trade Remedies Act, 2020)*

125. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea na taratibu za kutunga Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Kibiashara ya mwaka, 2020 (Trade Remedies Act, 2020) ambayo inalenga kulinda biashara na viwanda vya ndani. Ulinzi huo unalenga kuzuia uingizwaji wa bidhaa kwa wingi (import surge); bidhaa kuuzwa kwa bei ya chini ikilinganishwa na bei ya bidhaa kama hizo kwenye nchi zinakotoka (dumping); na bidhaa nyingine kupewa ruzuku (subsidies) na nchi zao au taasisi nyingine na hivyo kuathiri bidhaa ambazo zinazalishwa ndani ya nchi bila kupata ruzuku. Mapendekezo ya kutunga Sheria hiyo yameshawasilishwa Serikalini kwa ajili ya maamuzi.

### *ix) Nafasi ya Tanzania katika Biashara ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa*

**a) CHINA**

126. ***Mheshimiwa Spika;*** Mauzo ya bidhaa kwenye masoko ya upendeleo yalikuwa kama ifuatavyo: soko la China yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 144.28 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani milioni 233.60 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 61.9. Ongezeko hilo linatokana na uzalishaji na uuzaji kwa wingi mbegu za ufuta. Bidhaa zingine zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na tumbaku, pamba, *jute*, manila (coconut, abaca) na nguo na mavazi. Manunuzi ya Tanzania kutoka China yalikuwa Dola za Marekani milioni 1,762.78 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 1,987.60 mwaka 2019 sawa na asilimia 12.8. Ongezeko hilo limetokana na uagizaji kwa wingi bidhaa zenye thamani kubwa ambazo zinatumika katika uzalishaji na ujenzi wa miundombinu, bidhaa hizo ni matrekta, matairi ya magari, *gas oil* na vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa reli (tramway track construction material of iron and steel). Urari wa biashara unaonyesha nakisi ya Dola za Marekani 1,754.00 milioni. **(*Kiambatisho Na. 7)***

***b) INDIA***

127. ***Mheshimiwa Spika;*** Mauzo katika Soko la India yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 734.27 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani Milioni 867.70 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 18.2. Ongezeko hilo lilitokana na uuzaji kwa wingi bidhaa za maua, kahawa, alizeti, madini. Aidha, Manunuzi ya Tanzania kutoka India yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 1,218.07 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani Milioni 1,258.40 mwaka 2019 sawa na asilimia 3.3. Hali hiyo ilisababishwa na uagizaji kwa wingi bidhaa za madawa gesi na mafuta. Kutokana na hali hiyo urari wa biashara unaonyesha nakisi ya kiasi cha Dola za Marekani Milioni 90.70. **(*Kiambatisho Na. 7)***.

***c) JAPAN***

128. ***Mheshimiwa Spika;*** Mauzo katika soko la Japan yalipungua kutoka Dola za Marekani Milioni 66.72 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani Milioni 64.10 mwaka 2019 sawa na upungufu wa asilimia 3.9. Mwaka 2018, manunuzi ya bidhaa kutoka Japan yalikuwa na thamani ya Dola za Marekani Milioni 398.13 ikilinganiswa na Dola za Marekani Milioni 485.10 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 21.8. Ongezeko hilo linatokana na

uagizaji kwa wingi bidhaa zinazotumika kwenye uzalishaji viwandani kama vile mitambo na kemikali. Urari wa biashara umeonyesha nakisi ya Dola za Marekani Milioni 421. ***(Kiambatisho Na. 7)***

### d) *JUMUIYA YA UMOJA* WA ULAYA- EU

129. ***Mheshimiwa Spika;*** Bidhaa zilizonunuliwa na Tanzania kutoka Jumuiya ya Ulaya zilikuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 1,015.76 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 909.01 kwa mwaka 2019, ikiwa ni upungufu wa asilimia 10.5. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na; vifaa vya mitambo, vipuri vya magari, magari,nguo, vyombo vya majini (marine vessels), gesi na mafuta, vifaa vya madawa (medical apparatus), *paper board, fittings, gas tubes, mineral/chemical fertilizers, data processing machines*, vifaa vya mawasiliano na vifaa vya uchunguzi wa kimaabara. Pia, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Jumuiya ya Ulaya yalipungua kutoka Dola za Marekani Milioni 497.82 kwa mwaka 2018 hadi kufikia Dola za Marekani Milioni 399.30 mwaka 2019, ambayo ni sawa na upungufu wa asilimia 19.8. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni bidhaa za tumbaku, madini, kahawa, maharage ya soya, alizeti, pamba na maua. Kutokana na hali hiyo urari wa biashara umeonesha nakisi ya Dola za

Marekani Milioni 509.71 ikimaanisha thamani ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ni kubwa ikilinganishwa na thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko hilo. Hii inatokana na Tanzania kuuza zaidi malighafi katika soko la Jumuiya ya Ulaya wakati Tanzania inaagiza bidhaa za viwandani (finished products). Kutokana na hali hiyo urari wa biashara umeonyesha nakisi ya Dola za Marekani Milioni 509.71. Kupungua kwa biashara baina ya Tanzania na Jumuiya ya Ulaya kumechagiwa na kudorora kwa uchumi kwa baadhi ya nchi za Jumuiya ya Ulaya pamoja na kuimarika kwa uzalishaji wa viwanda vya ndani na kuimarisha bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi. ***(Kiambatisho Na. 8)***

***e) AGOA***

130. ***Mheshimiwa Spika;*** Mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Marekani kupitia Mpango wa AGOA kwa mwaka 2019 yaliongezeka na kufikia Dola za Marekani Milioni 21,116 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 42,432 kwa mwaka 2018 ***(Kiambatisho Na. 8)*** Mauzo hayo kwa kiasi kikubwa yalichangiwa na Sekta ya Nguo na Mavazi. Aidha, ili kuongeza mauzo zaidi katika soko hilo, Wizara imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Mauzo ya Tanzania katika soko la Marekani kupitia Mpango wa AGOA.

## f) JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)

131. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kutumia fursa za masoko ya kikanda, mauzo ya Tanzania katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2019 yalikuwa Dola za Marekani Milioni 674.40 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 447.50 mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 50.70. Ongezeko hilo limetokana na mauzo ya bidhaa za chai, mahindi, ngano, alizeti, mchele, bidhaa za karatasi, mabati, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), saruji na mafuta ya kupaka. Aidha, bidhaa za Tanzania zilizouzwa kwa wingi katika soko hilo ni pamoja na mbogamboga, chai, matunda, magunia, mifuko ya plastiki, wanyama hai, viazi, samaki, udongo asilia, kahawa, mahindi, mchele, unga wa nafaka, karanga, mawese, ufuta, pamba na makaa ya mawe. Mauzo hayo kwa kiasi kikubwa yanaenda katika nchi ya Kenya ikifuatiwa na Rwanda. Kwa upande mwingine, ununuzi wa Tanzania kutoka nchi za Jumuiya hiyo uliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 302.93 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 329.10 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 8.6. ***(Kiambatisho Na. 8)***

## g) *JUMUIYA YA MAENDEL*EO YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA *(SADC)*

132. ***Mheshimiwa Spika;*** Mauzo ya Tanzania kwenda katika soko la nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), mwaka 2019 yalikuwa Dola za Marekani Milioni 1,330.90 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 999.34 mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 33.20. Ongezeko hilo linatokana uuzaji kwa wingi bidhaa za madini, pamba, chai, kahawa, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), *petroleum coke*, saruji, sabuni na mafuta ya kupaka. Aidha, bidhaa hizo ziliuzwa katika nchi za Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Malawi. Ununuzi wa Tanzania kutoka katika soko hilo ulipungua kutoka Dola za Marekani milioni 604.32 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani Milioni 155.10 mwaka 2019 sawa na upungufu wa asilimia 74.3. Upungufu huo unatokana na kuimarika kwa uzalishaji viwandani hususan bidhaa zinzotumiwa kwa wingi nchini (consumable goods). ***(Kiambatisho Na. 8)***

### *4.2.4.* Sekta ya Masoko

***i) Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara Nchini***

133. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuhakikisha kwamba mazingira ya biashara nchini yanaendelea kuboreshwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta imeendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara Nchini (Blueprint for Regulatory Authority Reforms to Improve the Business Environment) ambao ulipata ridhaa ya Serikali na kuanza kutekelezwa rasmi Julai 2019. Aidha, *Blueprint* imeandaliwa Mpango Kazi (Blueprint Action Plan-BAP) ili kuongoza utekelezwaji wake na utungaji wa Sheria ya Uwezeshaji Biashara *(Business Facilitation Act)* uko hatua ya juu. Waraka wa Mapendekezo ya kutunga Sheria hiyo umekamilika kwa ajili ya maamuzi ya Serikali. Sheria hiyo itaweka misingi ya kusimamia maboresho kwenye Sekta ya Biashara na kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali zinazoathiri mazingira ya biashara.

134. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imeendelea na jitihada za kuhakikisha Leseni za Biashara Kundi A na B zinatolewa *kwa njia ya*

*mtandao kupitia Dirisha la Taifa la Biashara (National Business Po*rtal - NBP). Leseni za Biashara za Kundi "A" ambazo hutolewa na BRELA sasa zinatolewa kwa *n*jia ya mtandao kuanzia tarehe 1 Oktoba, 201*9*. Aidha, utoaji wa leseni za Biashara Kundi B ambazo ziko chini ya TAMISEMI zimeendelea kutolewa kwa njia ya mtandao kwa kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2019 katika Halmashauri y*a* Jiji la Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Hata hivyo, Halmashauri za Manispaa ya Bukoba, Chalinze, Mafinga na Karagwe zilifanyiwa mafunzo ya majaribio na taratibu za utekelezaji wake ziko mbioni. Majaribio ya Mfumo huo yamewezesha kubaini uwezo wa Halmashauri katika utoaji leseni kwa njia ya mtandao. Majaribio hayo yaliambatana na utoaji wa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa Maafisa Biashara 45, Maafisa TEHAMA 42 na Wafanyabiashara 250.

135. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha majaribio, jumla ya Leseni 12,621 zimetolewa zinazojumuisha Leseni za Kundi 'A' 4,332, na Leseni Kundi 'B' 1,957 katika Jiji la Mwanza na Leseni 6332 katika *Manispaa ya Ilala. Wizara i*mefanikisha kuunganishwa kwa Mfumo wa NBP na Mifumo ya GePG, Benki Kuu ya Tanzania na Mfumo wa Taarifa za Makusanyo ya Mapato wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Local Government Revenue Collection Information System -LGRCIS). Mafanikio hayo

yanatokana na jitihada za BRELA za kuboresha mazingira ya Biashara nchini ili kumwezesha mfanyabiashara kupata huduma popote alipo na kumpunguzia mteja gharama na muda unaohitajika kutumika.

136. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na BRELA imekamilisha Mfumo wa Utoaji wa Taarifa za Biashara za Kimataifa (Trade Information Portal). Mfumo huo unawezesha wafanyabiashara kupata taarifa muhimu za hatua za kupata leseni na vibali vinavyohitajika kutoka Taasisi mbalimbali kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi, kuingiza au kupitisha nchini mazao na bidhaa mbalimbali. Mfumo huo una taarifa zinazohusiana na taratibu za uuzaji wa mazao kama vile maua, Mwani, Parachichi, Maziwa na mazao yake, Asali, Nyama na mazao yake, Kahawa, Karafuu, Korosho, Chai na mengine. Kwa upande wa uingizaji bidhaa nchini, kuna taarifa zinazohusu bidhaa za Madawa, urembo, vyakula, vipodozi, vifaa tiba na magari. Aidha, katika kipindi cha mwezi Julai 2019 hadi Aprili 2020, jumla ya wadau 42,390 walitumia taarifa hizo, ambapo asilimia 85 ni Watanzania, ikilinganishwa na wadau 5,958 waliotumia taarifa hizo katika kipindi cha Julai 2018 hadi Juni, 2019.

137. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa

kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania imeanzisha Mfumo wa Kupata Huduma ya Usajili wa Majengo, Maeneo ya Uzalishaji, Uuzaji, Usambazaji wa Bidhaa za chakula, vipodozi na ukaguzi wa shehena zinazotoka nje ya nchi kwa njia ya mtandao, TBS *Online Applicaton System*-OAS. Mfumo huo, umewezesha wateja kuomba huduma za TBS popote alipo kwa njia ya mtandao, kupunguza gharama mbalimbali (usafiri, mawasiliano, utoaji wa vivuli kwa nyaraka), kuokoa muda ambao ungetumika kufuata huduma katika ofisi za Shirika na kuepusha mazingira ya rushwa kwa kutokuonana ana kwa ana na mtoa huduma. Vilevile, Shirika lina mfumo wa *Quality Management System* (QUALIMIS) ambao hutumika kumfikishia mteja taarifa za sampuli alizopeleka katika maabara kwa njia ya barua pepe.

138. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imeendelea kutoa huduma za usajili wa Makampuni; Majina ya Biashara; Alama za Biashara na Huduma; Kutoa Hataza; Kutoa Leseni za Viwanda na Leseni za Biashara ikiwa ni pamoja na huduma baada ya usajili (Post Registration Services) kwa kutumia Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS). Katika kipindi cha Julai 2019 hadi kufikia Machi 2020 BRELA imesajili Makampuni 7,549 ikilinganishwa na

6,918 Aprili, 2014; Majina ya Biashara 12,627 ikilinganishwa na 11,382 Aprili, 2019; Alama za Biashara na Huduma 1,970, Hataza 55 ikilinganishwa na 28 Aprili, 2019 na imetoa Leseni za Viwanda 200 ikilinganishwa na 166 Aprili, 2019 na Leseni za Biashara 9,927.

**ii) *Mwenendo wa Bei za Baadhi ya Mazao***

139. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kukusanya na kuchambua taarifa za mwenendo wa bei za mazao (mahindi, mchele, mtama, uwele, ulezi, maharage, ngano, viazi mviringo na pamba) pamoja na taarifa za bei za baadhi ya bidhaa za viwandani (saruji, nondo na bati) upande wa Tanzania Bara kupitia Mifumo ya FAMS na One2two. Taarifa hizo hukusanywa , huchambuliwa na kusambazwa kila siku ya Jumatatu, Jumatano na Ijumaa kwa wadau mbalimbali wakimemo Ofisi ya Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kilimo (Usalama wa Chakula), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Shirika la Chakula Duniani (WFP), Benki ya NMB, Taasisi za Utafiti na Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA).

140. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha mwezi Machi, 2020, wastani wa bei kwa gunia la kilo 100 nchini ni shilingi kwa 65,217 mahindi, shilingi 179,410 kwa maharagwe,

Shilingi 183,859 kwa mchele, shilingi 114,062 kwa mtama, Shilingi 121,117 kwa ngano, Shilingi 128,463 kwa ulezi, Shilingi 117,461 kwa uwele na Shilingi 71,000 kwa viazi mviringo***.(Kiambatisho Na.9(a),(c),(d))***

141. ***Mheshimiwa Spika;*** Wastani wa bei ya mazao hayo ya chakula umepanda ikilinganishwa na robo ya tatu ya mwaka 2018/2019 na robo ya tatu ya mwaka 2019/2020. Kwa mfano, bei ya gunia la kilo 100 la mahindi imepanda kwa asilimia 57; maharage yamepanda kwa asilimia 24; mchele umepanda kwa asilimia 14; wakati viazi mviringo na ulezi bei imeshuka kwa asilimia 4 na 6 mtawalia. Aidha, ongezeko la bei limetokana na kupungua kwa ugavi wa mazao hao katika soko***.(Kiambatisho Na.9(a),(c),(d))***

142. ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia tarehe 16 Februari, 2020 Kilo 348,909,841 za pamba zenye thamani ya Dola za Marekani 3.5 zimenunuliwa katika Mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Geita, Mwanza, Mara, Tabora, Singida, Kigoma, Kagera, Katavi, Dodoma, Manyara, Morogoro, Iringa, Pwani na Tanga Aidha, Kilo 348,501,838 inayojumuisha kilo 348,133,421 katika Kanda ya Magharibi zimesafirishwa na kilo 776,420 katika Kanda ya Mashariki. Aidha, hadi kufikia tarehe 3 Aprili, 2020 tani 58,547 za

kahawa zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 111.3 ziliuzwa. Kati ya hizo, tani 24,282 ziliuzwa kupitia minada ya ndani na tani 34,265 ziliuzwa moja kwa moja kwenye soko la nje.

143. ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia tarehe 4 Aprili, 2020 wastani wa bei ya jumla ya Sukari kwa wafanyabiashara ni kati ya Shilingi 2,400 na Shilingi 2,610 kwa kilo na bei za rejareja ni kati ya Shilingi 2,700 na Shilingi 2,900 kwa kilo na baadhi ya maeneo bei imefikia Shilingi 3,500. Aidha, bei ya juu katika baadhi ya maeneo imetokana na gharama za biashara kutoka sukari inakozalishwa au kusambazwa. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 5,588.28 za Sukari zilikuwepo ghalani, ambapo tani 3,437.05 zikiwa kwenye ghala ya wazalishaji Sukari nchini na tani 2,151.23 zilikuwepo katika ghala ya Wafanyabiashara. Aidha, katika kuhakikisha kwamba nchi inaendelea kujiitosheleza kwa Sukari, Serikali kupitia Bodi ya Sukari, ilitoa idhini kwa wazalishaji kuagiza tani 40,000 za sukari ya kuziba pengo la mahitaji kwa mwaka 2019/2020. Kiasi halisi kilichoagizwa ni tani 37,866 ambapo shehena ya kwanza ya tani 9,990 ilifika Bandari ya Dar es Salaam na kuanza taratibu za kiforodha kuitoa shehena hiyo tarehe 15 Aprili,2020 na shehena ya awamu ya pili ya tani 9,990 imewasili tarehe 27 na 28 Aprili 2020 tayari kwa kuingia sokoni.

### iii) *Kuhamasisha na Kuwezesha Wananchi Kutangaza Bidhaa na Huduma za Tanzania*

144. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara pamoja na Taasisi zake 15 zilishiriki katika Maonesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwl. J. Nyerere, kuanzia tarehe 28 Juni hadi tarehe 13 Julai, 2019. Sambamba na wazalishaji na wafanyabiashara kuonesha bidhaa na huduma mbalimbali wanazozalisha, Wizara iliratibu mikutano ya kibiashara kati ya wafanyabiashara/wazalishaji na wanunuzi na kutenga siku maalum ya kutangaza fursa za masoko na usindikaji kwa mazao ya kimkakati na huduma za biashara. Tukio la siku hiyo liliambatana na utoaji wa mada kutoka Taasisi mbalimbali, wazalishaji/wafanyabiashara pamoja na wananchi walioshiriki kwa kuchangia na kutoa maoni yao.

145. ***Mheshimiwa Spika***; Kupitia Maonesho hayo 43, wadau wa biashara pamoja na wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara waliunganishwa kupitia Mikutano ya Biashara (B2B) iliyofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 6 Julai, 2019 ikiwa ni mbinu ya kutafuta masoko. Katika mikutano hiyo, Wazalishaji walipata fursa ya kujitangaza na kuainisha bidhaa wanazozalisha ili kuzitambulisha kwa makampuni mbalimbali

ya ndani na nje yenye uhitaji wa bidhaa hizo. Wafanyabiashara wapatao 520 walishiriki na kusaini mikataba ya awali yenye thamani ya Shilingi 6,089,750,000.00 ikihusisha Sekta Ndogo za Mboga Mboga na Matunda pamoja na Shilingi 4,240,000,000.00 katika Sekta Ndogo ya Asali.

146. ***Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, Maonesho hayo yalitenga siku maalum kwa baadhi ya mazao kama korosho, viungo na mwani. Katika siku maalum ya viungo na mwani iliyofanyika tarehe 05 Julai, 2019 alipatikana mnunuzi wa Iliki kutoka Pakistani aliyehitaji tani 1,000. Aidha, Kampuni 437 zilipata oda ya kufanya biashara (Business deals) zenye thamani ya Shilingi Bilioni 7.93 pamoja na Mauzo ya papo kwa papo yenye thamani ya wastani wa Shilingi 209,450,000.

147. ***Mheshimiwa Spika;*** Maonesho ya Kilimo (Nanenane) ya mwaka 2019 yalifanyika Kitaifa katika viwanja vya Nyakabindi Wilayani Bariadi mkoani Simiyu kuanzia tarehe 31 Julai hadi tarehe 8 Agosti, 2019. Katika Maonesho hayo, jumla ya wajasiriamali 49 wanaojihusisha na uchakataji wa mazao ya kilimo na mifugo walishiriki kupitia banda la Wizara. Lengo likiwa ni kuwahamasisha wadau kurasimisha shughuli za kibiashara, kuwaunganisha na masoko, na pia kujifunza mbinu bora za uchakataji wa

mazao ya Kilimo kutoka kwa washiriki wengine. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini yake ilitoa huduma mbalimbali zikiwemo usajili wa majina ya biashara, usajili wa Makampuni na elimu kuhusu ujasiriamali. Aidha, Wizara kwa uratibu wa TanTrade iliendesha Kliniki ya Biashara ambapo ushauri kuhusu utatuzi wa changamoto za kibiashara, maelezo na ufafanuzi kuhusu Sheria, Kanuni na taratibu zinazosimamia kibiashara nchini yalitolewa pamoja na huduma mbalimbali za Kibiashara. Jumla ya wajasiriamali na wakulima wapatao 155 walipata mafunzo mbalimbali kupitia darasa hilo ambapo pia walipata taarifa za masoko.

148. ***Mheshimiwa Spika;*** Maonesho hayo pia yalitumika kuonesha na kutambulisha teknolojia na mashine mbalimbali ambazo zimebuniwa kulingana na mazingira halisi ya nchi yetu. Baadhi ya teknolojia hizo ni: Mashine ya kupura mpunga, alizeti na maharage; Mashine ya kuchakata Ngozi; Mashine ya kukausha mbogamboga na matunda; Mashine ya kukausha Korosho na Karanga; Trekta na Planta yake; Planta ya Pamba ya kukokotwa na wanyamakazi na Jiko la kutumia mwanga wa jua.

149. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia BRELA imekusanya taarifa za bidhaa mbalimbali kutoka Taasisi za Serikali zaidi ya ishirini (20) za kutoka Tanzania Bara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vilevile imeweza kukusanya taarifa kutoka taasisi tatu (3) zisizo za kiserikali zinazosimamia ufanyaji wa biashara nchini. Tayari taarifa za bidhaa zaidi ya 18 zinazosafirishwa nje ya nchi (Export) na zaidi ya bidhaa 8 zinazoingizwa nchini (Import) zimeshakusanywa na kuingizwa kwenye Mfumo. Bidhaa ambazo taarifa zake zimeshaingizwa kwenye mfumo ni Korosho, Kahawa, Chai, Nafaka, mikunde, Mbolea, Madawa, Vifaa tiba, Vipodozi, vyakula vilivyosindikwa, Mbao, Maziwa na bidhaa zake, Nyama na bidhaa zake, Asali na bidhaa zitokanazo na asali, Matunda na mboga za majani, Parachichi, Viungo, kakao, Maua, Karafuu na Mwani. Aidha, kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi, taarifa na taratibu za kupata leseni na vibali zilizowekwa katika mfumo ni; Madawa, Vipodozi, Vifaa tiba, Magari, Nafaka na jamii ya Mikunde, Mbao, Maziwa na bidhaa zake, Nyama na bidhaa zake pamoja na Mbolea.

***iv) Kuwaunganisha Wazalishaji, Wasindikaji na Wafanyabiashara na Masoko ya Ndani na Nje ya Nchi***;

150. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanya uchambuzi wa kampuni za ndani zinazofanya biashara ya uuzaji na uingizaji wa mazao na bidhaa zake kwa lengo la kuwaunganisha wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara. Jumla ya kampuni 19 zinajishughulisha na zao la mahindi, kampuni 9 kwa zao la vitunguu, Kampuni 23 kwa zao la Pamba, na wasindikaji wapatao 33 wametambuliwa kwa ajili ya kuwahamasisha kutumia rasilimali za ndani. Aidha, mwaka 2019 minada mitatu ya Kahawa imeanzishwa katika mikoa ya Kagera, Ruvuma na Songwe lengo likiwa ni kuwasogezea na kuwaunganisha na soko wazalishaji katika mikoa husika. Hadi kufikia tarehe 3 Aprili, 2020 tani 58,547 za Kahawa zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 111.3 ziliuzwa. Kati ya hizo, tani 24,282 ziliuzwa kupitia minada ya ndani na tani 34,265 ziliuzwa moja kwa moja kwenye soko la nje.

151. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Ubalozi wa Tanzania nchini China iliratibu ushiriki wa kampuni 10 za Kitanzania katika Maonesho ya Pili ya Kimataifa ya Bidhaa za Nje (China

International Importation Expo) yaliyofanyika jijini Shanghai kuanzia tarehe 5 hadi 10 Novemba 2019. Maonesho hayo yalivutia zaidi ya kampuni 3,000 kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni na kutoa fursa kwa kampuni za Kitanzania kubadilishana taarifa, uzoefu na mbinu za kibiashara. Aidha, jumla ya wageni 500,000 walitembelea maonesho hayo kwa lengo la kujionea bidhaa mbalimbali.

152. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika maonesho hayo, Tanzania kupitia Banda la Kitaifa ilionesha bidhaa za korosho, kahawa, viungo, karafuu, chai, vito vilivyotengenezwa kwa madini ya Tanzanite na bidhaa zilizotengenezwa kwa Ngozi kama vile pochi na mikanda. Jumla ya wageni 6,000 walitembelea Banda la Tanzania na jumla ya kampuni 120 zilionesha nia ya kununua bidhaa mbalimbali za Tanzania hususan bidhaa za kilimo hasa korosho, ufuta, wanga wa muhogo, karafuu, bidhaa za ngozi, bidhaa za mbao, bidhaa za madini ya *Tanzanite, sapphire, ruby, spinal, tsavorite, gold,* na *tourmarine.* Kati ya kampuni 120, kampuni 38 zilionesha nia ya kununua korosho ambazo zilielekezwa taratibu za kufanikisha azma hiyo.

153. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade iliwezesha Wajasiriamali 38 kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Nairobi yaliyofanyika tarehe 30 Septemba hadi 6

Oktoba, 2019 kwa ajili ya kukuza soko la Bidhaa na Huduma za Tanzania nchini Kenya ikiwa ni sehemu ya jitihada ya kutumia vyema fursa za soko katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vile vile, kampuni 7 kutoka Sekta ndogo za nguo, Sanaa za Mikono na ngozi ziliwezeshwa kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Eswatin yaliyofanyika tarehe 30 Agosti hadi 9 Septemba, 2019. Maonesho hayo yalitoa fursa ya kutangaza bidhaa za Tanzania katika soko la Ukanda wa Kusini wa Afrika.

### *v) Taarifa za Ununuzi katika Baadhi ya Mazao ya Biashara*

154. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa bei ya uuzaji na ununuzi wa mazao ya kahawa, tumbaku, pamba na korosho. Katika msimu wa mwaka 2019, ununuzi na uuzaji wa Kahawa ulifanyika katika minada mitatu katika mikoa ya Songwe, Ruvuma na Kilimanjaro. Kwa minada iliyofanyika katika Wilaya za Songwe, Mbinga na Moshi kati ya tarehe 9 Agosti, 2019 na tarehe 19 Desemba, 2019, Kilo 22,409,218 zenye thamani ya Dola za Marekani 48,851,583 kiliuzwa. Vile vile katika kipindi hicho mauzo ya nje yalikuwa Kilo 25,948,538 zenye thamani ya Dola za Marekani 40,851,931. Hivyo, jumla kuu ya

mauzo ya Kahawa katika kipindi hicho yalikuwa Kilo 48,357,756 yenye thamani ya Dola za Marekani 89,714,514.

155. ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia tarehe 31 Agosti, 2019 kiasi cha Tumbaku ya mkataba kilichonunuliwa ni Kilo 60,691,972.21 yenye thamani ya Dola za Marekani 92,927,331.79. Tumbaku iliyonunuliwa ni asilimia 105.9 ya matarajio ya uzalishaji ya kilo 57,305,127 yaliyobainishwa kwenye Mikataba ya Kilimo. Aidha, jumla ya Kilo 9,395,078.12 zilinunuliwa nje ya utaratibu wa mkataba ikiwa na thamani ya Dola za Marekani 7,232,521.78. Hivyo, hadi kufikia mwezi Desemba 2019, jumla ya Kilo 70,087,048.43 zenye thamani ya Dola za Marekani 100,159,853.51 zimeuzwa na wakulima.

156. ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia tarehe 22 Desemba, 2019 Kilo 348,331,518 za pamba zenye thamani ya Dola za Marekani 182,060,796.6 zilinunuliwa kutoka katika Mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Mwanza, Geita, Singida, Kagera, Kigoma, Dodoma, Katavi, Tabora na Mwanza. Kiasi hicho kimenunuliwa na kampuni 21 na Kilo 348,501,838 tu zilisafirishwa ambapo katika Kanda ya Magharibi kiasi kilichosafirishwa ni Kilo 348,030,378 na Kanda ya Mashariki ni Kilo 471,460.

157. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika msimu wa Korosho wa mwaka 2019/2020, kampuni 61 zilisajiliwa baada ya kutimiza vigezo vyote ikiwa ni pamoja na kuweka kinga ya zabuni (Security Bond) na kupatiwa leseni. Aidha, katika msimu huo minada ya Korosho ilianza rasmi tarehe 31 Oktoba, 2019 na kuisha 2 Februari, 2020 ambapo minada 72 imefanyika kupitia vyama Vikuu vya CORECU, TAMCU, MAMCU, TANECU, RUNALI, LINDI MWAMBAO pamoja na TACACU. Hadi kufikia tarehe 2 Februari, 2020, Tani 224.426.283 za Korosho ghafi zenye thamani ya Shilingi 575,416,173,694.90 ziliuzwa.

158. ***Mheshimiwa Spika;*** Kupitia Mradi wa ASDP II, Wizara inafanya maandalizi ya kufanya tafiti za mazao ya Kahawa, Korosho, Pamba, Chai, Mkonge, Tumbaku na Pareto. Lengo la tafiti hizo ni kubaini maeneo ya uzalishaji, kiwango cha uzalishaji, bei ya mkulima, mauzo ndani na nje ya nchi na changamoto za biashara na usindikaji wa mazao ya kilimo katika kuyaongeza thamani.

***Taarifa za Bei ya Vifaa vya Ujenzi***

159. ***Mheshimiwa Spika;*** Bei ya nondo mm 16 imeshuka kutoka wastani wa Shilingi 36,571 kipindi cha mwezi Machi, 2019 na kufikia wastani wa Shilingi 35,454 mwezi Machi,

2020 na bei ya juu kuwa Shilingi 42,500 mkoani wa Mtwara. Vilevile, nondo mm 12 imepanda kutoka wastani wa Shilingi 20,404 na kufikia wastani wa Shilingi 20,639, nondo mm10 zimeshuka na kufikia Shilingi 15,346 kutoka wastani wa bei ya Shilingi 15,364 na nondo mm 8 zimeshuka kutoka wastani wa Shilingi 12,143 na kufikia wastani wa Shilingi 12,089 kwa kipindi cha mwezi Machi, 2020.

160. ***Mheshimiwa Spika;*** Kufikia mwezi Machi 2020 wastani wa bei ya bati geji 32 imepanda na kufikia Shilingi 15,404 ikilinganishwa na wastani wa bei ya Shilingi 15,377 ya mwezi Machi, 2019, bati ya geji 30 imeshuka kutoka wastani wa Shilingi 18,705 na kufikia wastani wa Shilingi 18,473 na geji 28 imepanda kutoka wastani wa Shilingi 25,594 na kufikia wastani wa Shilingi 26,643 kwa bati. Aidha, Wastani wa bei ya rejareja ya saruji kwa mfuko wa kilo 50 imepanda na kufikia Shilingi 16,037 ikilinganishwa na wastani wa bei ya mwezi Machi, 2019 ya Shilingi 15,633. **(Kiambatisho Na. 9(b))**

161. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kipindi cha kuanzia Julai-Desemba 2019, wastani wa bei ya jumla ya Sukari kwa wafanyabiashara ni kati ya Shilingi 2,120 na Shilingi 2,583 kwa kilo na bei za rejareja ni kati ya Shilingi 2,400 na Shilingi 2,900 kwa kilo. Hata hivyo, bei ya sukari

ilipanda ghafla katika kipindi cha mwezi Aprili 2020 na kufikia wastani wa Shilingi 3,500 katika mikoa mingi nchini na baadhi ya maeneo kufikia kiwango cha Shilingi 4,000. Hali hiyo, imedhibitiwa kwa Serikali kuhakikisha kiasi cha sukari kilichoidhinisha tani 40,000 kuziba kiasi cha upungufu wa mahitaji ya sukari nchini (Gap sugar) kuanza kuingia nchini na kusambazwa kwa ajili kurekebisha mwenendo wa soko hususan katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha na kuathiri ufanisi wa usafirishaji wa bidhaa na uzalishaji wa sukari viwandani.

### vi) Kufanya Utafiti wa Masoko ya Nje ambapo Bidhaa za Tanzania zina Fursa

162. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade imeratibu tafiti za kutambua fursa za masoko ili kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania katika masoko ya nje. Kipaumbele ni katika masoko ya: China (Madini, Vito, Nyama, Tumbaku, Korosho na Muhogo); India (Mikunde, Korosho, Ngozi na Nafaka); Ulaya (Matunda, Mbogamboga, Asali, Kahawa na Korosho); na Nchi za EAC (nafaka, bidhaa za ujenzi, bidhaa za ngozi, bidhaa za viwandani na vyakula vya mifugo); Nchi za SADC (Madini, nafaka, bidhaa za viwandani, bidhaa za ujenzi). Aidha, mikutano na misafara ya kibiashara iliyoratibiwa ilizingatia na kutumia matokeo ya tafiti hizo na hivyo na

kufanikisha kutumia fursa hizo za biashara. Kwa mfano, ushiriki wa TanTrade katikamakongamano mawili ya kibiashara nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; na ujio wa misafara ya kibiashara kutoka Misri, Uganda, India, China pamoja na mikutano ya kisekta ilitumia taarifa za fursa hizo za biashara.

163. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade ilitoa taarifa za biashara kwa Kampuni 3,200 za uzalishaji bidhaa na huduma mbalimbali zinazozalishwa nchini kama sehemu ya mkakati wa kuimarisha uwezo wa upatikanaji wa taarifa za biashara kwa ajili ya kuwezesha kufanyika kwa maamuzi yenye tija ya kukidhi ushindani. Katika kipindi hicho, TanTrade ilipokea na kusambaza majibu ya maulizo 205 kuhusu upatikanaji wa masoko, bidhaa na mazao mbalimbali kama vile nafaka, mbogamboga, mazao jamii ya kunde, muhogo, mashudu, viungo, asali, soya, pamba, mbegu za chia, ufuta, alizeti, soyambuzi, samaki, mbao, na vifaa vya ujenzi, katika soko la Kenya, Uganda, India, China, Rwanda, Congo, Morocco, Jumuiya ya Nchi za Falme za Kiarabu (UAE) na Jumuiya ya Ulaya (EU). Aidha, jumla ya wafanyabiashara 284 waliunganishwa na wanunuzi wa bidhaa za kilimo, uvuvi, misitu na mifugo katika masoko hayo.

### *vii) Uendelezaji wa Masoko ya Kimkakati na Biashara Mipakani*

164. ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na masoko ya kimkakati kwa ajili ya kukuza biashara na mauzo nje ya nchi kwa maendeleo ya wananchi wake na Taifa kwa ujumla. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imekuwa ikichukua hatua za kuanzisha, kuboresha na kuendeleza masoko ya kimkakati ya mipakani kutokana na umuhimu wa eneo husika ili kurasimisha ufanyaji biashara. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) inaratibu Mradi wa Ujenzi na Uboreshaji wa Masoko ya Mipakani ya Rusumo (Tanzania/Rwanda) na Tarakea (Tanzania/ Kenya) kuhakikisha wananchi waishio mipakani wananufaika ipasavyo. Jitihada hizo zimekwenda sambamba na mpango wa Wizara wa ujenzi wa masoko ya Kimkakati katika mipaka ya Tunduma (Tanzania/Zambia), Mutukula (Tanzania/Uganda) na Holili (Tanzania/Kenya) kwa kushirikiana na TMEA. Ujenzi wa masoko hayo pamoja na uwepo wa Vituo vya OSBP utasaidia kurahisisha ufanyaji biashara mipakani, kuimarisha usalama wa biashara mipakani na hivyo kuiwezesha Serikali kurasimisha biashara kwa urahisi na kupata

taarifa na takwimu muhimu na za uhakika katika biashara za mipakani.

165. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zinazosimamia ufanyaji biashara mipakani imeendelea kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za biashara mipakani na kuhakikisha Taasisi za Umma zinawezesha biashara badala ya kukwamisha biashara kati ya nchi na nchi. Timu ya Wizara ikiongozwa na Naibu Waziri Mhe. Injinia Stella Manyanya (Mb) ilifanya ziara ya kutathmini hali ya biashara katika mipaka ya Namanga tarehe 15 Novemba 2019 na ziara katika mkoa wa Mara kuanzia Desemba 2 hadi 5, 2019 katika mpaka wa Sirari, mpaka wa Kilongwe na eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa soko la mpakani la Lemagwe wilayani Tarime. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha Wafanyabiashara wa mipakani kutoa taarifa juu ya vikwazo, changamoto au kero za kibiashara hasa zile zisizokuwa za kikodi.

166. ***Mheshimiwa Spika;*** Vituo vya Pamoja Mipakani (OSBP) vimeongeza ufanisi wa ufanyaji biashara kwa kuwezesha watu, magari na bidhaa mipakani kukaguliwa kwa urahisi na kwa haraka zaidi hivyo kupunguza muda unaotumiwa na kuwaondolea wafanyabiashara gharama za ziada watumiazo mipakani wakisubiri kupatiwa huduma. Katika kujenga

uendelevu wa huduma bora, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka zinazosimamia taasisi za Umma zinazoshughulika na biashara mipakani imeanzisha mfumo wa mawasiliano kwa njia ya mtandao (*WhatsApp Group*) unaojumuisha Viongozi na watendaji wote mipakani kwa ajili ya kubadilishana taarifa kwa urahisi na haraka lengo likiwa ni kutolea ufumbuzi changamoto zinazojitokeza katika mipaka husika. Aidha, mfumo huo pia unatumiwa na wadau katika sekta ya biashara kutoa taarifa ya vikwazo, changamoto na kero za kibiashara hasa zile zisizokuwa za kikodi (NTBs).

***viii) Kutangaza Bidhaa na Huduma Zinazozalishwa Nchini na Kuwaunganisha Wazalishaji Watanzania katika Masoko Nje na kuongeza ushiriki wa Tanzania katika biashara ya nje***

167. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade imeratibu na kusimamia zoezi la kuwaunganisha wanunuzi wa bidhaa na wazalishaji kwa kufanikisha yafuatayo: - Mkataba kati ya Nchi ya Zimbabwe na Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) kununua tani 83,000 za mahindi; Mkataba kati ya Kampuni ya *Rafael Group* ya Mbeya na Kampuni ya *Dar Lion* ya Ufaransa kuuza tani 360 za mchele; Mkataba kati ya *Bakhresa Food Products* na Umoja wa Wafanyabiashara wa Matunda

Buguruni wa kununua ukwaju tani 30 wenye thamani ya Shilingi milioni 18; Mkataba kati ya Kampuni ya *Eleven Agri* na *World Farmers Tanzania Ltd,* kununua unga wa Ubuyu tani 50; Mkataba kati ya Kampuni ya *Bakhresa Food Products* na Asasi ya *Sustainable Agriculture Tanzania Ltd,* kununua unga wa ubuyu tani 20, machungwa tani 5 na nazi tani 5; na Kiwanda cha ALAF kilipata oda ya kuuza tani 1,200 za chuma nchini Rwanda.

168. ***Mheshimiwa Spika;*** Makubaliano kwa Kampuni 3 kufanya biashara ya mbogamboga na matunda zenye thamani ya jumla Shilingi 8,376,235,793.36 kwa mwaka yalifanyika. Kampuni husika ni *TanzaNice* ambayo ilipata oda ya kuuza tani 700 za parachichi zenye thamani ya Euro 3,250,000 kwenye nchi za Ufaransa, Ujerumani, Uingereza na Uholanzi; *Frank Horticultural & Timber Company Ltd* ilipata oda ya kuuza parachichi, maharage machanga (green beans), njegere changa (snow peas) na njegere mbichi (Garden peas) zenye thamani ya Dola za Marekani 1,980,000 kwenda Denmark, Dubai, Kuwait na Ubelgiji; na Kampuni ya *Hortanzia* ilipata oda ya kuuza kitunguu jani (chives) yenye thamani ya Euro 2,000 kwenda Ujerumani. Aidha, TanTrade kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) kusimamia mauzo ya tani 215,484.90 za korosho kwa njia ya minada kwa msimu wa

Mwaka 2019/2020; Kuunganisha wadau wa muhogo na kampuni yenye uwezo wa kununua wastani wa tani 100 za muhogo mbichi kwa wiki kutoka kwa wakulima wadogo; na kushiriki katika mnada wa mauzo ya miti katika mashamba ya miti ya Serikali yaliyopo Mtibwa katika Mkoa wa Morogoro, na Longuza, Muheza katika Mkoa wa Tanga ambapo mauzo ya jumla ya Shilingi Bilioni 4.77 yalifanyika.

169. ***Mheshimiwa Spika***, Baada ya mikutano ya B2B iliyofanyika katika maonesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara kampuni kadhaa zilifanikiwa kuendelea kufanya biashara. Kampuni hizo ni pamoja na *Dow elef Agri* yenye bidhaa za Pilipili zenye thamani ya Shilingi Milioni 400, *Dar Carton* yenye bidhaa ya Mihogo zenye thamani ya Shilingi Milioni 90, *Follow Honey* yenye bidhaa ya Nta yenye thamani ya Shilingi Milioni 900 na Shilingi Milioni 390 za bidhaa ya asali. Kampuni hizo zina fursa ya kuuza kwa miezi 10 toka kumalizika kwa Maonesho ya 43 ya DITF.

170. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade ilifanikiwa kushiriki maonesho ya nje na kutangaza bidhaa za Tanzania nchini China na Ujerumani. Katika Maonesho ya China yaliyofanyika Beijing, TanTrade ilifanikiwa kupata Kampuni ya *Jingsu Overseas Group Company Limited* ambayo inajihusisha na uuzaji

wa nyama ili kuitembelea Tanzania na kuwakutanisha na wauzaji wakuu wa nyama. Aidha, kikao cha maandalizi ya kutambua mahitaji ya mnunuzi kwa ajili ya kukidhi fursa ya soko hilo kilifanyika na wauzaji kubainishwa. Katika maonesho ya Ujerumani ya Fruit *Logistica,* TanTrade iliambatana na msafara wa kampuni 18 na katika ushiriki kampuni 20 za Ujerumani zilionesha uhitaji wa bidhaa za matunda, hivyo kuunganishwa na kampuni za kitanzania. Aidha, kulipatikana kampuni 20 nyingine za teknolojia ambazo zilitoka mataifa mbalimbali ya Ulaya na Amerika ambapo kampuni hizo ziliingia makubaliano ya kibiashara na kampuni tano (5) za Kitanzania.

### *ix) Uimarishaji Ushindani katika Soko na Biashara ya Ndani*

171. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Mwaka 2019, limetoa leseni za ubora 358 ikilinganishwa na leseni 259 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 38.2. Ongezeko hilo limetokana na mafunzo yaliyotolewa kwa wazalishaji mbalimbali kuhusu umuhimu wa kuzingatia ubora wa bidhaa. Aidha, mafunzo 108 ya udhibiti ubora yalitolewa kwa washiriki 7,464 ikilinganishwa na mafunzo 59 yaliyotolewa kwa washiriki 4,208 mwaka 2018.

172. ***Mheshimiwa Spika;*** Vilevile Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imeendelea kutoa huduma za kuhakiki usahihi wa vipimo na mifumo ya upimaji katika Sekta ya Biashara, Afya, Usalama na Mazingira kwa lengo la kumlinda mlaji. Katika kipindi cha mwaka 2019, Wakala imekagua vipimo 841,518 ikilinganishwa na vipimo 732,912 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 14.8. Hii imetokana na kuongezeka kwa vitendea kazi vikiwemo magari na vifaa vya kisasa vya kupima dira za maji na mizani ya kuhakiki usahihi wa vipimo vya madini. Vilevile, Wakala imetoa leseni za ufundi na uundaji wa vipimo kwa wadau 300 mwaka 2019 ikilinganishwa na wadau 200 mwaka 2018.

173. ***Mheshimiwa Spika;*** Vilevile, Mwaka 2019, Wakala imeongeza uwezo wa kuhakiki magari yanayobeba mafuta kutoka wastani wa magari nane na kufikia magari 70 kwa siku. Hii imetokana na kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Uhakiki wa Magari kilichopo Misugusugu-Kibaha. Aidha, Wakala umeongeza Kituo cha Tarakea mkoani Kilimanjaro kwa lengo la kuboresha udhibiti wa bidhaa zinazofungashwa mipakani na hivyo kuwa na jumla ya vituo nane.

174. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika

kuhakikisha udhibiti wa bidhaa bandia nchini, Mwaka 2019 Serikali kupitia Tume ya Ushindani ilikagua makasha 3,260 ya kusafirishia mizigo ambapo makasha 114 yalibainika kuwa na bidhaa bandia. Bidhaa bandia zilizokamatwa zilikuwa na alama zilizogushiwa pamoja na kukosa alama za utambulisho wa bidhaa, anuani ya mzalishaji na nchi ya uasili ilipotengenezwa. Aidha, Tume ilifanya kaguzi 32 za kushtukiza katika ghala na maduka mbalimbali kwa lengo la kubaini bidhaa bandia.Tume ilifanikiwa kukamata bidhaa bandia ikiwa ni pamoja na vifaa vya ujenzi (pisi 12,571); mafuta na vipodozi (pisi 850); vifaa vya ofisi (pisi 6,652); vipuri na vilainishi (dazeni 129); nguo na viatu (jozi 6,906) pamoja na vifaa vya elektroniki (pisi 3,750) na kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria.

### *x) Uendelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala*

175. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuhamasisha na kusimamia matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwenye mazao ya kilimo. Hadi sasa, jumla ya mazao 10 yameingizwa katika Mfumo huo ambayo ni Mbaazi, Dengu, Soya, Mpunga, Ufuta, Kakao, Kahawa, Alizeti, Korosho, na Mahindi. Katika msimu wa 2019, jumla ya Tani 5,926.726 za ufuta zimeuzwa kupitia Mfumo wa

Stakabadhi za Ghala, Mbaazi Tani 775.543, Dengu Tani 80.804, Soya Tani 2,892.004, Kahawa Tani 1,406.205 na Kakao Tani 6,603.240. Aidha, hadi kufikia Desemba 22, 2019 jumla ya Tani 187,273. 252 za kahawa zimeuzwa kupitia minada 43 na ghala 21 zimesajiliwa na kupewa leseni ya kushiriki katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa zao la korosho katika msimu wa mwaka 2019.

176. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika msimu wa Mwaka 2019/2020, jumla ya leseni 55 zilitolewa kwa waendeshaji wa ghala katika mazao mbalimbali nchini. Kati ya hiyo, sekta ndogo ya Zao la Korosho leseni 34; Zao la Kahawa leseni tano; Zao la Ufuta leseni sita; Zao la Kakao leseni mbili; Zao la Soya leseni nne; Zao la Mbaazi leseni mbili ; Zao la Dengu leseni moja; Zao la Mpunga leseni moja. Pia, Bodi imepewa mamlaka ya kutoa leseni kwa Mameneja Dhamana pamoja na Wakaguzi wa Ghala. Hivyo, kwa mwaka 2019/2020, Bodi imetoa jumla ya leseni tatu kwa Meneja Dhamana katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

177. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa miongozo minne mipya ifuatayo:

Mwongozo Namba 10 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika zao la Soya Toleo Namba 1; Mwongozo Namba 11 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala zao la Dengu Toleo Namba 1; Mwongozo Namba 15 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala zao la Mbaazi Toleo Namba 1; na Mwongozo Namba 16 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala zao la Pamba Toleo Namba 1. Aidha, miongozo miwili ilifanyiwa marejeo kabla ya kuendelea kutumika katika mazao husika ambayo ni: Mwongozo Namba 1 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala Sekta Ndogo ya Korosho Toleo Namba 10; na Mwongozo Namba 9 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala Sekta Ndogo ya Ufuta Toleo Namba 4. Kuandaliwa kwa miongozo hiyo kutasaidia kikamilifu utekelezaji wa Mfumo huo katika mazao hayo mapya yaliyoingizwa.

178. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) kwa kushirikiana na Mfuko wa Kuimarisha Sekta ya Fedha (FSDT), Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX),Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), taasisi za fedha za CRDB na NMB, Shirika la Bima la Taifa (NIC) na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) ziliunda Jukwaa Jumuishi kwa lengo la kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu mifumo rasmi ya kifedha kwa mkulima na biashara za kijasiriamali vijijini. Lengo ni kuhakikisha kwamba wakulima wanapata

huduma za kifedha ili kuwawezesha kuendeleza shughuli zao. Uhamasishaji huo ulifanyika katika Mkoa wa Kagera Wilaya za Karagwe, Bukoba (M), Bukoba (V), Misenyi, Kyerwa, Muleba, Ngara na Biharamulo kwa kuhamasisha na kutoa elimu katika AMCOS na wakulima waliopo katika Wilaya hizo. Zoezi hilo liliambatana na ufunguzi wa akaunti ambapo zaidi ya wakulima 3,200 walipata elimu ya huduma za kifedha na baadhi yao kuweza kufungua akaunti na kuunganishwa na huduma nyingine za kifedha kupitia simu kama vile *Simu Account* na *NMB mobile.*

179. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Bodi ilihamasisha na kutoa mafunzo ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Mkoa wa Manyara Wilaya ya Babati na Mkoa wa Dodoma Wilaya ya Kondoa. Vilevile, Elimu ilitolewa kwa viongozi wa Serikali Mkoa wa Dodoma, wakulima 60 katika Wilaya ya Babati na wakulima 70 katika Wilaya ya Kondoa. Aidha, Elimu ya Mfumo ilitolewa kwa wakulima wa mpunga wa Pawaga Iringa chini ya Kampuni ya *Tuungane Company Limited* wanaoendesha ghala la IGODI KAVU ambapo jumla ya wakulima 34 walipata mafunzo ya kina ya namna ya kuendesha Mfumo.

180. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa ilikamilisha ujenzi wa ghala na kuweza kulitumia katika Mfumo wa Stakabadhi kuhifadhi zao la korosho. Aidha, ghala la kuhifadhi mazao lililojengwa kupitia Mradi wa MIVARF Wilayani Kondoa, limeweza kutumika kwa mara ya kwanza katika msimu wa 2019/2020 katika Mfumo kwa kufanya biashara.

### *xi) Udhibiti wa Ubora na Viwango vya Bidhaa zinazozalishwa Nchini*

181. ***Mheshimiwa Spika***; Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara kupitia TBS imekamilisha viwango muhimu 228 ambavyo ni sawa na asilimia 50.7 ya lengo la kutayarisha viwango 450 kwa mwaka. Viwango hivyo ni katika kilimo, chakula, uhandisi na viwango vya vifungashio mbalimbali. Kati ya viwango 228 vilivyokamilika, viwango 31 ni katika nyanja za uhandisi mitambo *(mechanical),* 16 katika nyanja ya kemikali *(chemical),* 19 katika nyanja ya uhandisi umeme (*electro technical)*, 27 katika nyanja za nguo na ngozi *(textile and leather),* viwango 17 katika nyanja ya mazingira *(environmental),* 17 katika nyanja ya madini (Mining and minerals) na 101 katika sekta ya kilimo na chakula *(food and agricultur*e). Pia, Shirika liliendelea kusimamia viwango vya

kitaifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora *(Certification Schemes).*

182. ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya leseni 366 za nembo ya ubora ya TBS zilitolewa ambayo ni sawa na asilimia 101.7 ya lengo la kutoa leseni 360 kwa mwaka 2019/2020. Miongoni mwa leseni hizo, leseni 126 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha kashata, mafuta ya kula, pombe, unga wa ngano, unga wa muhogo na lishe, maji ya kunywa, tindikali ya betri, kachumbari, mvinyo, pombe isiyotokana na nafaka, siagi ya karanga, pilipili, kripsi za maembe na kripsi za ndizi. Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali (SMEs) na wadau mbalimbali katika dhana nzima za kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

### *xii) Udhibiti wa Ubora na Viwango vya Bidhaa Zinazozalishwa Nje ya Nchi*

183. ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara kupitia TBS imetoa jumla ya vyeti vya ubora (*Certificate of Conformity - CoCs*) 25,821 kwa shehena za bidhaa zitokazo nje ya nchi; hii ni sawa na asilimia 68.0 ya matarajio ya kutoa jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa 38,000 kwa mwaka mzima. Aidha, jumla ya vyeti vya ukaguzi wa

magari 28,820 vilitolewa sawa na asilimia 70.3 ya malengo ya kufikisha jumla ya vyeti 41,000. Jumla ya sampuli 20,854 zilipimwa katika maabara mbalimbali za Shirika kwa lengo la kuhakiki ubora wake, hii ni sawa na asilimia 90.7 ya lengo la kupima sampuli 23,000 kwa mwaka. Jumla ya mitambo 7,157 ilifanyiwa Ugezi, hii ni sawa na asilimia 95.4 ya lengo la kufanyia ugezi mitambo 7,500 kwa mwaka.

184. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia WMA imeendelea kufanya kazi ya udhibiti wa bidhaa zilizofungashwa mipakani. Wizara imeongeza kituo cha Tarakea Mkoani Kilimanjaro hivyo kufanya Wizara kuwa na jumla ya vituo nane vya ukaguzi ambavyo ni Sirari (Mara), Mutukula(Kagera), Namanga (Arusha), Holili (Kilimanjaro), Tunduma (Songwe), Tarakea (Kilimanjaro), Horohoro (Tanga) na Kasumuru (Mbeya). Vilevile, Wizara iliendelea na usimamizi wa mafuta yanayoingia nchini jamii ya *petrol* na mafuta ya kula (edible oil) ambapo kwa sasa Wizara inahudumia bandari za Mtwara, Tanga na Dar es Salaam.

185. ***Mheshimiwa Spika****;* Wizara kupitia TBS, imeendelea kutoa mafunzo kwa Wajasiriamali (SMEs) na wadau mbalimbali katika dhana nzima za kuzingatia mifumo bora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora. Kwa kipindi

cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya mafunzo na semina 87 zilitolewa; idadi hii ni sawa na asilimia 96.7 ya lengo la kutoa mafunzo na semina 90 kwa mwaka. Mafunzo na semina hizo zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo pamoja na wadau mbalimbali wapatao 6,328 katika mikoa ya, Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, na Pwani, Ruvuma, Tanga.

186. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imekagua na kuhakiki idadi ya vipimo 626,552 ikiwa ni sawa na asilimia 91 ya lengo la kukagua vipimo 686,765 vilivyokadiriwa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi mwezi Februali, 2020. Aidha, WMA imeendelea kutoa elimu kwa wakulima wa zao la korosho katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma. Pia, Wakala imeendesha zoezi la ukaguzi (wa kawaida na wa kushitukiza) wa mizani itumikayo kupimia zao la korosho. Katika kaguzi hizo jumla ya mizani 1,924 ilikaguliwa ambapo kati ya mizani hiyo, mizani 326 ilikutwa na makosa na kuamriwa kurekebishwa kabla ya kuendelea kutumika tena. Aidha, Wakala imeendelea kukagua bidhaa zilizofungashwa ili kuhakiki usahihi wa kiasi kilichotamkwa. Baadhi ya bidhaa zilizokaguliwani ni vyakula (unga, Mchele, mafuta ya kula, Maji, maziwa na vinywaji), vilainishi, saruji, rangi, mitumba,

mabati na nondo. Hivyo, kufanya malengo kufikiwa kwa zaidi ya asilimia 90.

187. ***Mheshimiwa Spika;*** Jumla ya taarifa/maandiko 44 yalitolewa kwenye magazeti mbalimbali katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februali, 2020. Pia, Vipindi Saba (7) vya Redio, vipindi tisa (9) vya TV, na mikutano mitatu (3) (press conference) ilifanyika. Aidha, Wakala imeshiriki katika maonesho ya Sabasaba, Nanenane na maonesho ya Viwanda. Pia, Wakala ilitoa elimu kwa wakulima wa korosho sambamba na zoezi la ukaguzi lililofanyika wakati wa msimu wa ununuzi wa korosho katika Mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Pwani na Lindi ambapo Elimu ilitolewa kwa Wakulima ma vyama vya Msingi (AMCOS) 725. Elimu ilihusu Matumizi sahihi ya Vipimo ili waweze kutambua mizani sahihi na iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo. Pia Wakulima walipatiwa namba ya bure ya WMA ambayo ni 0800110097 ili waweze kutoa taarifa kwa Wakala wa Vipimo Makao Makuu pale wanapokutana na changamoto au wanapobaini matumizi yasiyo sahihi ya Mizani katika vyama vya Msingi. Ukaguzi uliofanyika ni Ukaguzi wa Mizani ya Korosho.

### *xiii) Udhibiti wa Ushindani Usio Haki katika Soko*

188. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeendelea kufanyia kazi jumla ya mashauri tisa (9). Mashauri hayo yanahusu makubaliano yanayofifisha ushindani (5), miunganiko ya kampuni yaliyofanyika bila kuiarifu Tume (2), makubaliano ya siri (1) na matumizi mabaya ya nguvu (1). Katika mashauri yanahusu makubaliano yanayofifisha ushindani (Anti-Competitive Agreements) kutoka katika sekta ndogo ya Tumbaku, Tume imeendelea kufanya majadiliano na mmoja wa watuhumiwa aliyeomba kumalizika kwa shauri lake kwa njia ya suluhu(settlement proceeding). Aidha, Tume inaendelea kufanya uchambuzi wa utetezi wa kimaandishi wa watuhumiwa katika mashauri yaliyobaki. Katika mashauri yanayohusu matumizi mabaya ya nguvu za soko (Abuse of Dominance) kutoka katika Sekta Ndogo za Kufukiza na Sekta ya Saruji, Tume imeandaa rasimu ya maamuzi ya awali (provisional findings) kwa shauri kutoka Sekta Ndogo ya Kufukiza. Tume inaendelea kufanya uchunguzi kwa shauri kutoka Sekta Ndogo ya Saruji.

189. ***Mheshimiwa Spika;*** Tume inaendelea kufanya uchunguzi dhidi ya shauri linalohusu makubaliano ya siri (cartel) kutoka katika Sekta Ndogo ya Chuma. Aidha, katika

mashauri yanayohusu muungano wa kampuni bila kuiarifu Tume (Un-notified Merger) kutoka katika Sekta Ndogo ya Nishati Mbadala na Sekta ya Usafirishaji, Tume ilitoa hati ya shauri (statement of case) pamoja na maamuzi ya awali (provisional finding) kwa shauri kutoka Sekta Ndogo ya Nishati Mbadala. Aidha, katika shauri kutoka katika Sekta ya Usafirishaji, mtuhumiwa ameahidi kutekeleza maamuzi ya makubaliano (settlement agreement).

190. ***Mheshimiwa Spika;*** Pia, Tume imefanya kaguzi katika Bandari ya Dar es Salaam na ICDs ambapo jumla ya makasha elfu moja mia nne thelathini na moja (1,431) yalikaguliwa. Kati ya hayo, makasha arobaini na nane (48) yalikamatwa kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 (kama ilivyorekebishwa). Bidhaa zilizokamatwa katika kaguzi hizo ni pamoja na vifaa vya umeme kama (fridge, fridge guard na viyoyozi), vifaa vya ujenzi, miswaki yenye nembo ya Goldegate, vipuri vya magari na pikipiki, vikombe, viatu (vya wanaume na wanawake), vitenge, box tupu zenye nembo ya Vim na Harpic.

191. ***Mheshimiwa Spika;*** Tume imefanya kaguzi za kustukiza (***raids***) mara kumi na tisa (19) katika Mkoa wa Dar Es Salaam kwenye bidhaa za wino wa kudurufu karatasi (*toner)* zenye alama ya HP na CANON, nguo na viatu

vyenye alama ya HUGO, BOSS na NGK, dawa za nywele zenye nembo ya SUPER BLACK, bidhaa za tochi zanye alama ya TOURCH, nyembe zenye alama ya RUNGU MAX na SUPER MAX pamoja na fulana (T-shirts) zenye alama ya AFRICAN BOY. Kupitia kaguzi hizo za kushtukiza, bidhaa bandia zenye thamani ya Shilingi 1,031,163,532 zilikamatwa kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 kama ilivyorekebishwa.

### *xiv) Kukamilisha Sera ya Ubora*

192. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea na maandalizi ya Kutunga Sera ya Taifa ya Ubora ambayo itasaidia wazalishaji wakubwa kwa wadogo kuweza kukidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa na hatimaye kufikia masoko ya nje ya nchi. Rasimu ya Sera pamoja na Mkakati wake wa utekelezaji umekamilika. Hatua inayofuata ni kupata maoni ya wadau mbalimbali kuhusiana na Rasimu hizo zilizokwishaandaliwa ili hatimaye Serikali ifanye maamuzi ya mwisho.

### *xv) Mikataba/Itifaki na Marekebisho ya Sheria za Taasisi*

193. ***Mheshimiwa Spika,*** Itifaki ya Marrakesh iliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 16 uliofanyika Jijini Dodoma kuanzia tarehe 3 hadi

13 Septemba 2019. Itifaki ya Marrakesh inalenga kuwezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona, wenye uoni hafifu, ulemavu unaofanya mtu kushindwa kusoma wa mwaka 2013 (The Marrakesh Treaty to Facilitate Access to Published Works for Persons who are Blind, Visually Impaired or Otherwise Print Disabled 2013) ili kuwawezesha wanufaika wa mkataba huo kuweza kupata wasaa wa machapisho na vifaa vya kuwawezesha kupata elimu kwa njia rahisi. Wizara kwa kushirikiana na COSOTA na COSOZA iliandaa Mpango kazi wa utekelezaji na azimio la kuridhia Itifaki ya Marrakesh na kuwasilisha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli alitia saini azimio la Itifaki hiyo mnamo Januari, 2020 na Hati hiyo kuwasilishwa WIPO mwezi Machi, 2020. Hatua za utekelezaji wa mkataba wa Itifaki hiyo unatarajia kuanza kwa kufuata mpango kazi ulioandaliwa.

***xvi) Athari za Mlipuko wa Virusi vya Corona katika Sekta ya Biashara***

194. ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa kuzingatia kuwa Sekta ya Biashara ni mtambuka, mlipuko wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19) umesababisha sekta mbalimbali za uchumi kuathirika na kiasi

kikubwa kuathiri sekta hii. Kutokana na mlipuko ugonjwa huo, Mamlaka za nchi zimelazimika kuchukuwa hatua mbalimbali kwa ajili ya kujikinga na kupambana na janga hili. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kusitishwa kwa usafiri wa anga kuingia katika nchi mbalimbali na hatua zingine ambazo kwa kwa kiasi kikubwa zimeathiri shughuli za kibiashara. Kimsingi Sekta zote za kiuchumi zimeathirika na miongoni mwao ni Sekta ya Viwanda na Biashara. Fursa za masoko zinatokana na Tanzania kuwa mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Tanzania pia inategemea Jumuiya ya Ulaya (EU) kama soko la mazao na bidhaa za mazao, Asia kupitia (Quota Free Duty Free - QFDF) China, India na Japan na katika soko la AGOA bidhaa inaouza huko kwa wingi almasi, dhahabu, chai, kahawa, maua na viungo (spices).

195. **Mheshimiwa Spika;** Baadhi ya mazao ya kimkakati ikiwemo pamba, korosho na kokoa bei zake zimeshuka. Katika kipindi cha mwezi Februari na Machi 2020, bei ya pamba duniani imeshuka kwa kiasi cha asilimia 12; bei ya kakao imeshuka kwa asilimia 22; na kahawa imeshuka kwa asilimia 5 (Arabika) na asilimia 3.5 (Robusta). Kushuka kwa ununuzi wa kahawa kumesababishwa kwa kiasi kikubwa na

kufungwa kwa maduka nchini China, Ulaya na Marekani kutokana na zuio la kutotoka nje. Mfano, Kampuni ya *Starbucks* imefunga maduka 2,150 kati ya 4,300 nchini China. Aidha, mauzo (volumes) ya mazao na bidhaa za kilimo yameshuka. Kiwango cha ununuzi wa kakao kilishuka kutoka tani 116,440 mwezi Februari 2020 hadi kufikia tani 38,354 mwezi Machi 2020 ikiwa ni sawa na asilimia 67.1.

196. **Mheshimiwa Spika;** Wazalishaji wa mazao Mbogamboga, Matunda, Maua na Viungo (horticulture) wamekuwa kwa miaka mingi wakitegemea soko la nje hasa Ulaya, Marekani na Asia. Kutokana na mlipuko wa ugojwa huo na kufungwa kwa mipaka, kumeathiri biashara hiyo ambayo mazao yake yanaharibika kwa wepesi. Sekta hiyo imeathirika kama ifuatavyo: Mauzo ya mazao ya mbogamboga na matunda nchini umeshuka kwa asilimia hamsini (50). Hali hiyo imesababishwa na kushuka kwa mahitaji ya bidhaa hizo hususan katika soko la nje, na kupungua kwa safari za ndege. Mfano, Shirika la KLM limepunguza safari zake kutoka safari 7 kwa wiki hadi 3. Hata hivyo, uhitaji wa mazao hayo katika masoko ya ndani ni mdogo na kukosa masoko mbadala ya kupeleka bidhaa zao zaidi ya kuendelea kuzihifadhi kwa muda mfupi na baadaye kuziteketeza kabisa

### *4.2.5. Maendeleo ya Rasilimali Watu na Utoaji Huduma*

197. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara ilipokea IKAMA ya watumishi kwa mwaka 2019/2020 kutoka Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora ambayo inatoa mwongozo wa kuajiri baada ya kibali cha kuajiri kutolewa. Aidha, Wizara imepokea muundo mpya ambao utasaidia katika kujaza nafasi za uteuzi zilizoko wazi.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuwajengea uwezo watumishi wake, Wizara imepeleka watumishi saba katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Kati ya hao, mtumishi mmoja anashiriki Shahada ya Uzamivu (Phd), watumishi watano wanashiriki mafunzo ya Shahada ya Uzamili (Masters Degree), na mmoja anashiriki mafunzo ya Diploma ya Utunzaji Kumbukumbu. Aidha, watumishi 17 wameweza kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi katika kozi mbalimbali zilizochangia katika kujenga uwezo na kuongeza ufanisi katika maeneo yao ya kazi.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mwaka 2019/2020, Wizara imewapeleka watumishi wawili katika mafunzo ya muda mfupi ya

ujasiriamali ambao wamestaafu katika Utumishi wa Umma, ikiwa ni kuwaandaa na maisha baada ya kustaafu. Aidha, watumishi hao tayari wamekwisha andaliwa nyaraka zao muhimu na kuwasilishwa katika mamlaka husika kwa ajili ya uandaaji wa mafao yao kwa wakati.

200. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Wizara imefanikiwa kufanya kikao kimoja cha Kamati Maalum ya Maadili ya Wizara kikilenga kupanga mikakati ya kudumisha uadilifu kwa watumishi wa Wizara. Pia kupitia vikao vya idara vinavyofanyika kila mwezi, elimu imetolewa kwa watumishi athari za vitendo visivyo na uadilifu kazini vikiwemo vya rushwa lakini pia kusisitiza uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya kiutumishi wakati wa kutoa huduma.

201. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe bora na posho ya usafiri kila mwezi kwa watumishi saba (7) wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ambao wamejiweka wazi kwa mujibu wa Mwongozo wa Serikali. Wizara pia iliweza kushiriki katika semina zilizofanyika kuanzia tarehe 27 Novemba 2019 na kufikia kilele siku ya maadhimisho ya siku ya kimataifa ya UKIMWI tarehe 1 Desemba, 2019 iliyofanyika jijini Mwanza.

202. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuendelea na jitihada za kupambana na kujikinga maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza (MSY) kazini. Wizara imeweza kufanya kikao kimoja cha Kamati Maalum ya Masuala ya UKIMWI na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza (MSY) kilichofanyika tarehe 21 Januari, 2020. Aidha, Wizara inatoa vifaa tiba na vifaa kinga kwa watumishi wake bure pamoja na elimu kwa watumishi kujikinga yanaendelea kutolewa.

### *4.2.6. Ukaguzi wa Ndani*

203. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na Sheria, miongozo na kanuni zilizowekwa. Katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo kwa matumizi sahihi ya rasilimali za serikali, Wizara imefanya ukaguzi wa fedha, rasilimali watu na ununuzi na kuhakikisha kwamba sheria, kanuni na taratibu zinafuatwa na hatimaye Wizara imepata hati safi ya Ukaguzi. Aidha, Kamati ya ukaguzi ya Wizara ilifanya vikao vinne ili kupitia taarifa za hesabu pamoja na ukaguzi na kutoa ushauri unaostahili kwa Afisa Masuuli.

### *4.2.7. Ununuzi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha*

204. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara kupitia Kitengo cha Ununuzi kiliweza kutekeleza yafuatayo:- Kusimamia shughuli za ununuzi wa bidhaa na huduma kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya mwaka 2011 na kanuni zake GN Na, 446 ya mwaka 2013, kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016 pamoja na miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Udhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA); Kuandaa Mpango wa Ununuzi kwa mwaka fedha 2019/2020; Kuwezesha Watumishi watatu (3) kupata mafunzo ya mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki *Tanzania Electronic Procurement system*(TANePS); Kuratibu vikao vitatu (3) vya Bodi ya Zabuni ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020; Kuandaa taarifa za ununuzi za kila mwezi, robo pamoja na taarifa ya mwaka na kuziwasilishwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA); na Kufanya uhakiki mali za Wizara na kuhuisha taarifa za Daftari la Mali la Wizara kwa mujibu wa muongozo wa mali za Serikali wa mwaka 2019 pamoja na Sheria ya Fedha Na. 6 ya mwaka 2001 na Kanuni zake, GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

### *4.2.8. Mawasiliano Serikalini*

205. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka wa fedha 2019/2020 kitengo kimeendelea kutoa elimu na kuhabarisha Umma kupitia vyombo vya Habari ikiwemo Radio, Televisheni, Magazeti, Majarida, Mitandao ya Kijamii na kupitia maonesho ya Biashara yanayofanyika nchini. Aidha, Kitengo kimekamilisha Makala (Documentary) inayohusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano katika sekta ya Viwanda na Biashara ambayo inarushwa kupitia Televisheni mbalimbali za hapa nchini.

### *4.2.9. Huduma za Sheria*

206. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya Marekebisho ya Sheria tatu. Sheria hizo ni:- Sheria ya Viwango Sura 130 ili kuhamishia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) majukumu ya chakula na vipodozi kutoka iliyokuwa TFDA (TMDA ya sasa) ikiwa ni utekelezaji wa Andiko la BLUEPRINT; Sheria ya Makampuni Sura 212 ili BRELA ibaki na majukumu ya makampuni yanayohusika na biashara tu kama ilivyo dhamana ya Wizara; na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura, 218 kwa kuiwezesha COSOTA kufifilisha makosa mbalimbali, kuboresha

adhabu chini ya sheria hiyo kuendana na muda wa sasa na kuitambua *re-sale right.*

207. ***Mheshimiwa Spika;*** Pia, Wizara imefanya upekuzi na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali Alama mbalimbali za Viwango chini ya Sheria ya Viwango, Sura 130 ili kumlinda mlaji na mtumiaji wa bidhaa na huduma mbalimbali Tanzania.

### *4.2.10. TEHAMA na Takwimu*

208. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ilitekeleza yafuatayo:- Kusimamia na kuratibu matumizi bora, salama na sahihi ya miundombinu na Rasilimali za TEHAMA; na Kuimarisha ulinzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa kufanya tathmini ya ulinzi wa mifumo ya TEHAMA. Tathmini hiyo ilifanywa na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) mwezi Oktoba, 2019 na kubaini kuwa mifumo ya TEHAMA wizarani ina ulinzi na usalama wa kutosha na kuipa wizara alama ya utoshelevu ambao ni zaidi ya asilimia 40.

## 5. MWELEKEO NA VIPAUMBELE VYA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA

### 5.1. *Mwelekeo wa Sekta ya Viwanda na Biashara*

209. ***Mheshimiwa Spika;*** Mtazamo na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kuhusu maendeleo ya viwanda na biashara nchini, unalenga kujenga uchumi wa viwanda utakaowawezesha Watanzania kufikia na kunufaika na uchumi wa kati ifikapo 2025. Hatua hiyo itawezesha Watanzania kutumia fursa za kiuchumi na kijamii katika mifumo iliyoboreshwa na inayozingatia haki na utawala bora. Ni dhamira ya nchi yetu kumfanya kila Mtanzania kuwa na maisha bora na kunufaika na rasilimali na fursa zilizopo na zinazojitokeza. Hivyo, ni jukumu letu sote kuwaandaa na kuwawezesha Watanzania kuchangamkia fursa zilizopo ipasavyo.

#### i) *Kuimarisha Taasisi za Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia na Uwekezaji*

210. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuendeleza uchumi wa viwanda, Serikali inaimarisha taasisi zake ili ziweze kukidhi na kuhimili mahitaji ya maendeleo na ujenzi wa viwanda nchini. Wizara inajizatiti kuimarisha

Taasisi za Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia yaani TIRDO, TEMDO na CAMARTEC, kwa kupitia upya na kwa kina majukumu na miundo ya kisheria ya taasisi hizo. Lengo ni kuzifanyia maboresho mahsusi na itakapoonekana inafaa, zitafanyiwa maamuzi ya kimuundo ikiwemo kuziunganisha ili ziweze kuwa na tija na ufanisi katika kuleta mwendelezo wa mafanikio ya taasisi hizo na pia kuongeza nguvu katika kuendeleza viwanda nchini.

211. ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali itajielekeza katika kuimarisha taasisi za uwekezaji nchini hususan EPZA na NDC ili ziwe mihimili na nguzo za uwekezaji katika viwanda ambavyo ni muhimu katika kujenga uchumi wa Taifa lakini wakati mwingine sekta binafsi haiko tayari kuwekeza. Msukumo ukiwa ni kujenga viwanda mama, viwanda vya kimkakati na viwanda ambavyo kutokana na unyeti wake haviwezi kuachiwa sekta binafsi.

***ii) Kuimarisha SIDO***

212. ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa kutambua umuhimu na mchango wa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo katika uchumi na hususan ujenzi wa viwanda, Serikali itachukua hatua za makusudi kuimarisha ujasiriamali nchini. Kipaumbele kitakuwa katika kuimarisha

taasisi ya SIDO kwa kupitia upya muundo wake na kuijengea uwezo ili iweze kubeba ipasavyo dhamana ya uendelezaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo inayowabeba Watanzania walio wengi.

### *iii) Utoaji Huduma kwa Kulenga Wateja*

213. ***Mheshimiwa Spika;*** Utoaji huduma bora kwa wananchi kwa kiwango kinachoridhisha ni lengo kuu la mabadiliko ya kiutendaji ambayo Serikali ya Awamu ya Tano inayapa kipaumbele. Hivyo, mwelekeo wetu ni kuhakikisha kuwa taasisi za kisekta tukianzia na TBS na BRELA zinajielekeza katika kutoa huduma kwa kiwango kinachokidhi matarajio ya wananchi. Wizara yangu na taasisi zake zitaongeza ubunifu katika utendaji kazi kwa tija na kutoa huduma kwa weledi ili kuchochea ufanisi katika Sekta ya Viwanda na Biashara na hatimaye kuongeza Pato la Taifa.

### *xvii) Kuimarisha Huduma ya Usajili Biashara kwa Njia ya Mtandao*

214. ***Mheshimiwa Spika;*** Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inatoa huduma za usajili wa Makampuni, Majina ya Biashara, Hataza na Alama za Biashara kwa kutumia Mfumo wa *Online Registration System* (ORS) na utoaji wa Leseni za Biashara kupitia

Mfumo wa *National Business Portal* (NBP). Utekelezaji wa mifumo hiyo katika kutoa huduma umesaidia kuongeza tija na ufanisi wa utendaji kazi wa Taasisi na Jumuiya ya Wafanyabiashara ambapo cheti cha usajili kilichokuwa kikipatikana katika kipindi cha siku saba sasa kinapatikana ndani ya siku moja kwa mteja aliyekamilisha taratibu zote kama inavyotakiwa. Aidha, mifumo hiyo imewezesha wafanyabiashara na wawekezaji kupata huduma za usajili wa kampuni, majina ya biashara na leseni za biashara wakiwa mahali popote ndani na nje ya nchi. Pia, mifumo hiyo imesaidia kupunguza urasimu na vitendo vya rushwa kwa baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu.

215. ***Mheshimiwa Spika;*** Kutokana na mifumo hiyo, wasimamizi wa mifumo (System Administrators) wanafuatilia hatua kwa hatua maombi (Application) ya wateja na kutambua kila mtumishi na muda uliotumika kushughulikia suala husika. Aidha, mifumo inaweza kutoa taarifa za jumla ya maombi yaliyofanyiwa kazi na Afisa husika kwa kipindi husika. Hatua hiyo imeongeza umakini na uwajibikaji kwa watumishi na hivyo kuongeza ufanisi katika utoaji huduma kwa wateja. Aidha, mifumo imewezesha taarifa za wateja kupatikana kirahisi tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo kulikuwa na malalamiko mengi

kutoka kwa wafanyabiashara ya kupotea kwa baadhi ya taarifa katika mafaili ya usajili wa makampuni.

216. ***Mheshimiwa Spika;*** Wakala pia kupitia mifumo hiyo imefanikiwa kupunguza gharama za uendeshaji ambazo ilikua ikizipata kabla ya kuanza kutumia mifumo. Baadhi ya gharama zilizopunguzwa ni pamoja na matumizi ya karatasi za kuchapisha vyeti vya usajili na leseni za biashara ambapo kwa sasa mfanyabiashara anachapisha cheti cha usajili na leseni za biashara akiwa ofisini kwake.

### *xviii) Kuimarisha Huduma za Wasanii Nchini*

217. ***Mheshimiwa Spika;*** Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) imeendelea kutekeleza majukumu yake ambayo ni pamoja na kubainisha, kutetea na kulinda maslahi ya watunzi wa kazi mbalimbali za sanaa. Hadi kufikia Machi, 2020 COSOTA imekusanya Shilingi 257,987,500 ambapo Shilingi 152,557,500 ni fedha zinazotokana na makusanyo ya mirabaha kutoka kwenye biashara za vileo, hoteli, klabu, casino na kumbi za shughuli; Shilingi 17,010,000 ni makusanyo kwenye kazi za maandishi; usajili wa kazi za Sanaa Shilingi 33,420,000; na Vyombo vya utangazaji (TV na radio) Shilingi 55,000,000.

Aidha, COSOTA imeendelea kufanya ukaguzi wa watumiaji haramu wa kazi za Hakimiliki kwenye mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mwanza, Kilimanjaro, Manyara, Dodoma, Arusha, Pwani na Dar es Salaam. Aidha, COSOTA imeingia Mkataba wa Makubaliano (MOU) na WIPO kwa ajili ya kutatua migogoro ya kisanaa (Alternative Dispute Resolutions (ADR) activities).

218. ***Mheshimiwa Spika;*** utakumbuka Bunge lako tukufu lilifanya Marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na 7/1999 yaliyopitishwa na Bunge mwezi Juni, 2019 kupitia Misc. Written Laws Act No. 3 of 2019 (Gazeti la Serikali Na 27 la tarehe 30 Juni, 2019). Kifungu cha 16 cha Sheria hiyo kimerekebisha Sheria kwa kuongeza Kifungu 42A kinachohusu *Compounding of Offences*. Kupitia kifungu hicho, COSOTA imepewa mamlaka ya kutoza faini za papo kwa papo katika makosa ya ukiukwaji wa Hakimiliki mara baada ya mtuhumiwa kukiri kosa lake bila ulazima wa kwenda Mahakamani. Aidha, marekebisho hayo yameleta pia kifungu cha *resale right* kwa ajili ya kufuatilia na kusimamia faida ya wabunifu kila kazi zao zinapouzwa kwa zaidi ya mara moja kutoka mtumiaji mmoja kwenda mtumiaji mwingine. Hatua hiyo ni ya msingi sana kwa COSOTA na Sekta Ndogo ya Sanaa na Ubunifu.

### *xix) Kuimarisha Sekta Binafsi na Wajasiriamali*

219. ***Mheshimiwa Spika;*** Mtazamo wa sera za Taifa zinatambua nafasi ya sekta binafsi kama injini ya maendeleo ya kiuchumi. Kujenga sekta binafsi hasa wajasiriamali wadogo kwa kuwawekea mazingira wezeshi na rafiki kupitia upatikanaji wa mitaji, teknolojia rahisi na rafiki, masoko ya uhakika na huduma muhimu zinazolenga kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji ni suala lisilohitaji mjadala. Hivyo, katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara, mtazamo wa kisera utalenga kukuza na kutengeneza uwekezaji kuanzia ngazi ya ujasiriamali mdogo hadi kuwa matajiri wazalendo wa baadaye. Aidha, sera na mikakati itazingatia mahitaji ya uwekaji mazingira wezeshi, yanayotabirika na yanayojenga kuaminika kwa mwekezaji na hivyo kumfanya mwekezaji aamini na kuamua kuwekeza mtaji wake nchini.

### *xx) Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini*

220. ***Mheshimiwa Spika;*** Ujenzi wa mazingira bora na endelevu ya biashara ni kichocheo kikubwa na muhimu katika kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Hivyo, Serikali kupitia Wizara yangu imejizatiti kwa

kuhakikisha kuwa inaendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini. Maboresho hayo yatavutia wawekezaji wa ndani na nje katika viwanda na biashara na hivyo kuwezesha kutumia fursa mbalimbali za ndani na nje ya nchi kadri zinavyojitokeza. Misingi ya maboresho ya mazingira ya kibiashara yanategemewa kuwekewa nguvu ya kisheria na utaratibu wenye ushirikishaji mpana zaidi wa wadau. Aidha, katika kuhakikisha uendelevu na uhakika wa kuvutia wawekezaji na upatikanaji wa soko kwa bidhaa zetu nje ya nchi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kutumia Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi kutangaza bidhaa zetu ikiwa ni pamoja na kuzishirikisha katika maonesho ya Kimataifa ambayo nchi inashiriki.

### *xxi) Kulinda Soko na Biashara ya Ndani*

221. ***Mheshimiwa Spika;*** Uchumi himilivu, unaotabirika na shindani unatokana na jitihada za makusudi za kuujenga, kuuendeleza na kuulinda. Kujilinda isitafsiriwe kuwa ndiyo kujitenga kiuchumi na nchi nyingine na wala siyo dhambi, kwani hata nchi zilizoendelea kiuchumi duniani mbinu mbalimbali zinaendelea kutumika kwa njia tofauti. Hivyo, sera, sheria na mikakati ya kisekta itaendelea kuhakikisha kuwa

kunakuwepo ushindani wa haki ili kulinda viwanda na biashara nchini. Aidha, tutaendelea kulinda haki za msingi za walaji kwa kuweka utaratibu wa kisheria utakaotaka wawekezaji, wenye viwanda na wafanyabiashara katika mazao, bidhaa na huduma kutotumia nguvu ya soko isivyotakiwa na kusababisha kuwakandamiza wanyonge walio wengi.

### *xxii) Kuhamasisha Uuzaji wa Bidhaa na Mazao Yanayozalishwa Nchini*

222. ***Mheshimiwa Spika;*** Ni dhahiri kuwa nchi yetu inazalisha mazao na bidhaa nyingi ambazo zinapaswa kupewa kipaumbele katika kuzilinda na kuzitangaza ipasavyo. Kupitia maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya Bidhaa za Viwanda vya Ndani yanayofanyika mwezi Desemba kila mwaka katika Viwanja vya Sabasaba, nimejiridhisha kuwa bidhaa hizo zina ubora wa hali ya juu. Ni wakati muafaka sasa kupitia Bunge lako tukufu kuangalia namna ya kipekee kama nchi kushiriki kujitangaza na kuhamasisha matumizi ya bidhaa zetu za ndani kupitia kampeni ya NUNUA BIDHAA ZA TANZANIA JENGA TANZANIA - NUBITAJETA. Moja ya njia ya kuzitangaza bidhaa zetu ni kuhamasisha jitihada za *branding* na *Made in Tanzania* kwa Watanzania waliopo ndani na nje ya nchi. Jitihada hizo zinaweza kuanzishwa hapa

Bungeni kwa kutenga siku maalum ya kuvaa vazi la kitaifa lililobuniwa na wabunifu wetu wa ndani. Vilevile, ofisi za Serikali zinaweza kuangalia namna ya kujiwekea utaratibu kama huo wa kuvaa vazi hilo angalau kwa siku moja katika wiki. Hatua mahsusi kama hizo zitachochea uzalendo na kuhamasisha jamii zinazotuzunguka kupenda, kuthamini na hatimaye kutumia bidhaa za ndani kwa wingi zaidi na kwa uendelevu.

### *xxiii)Kuhuisha Kada ya Waambata wa Biashara*

223. ***Mheshimiwa Spika;*** Ili kuongeza nguvu za utafutaji na utumiaji wa fursa za masoko ya nje, Wizara inafanya uchambuzi wa kina kuhusu nafasi ya Waambata wa Kibiashara na mchango wa kada hiyo katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Lengo ni kutathmini tija itakayokuwepo katika kuhuisha na kurejesha Waambata wa Biashara (Trade Attachee) katika ofisi za Balozi zetu zilizo nje ya nchi. Sambamba na hilo, Wizara itatathmini nafasi ya Mawakala/ madalali ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa Kitanzania nje ya nchi wanaotumiwa na Jumuiya ya Wafanyabiashara katika kufanikisha upatikanaji na uuzaji wa bidhaa ndani na nje ya nchi.Lengo ni kuweka mfumo wa kufanya tathmini na utafiti wa mahitaji ya soko la bidhaa zinazozalishwa nchini kwa

kutumia Waambata hao. Tathmini na tafiti hizo zitatoa picha ya mahitaji ya soko la nje na kuwezesha wazalishaji wa bidhaa za ndani kuzalisha kwa kuzingatia mahitaji ya soko la nje.

***xxiv) Kuimarisha Mfumo wa Utendaji na Usimamiaji Kazi za Kisekta katika Ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa Nchini***

224. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuzingatia umuhimu wa utendaji kazi wenye tija katika ngazi za Makatibu Tawala Mkoa (RAS) na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), Kada za Maafisa Biashara zitapewa msukumo wa kipekee ili kuhakikisha inahuishwa na kufanya kazi zake kitaalam. Aidha, Wizara imeanza mazungumzo na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuandaa Mkataba wa Makubaliano (Memorandum of Undestanding) wa kuweka mifumo na mazingira bora ya kufanya kazi pamoja na kwa kushirikiana. (Kubadilika kimawazo (change of mindset) ni moja ya tiba muhimu katika kuleta mabadiliko yenye matokeo na yenye tija na endelevu katika uchumi wetu).

**xxv) Upatikanaji wa Teknolojia Rahisi na Nafuu kwa Wajasiriamali**

225. ***Mweshimiwa Spika;*** Wizara pia

itaweka mkazo na umuhimu katika upatikanaji wa teknolojia za kuongeza tija katika uzalishaji kwa kuimarisha taasisi za teknolojia zilizo chini ya Wizara. Jitihada hizo zitakwenda sambamba kwa Wizara kujikita zaidi katika ujenzi wa maeneo yenye miundombinu ya uzalishaji (Industrial shades) inayosimamiwa na SIDO. Hiyo itawawezesha wajasiriamali kupata mahali muafaka pa kufanyia kazi za uzalishaji na kuweza kuhudumiwa kirahisi na taasisi mbalimbali zikiwemo za udhibiti wa ubora wa bidhaa, taasisi za fedha na mafunzo. Aidha, juhudi za kuimarisha jasiriamali nchini zitaenda sambamba na kuimarisha SIDO ili imudu kutoa huduma bora na zenye kuleta tija katika uzalishaji wa bidhaa, huduma na ufanyaji biashara.

**xxvi) Uendelezaji wa Ujuzi na Nguvukazi Nchini**

226. ***Mheshimiwa Spika;*** Suala la kuwa na Rasilimali watu ya kutosha yenye sifa, uwezo na inayotumika vizuri ni muhimu katika kujenga uchumi endelevu wa viwanda. Wizara imejipanga kuendeleza kimkakati rasilimali watu iliyonayo kwa kuwa na mpango mpana wa kuwaendeleza na kuwajengea uwezo watumishi wa wizara ili kuongeza ujuzi na weledi katika kutekeleza majukumu yao. Hii itawezesha kuboresha huduma zitolewazo na kukidhi

matarajio ya wadau na umma wa ujumla. Pia tutajielekeza zaidi katika maeneo ya kuboresha huduma (service delivery) kwa njia mbalimbali, kuimarisha usimamizi na uratibu wa shughuli za kisekta (Regulatory role) na kuishirikisha sekta binafsi na wadau wengine kuchangia kikamilifu katika kukuza uchumi. Ili kuwa na rasilimali watu wenye afya, Wizara itahakikisha kuwa watumishi wanapata elimu ya afya na huduma za kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza. Jitihada pia zitafanywa za kushawishi taasisi za elimu kuandaa mitaala inayozingatia mahitaji ya soko ili kukidhi mfungamanisho wa kitaaluma unaohitajika katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

**xxvii) Ujenzi wa Miundombinu ya Msingi na Wezeshi kwa Ajili ya Uwekezaji wa Viwanda**

227. ***Mheshimiwa Spika;*** Kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya msingi na wezeshi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na ufanyaji biashara ni suala la msingi. Uendelezaji wa miundombinu hiyo kwa kushirikiana na sekta binafsi utapewa msukumo zaidi ili kuleta tija na mvuto kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Jitihada za kushirikisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kumiliki, kuendeleza na kusimamia maeneo maalum ya uwekezaji nazo

zitapewa kipaumbele kabla ya kukimbilia kutafuta wawekezaji wa nje. Wizara pia itashirikiana na Balozi za Tanzania pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge na Uwekezaji kuja na mkakati wa kuvutia wawekezji kutumia sehemu ambazo zimefidiwa chini ya EPZA. Mradi wa ujenzi wa Kongano la Viwanda Kizota (Kizota Industrial Cluster) kwa Mkoa wa Dodoma ambao umezindua miradi ya ujenzi wa miundombinu hiyo katika mikoa yote nchini ni moja ya jitihada zinazolenga kuendelezwa katika maeneo mengine ya mikoa nchini. Maeneo hayo yatakuwa *Center of Excellency* ambazo pamoja na mambo mengine itafungamanisha miradi mikubwa na ya kimkakati katika mnyororo wa thamani.

228. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kujengea uwezo na kuendeleza uwekezaji wa wajasiriamali wadogo na wa kati nchini, mwelekeo wa Wizara ni kuhakikisha kuwa ujenzi wa *Industrial Shades* unafanywa katika mikoa yote nchini na msukumo ukiwa katika kukamilisha miradi iliyoanza na ikifuatiwa na maeneo mengine ya pembezoni mwa nchi hususan Kyela, Nyasa, Kigoma, Karagwe ikiwa ni msukumo wa kufungamanisha maboresho ya vituo vya biashara za mipakani na viwanda katika maeneo hayo.

### ***xxviii) Kuthamini Bidhaa na Huduma zinazozalishwa Nchini Tanzania***

229. ***Mheshimiwa Spika;*** Kuthamini rasilimali na bidhaa za ndani ni ukombozi muhimu wa kiuchumi kwa Taifa lolote kwani nchi huwa soko la kwanza kabla ya kutafuta soko jingine. Suala la msingi ni wananchi kujenga imani na kupata thamani na ubora wanaouhitaji katika bidhaa na huduma za ndani ya nchi. Mifano hai ni nchi za Japan na China ambazo wananchi wake wamejijengea utamaduni wa kuthamini bidhaa zinazozalishwa katika uchumi wao. Kwa kutambua msingi huo, Wizara itaendelea kuhamasisha uimarishaji wa ubora na matumizi ya bidhaa za ndani, nguvukazi na malighafi za ndani ili kuleta ufungamanisho wa sekta katika kujenga uchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TanTrade inaendelea kuhamasisha wananchi kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani kupitia kauli mbiu ya Nunua Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania (Buy Tanzania, Build Tanzania). Mbinu hii ni muhimu sana katika kipindi hiki cha ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kuimarisha viwanda vya ndani kwa kutegemea soko la uhakika la ndani ya nchi. Hii itajumuisha kusimamia matumizi ya bidhaa, mazao na nguvukazi ya ndani katika miradi na

shughuli kubwa za nchi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya *Local Content*.

### 5.2. *Vipaumbele kwa Bajeti ya Mwaka 2020/2021*

230. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2020/2021, Wizara ina vipaumbele vifuatavyo:

(a) Kuendeleza na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kimkakati na vya kielelezo;
(b) Kufufua Viwanda Vilivyobinafsishwa, upanuzi na ukarabati wa viwanda vilivyopo na kuchochea/kuhamasisha uwekezaji/uanzishwaji wa viwanda vipya;
(c) Kuendeleza miundombinu ya msingi na saidizi ya maeneo ya uwekezaji na huduma ya viwanda kwa wawekezaji na wajasiriamali;
(d) Uendelezaji na uwekezaji katika maeneo maalum ya uwekezaji na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje;
(e) Uendelezaji wa taasisi za utafiti na maendeleo ya teknolojia ya viwanda na kuvutia na kuchochea matumizi ya teknolojia ya kisasa;
(f) Kulinda viwanda na biashara za ndani dhidi ya ushindani usio haki;

(g) Kudhibiti ubora na viwango vya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini na zile zinazoagizwa kutoka nje;
(h) Kujenga mifumo imara ya soko la ndani na kuhamashisha utafutaji na utumiaji wa fursa nafuu za masoko;
(i) Kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara na taasisi kwa kuwapa fursa za kupata elimu na ujuzi, vitendea kazi na huduma nyinginezo; na
(j) Kujenga uwezo wa Taasisi kuchangia Bajeti ya Serikali na kutoa gawio stahiki.

# 6. MALENGO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA 2020/2021

## 6.1. *Malengo ya Makuu ya Wizara*

231. ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa muhtasari malengo na mikakati ya Wizara itakayotekelezwa kwa mwaka 2020/2021 ni kama ifuatavyo:

(a) Kuendeleza miundombinu ya maeneo ya Uwekezaji nchini;
(b) Kuendeleza utafiti na maendeleo ya teknolojia;
(c) Kuboresha mazingira ya biashara nchini;
(d) Kulinda viwanda na biashara za ndani na kuimarisha ushindani;
(e) Kushughulikia masuala ya ubora na viwango nchini;

(f) Kutafuta fursa za masoko na kuwaunganisha na wazalishaji wa ndani;
(g) Kuwawezesha wajasiriamali kwa kuwapa elimu na mitaji;
(h) Kuendeleza biashara; na
(i) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi.

### *6.1.1. Sekta ya Viwanda*

232. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021 Sekta ya Viwanda itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera (SIDP) na Mikakati ya Mafuta ya Kula, Ngozi, Nguo na Mavazi;
(b) Kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda Nchini;
(c) Kusimamia na Kufuatilia Miradi ya Kimkakati;
(d) Kutekeleza Mkakati wa Kuvilinda Viwanda vya Ndani;
(e) Kuhamasisha Uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Maeneo Maalum ya EPZ/SEZ;
(f) Kuhamasisha Uendelezaji wa Sekta ya Mafuta ya Kula;
(g) Kueneza falsafa ya KAIZEN nchini; na
(h) Kuhamasisha ukuaji wa Sekta ya Viwanda nchini.

### *6.1.2. Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo*

233. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa utengaji na uendelezaji wa maeneo kwa ajili ya uanzishaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI);
(b) Kuratibu uanzishwaji na uendelezwaji wa Kongano za Viwanda kwa ajili ya wajasiriamali;
(c) Kukamilisha marejeo ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na kuandaa mkakati wake;
(d) Kuimarisha/kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali;
(e) Kuendelea kutafuta fursa za masoko ya ndani na nje kwa ajili ya bidhaa za Wajasiriamali;
(f) Kufanya utafiti juu ya mahitaji ya teknolojia (Technology Needs Assessment) kwa ajili ya uanzishawaji na uendelezwaji wa viwanda vidogo na vya Kati;

(g) Kuratibu na kutathmini utendaji wa shughuli za Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO); na
(h) Kuhamasisha urasimishaji wa wajasiriamali wasio rasmi.

### *6.1.3. Sekta ya Biashara*

234. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Sekta ya Biashara itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji nchini;
(b) Kuendeleza majadiliano ya biashara kwenye nchi za China, Urusi, Mauritus, Uturuki, Misri, Israel, DRC Congo, Sudani ya Kusini, Vietnam na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na kuingia nazo makubaliano ya biashara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi;
(c) Kuendelea na majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za

Afrika (Continental Free Trade Area – CFTA);

(d) Kukamilisha majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC;

(e) Kukamilisha majadiliano ya biashara ya huduma kwa sekta sita (6) za kipaumbele katika nchi wanachama wa SADC;

(f) Kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye masuala ya biashara ya bidhaa na huduma;

(g) Kuratibu na kushiriki kwenye majadiliano ya biashara ya kimataifa katika mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa na mengineyo ikiwemo WTO, UNCTAD, CFC na ITC;

(h) Kuhamasisha Jumuiya ya Wafanyabiashara kuhusu fursa za masoko ya upendeleo yatokonayo na majadiliano ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa;

(i) Kukamilisha utungaji wa Sheria ya Kujilinda Kibiashara (Trade Remedies Act);

(j) Kutekeleza Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) unaohusu uwezeshaji wa Biashara;
(k) Kukamilisha mapitio na kuanza utekelezaji wa Sera mpya ya Taifa ya Biashara;
(l) Kuimarisha kamati za kitaifa za kusimamia urahisishaji wa biashara nchini; na
(m) Kuandaa miradi na program mbalimbali kwa ajili ya kujenga uwezo kwa wataalam na Sekta Binafsi;

### *6.1.4. Sekta ya Masoko*

235. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Sekta ya Masoko itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini;
(b) Kuwaunganisha wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara na masoko ya ndani na nje ya nchi;
(c) Kupanua wigo wa Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;
(d) Kuhamasisha na kurahisisha biashara mipakani;

(e) Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania;
(f) Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Masoko; na
(g) Kuandaa na kupitia Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali.

### *6.1.5. Maendeleo ya Rasilimali Watu*

236. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Idara ya Utawala na Rasilimali Watu itatekeleza masuala yafuatayo:-

***Maendeleo ya Rasilimali Watu:***

(a) Kuajiri watumishi wapya 58 wa kada mbalimbali kwa lengo la kuwezesha Idara na Vitengo kuwa na watumishi wa kutosha;
(b) Kupandisha vyeo watumishi 124 wa kada mbalimbali;
(c) Kupeleka watumishi kumi na mmoja (11) katika mafunzo ya muda mrefu, ishirini na watano (25) mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi na ya uongozi na usimimamizi wa mabadiliko (Leadership and Change Management) kwa viongozi zikulingana na majukumu yao;
(d) Kuandaa mpango mpana wa kuendeleza rasilimaliwatu, kuandaa watumishi wanaotarajia kustaafu karibuni na warithi

wanaonyesha kuwa na sifa uwezo utayari (Talent pool) kujaza nafasi zinazoachwa wazi ili kukidhi mahitaji ya kimuundo na malengo ya muda mrefu ya Wizara;

(e) Kutekeleza Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi – MWAMTUKA (OPRAS) kwa kutoa mafuzo ya ujazaji wa fomu, watumishi 204 wanasaini na kufanya mapitio na tathmini ya utendaji ya mikataba yao kwa wakati;

(f) Kuratibu na kusimamia masuala yote ya uendeshaji na utendaji kazi wa watumishi katika shughuli za Wizara;

(g) Kutoa huduma stahiki kwa viongozi na watumishi wa Wizara kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali katika Utumishi wa Umma;

(h) Kuandaa programu mbalimbali za michezo kama vile mabonanza na kushiriki katika mashindano ya SHIMIWI kwa lengo la kujenga afya za watumishi, kuongeza ushirikiano na kufahamiana; na

(i) Kuhakikisha watumishi watakaohitimisha ajira zao wanalipwa mafao kwa wakati.

***Masuala Mtambuka:***

(a) ***Rushwa:*** Kuendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi kwa kuweka mikakati mbalimbali na kutoa mafunzo juu ya Sheria Kanuni na Taratibu kuhusu uzingatiaji wa maadili, uwajibikaji na

utoaji huduma bora katika utumishi wa umma na kuhakikisha zinafuatwa na watumishi wote. Vilevile, Wizara kupitia Dawati la Malalamiko itaendelea kukusanya na kupokea malalamiko na kero kutoka kwa wateja wa ndani na nje ya ofisi kwa lengo la kuzitatua ikiwa ni njia mojawapo ya kudhibiti na kupambana na rushwa mahali pa kazi.

(b) ***UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza:*** Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na maambukizi ya VVU mahala pa kazi kwa kuzingatia Waraka wa Utumishi Na. 2 wa mwaka 2014 kuhusu Kudhibiti Virusi vya UKIMWI, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma na kuwahudumia watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na waliojiweka wazi. Aidha, Wizara itaendesha Semina kwa watumishi ikiwa ni njia ya uhamasishaji na uelimishaji wa masuala ya UKIMWI pamoja na upimaji afya wa hiari ili kudhibiti UKIMWI na Magonjwa sugu yasiyoambukizwa mahala pa kazi.

(c) ***Masuala ya Jinsia:*** Wizara kupitia Dawati la Jinsia itaendelea kuratibu masuala ya kijinsia na kuyahuisha kwenye sera, mipango, mikakati na program za Wizara pamoja na Taasisi zake katika Mwaka 2020/2021.

### *6.1.6. TEHAMA na TAKWIMU*

237. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/ 2021, Wizara kupitia Kitengo cha TEHAMA na Takwimu kitatekeleza masuala yafuatayo:-

(a) Kusimamia matumizi bora na sahihi ya miundombinu ya TEHAMA katika kutoa huduma ndani na kwa wateja wa nje;
(b) Kuboresha miundombinu ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi kwa wafanyakazi katika utoaji wa huduma kwa umma;
(c) Kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu matumizi bora na sahihi ya Miundombinu na Rasilimali za TEHAMA; na
(d) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji Takwimu/taarifa za Viwanda, Biashara na Masoko.

### *6.1.7. Ununuzi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha*

238. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Kitengo cha Ununuzi kitaendelea kusimamia shughuli za ununuzi wa bidhaa na huduma kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya Mwaka 2011 na kanuni zake GN Na, 446 ya Mwaka 2013, kama zilivyo fanyiwa marekebisho mwaka 2016 pamoja na

miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Udhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA). Masuala yafuatayo yatatekelezwa:-

a) Kuandaa Mpango wa Ununuzi kwa mwaka 2020/2021;
b) Kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma kupitia Mfumo wa Kielektroniki (Tanzania Electronic Procurement system - TANePS);
c) Kuratibu vikao vinne (4) vya Bodi ya Zabuni ya Wizara kwa mwaka 2020/2021;
d) Kuandaa taarifa za ununuzi za kila mwezi, robo pamoja na taarifa ya mwaka na kuziwasilisha Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA); na
e) Kuhakiki mali za Wizara, kuhuisha taarifa za Daftari la Mali la Wizara kwa mujibu wa Muongozo wa Mali za Serikali wa mwaka 2019 pamoja na Sheria ya Fedha Na. 6 ya mwaka 2001 na Kanuni zake, GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

## 6.2. *MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021*

### *6.2.1.* Taasisi za Kuendeleza Uwekezaji

#### *i) Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)*

239. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la Taifa la

Maendeleo (NDC) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuanzisha Kilimo shirikishi cha Ufuta na Mawese (Block farming) katika mikoa ya Pwani na Kigoma;
(b) Kuzalisha zana ndogo ndogo za kilimo na Vipuri kwa kushirikiana na Taasisi za Utafiti na KMTC;
(c) Kuanzisha Kiwanda cha Mbolea na Upimaji wa afya ya Udongo;
(d) Kuanza utekelezaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga;
(e) Kukamilisha tafiti za mradi wa Magadi soda na kujenga kiwanda Engaruka;
(f) Kuendelea na Utekelezaji wa Mradi wa Matrekta ya URSUS;
(g) Kufanya ukarabati wa kiwanda cha KMTC kwa kujenga *foundry* na kubadilisha baadhi ya mashine;
(h) Kufufua na kuendesha Kiwanda cha Matairi cha Arusha bila kutegemea wawekezaji binafsi; na
(i) Kuchimba makaa ya mawe Katewaka.-

***ii) Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi (EPZA)***

240. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa Mauzo Nje ya

Nchi (EPZA) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Uendelezaji wa miundombinu ya msingi katika maeneo yaliyokwishalipiwa fidia, maeneo yanayosimamiwa na Serikali za Mikoa na Halmashauri pamoja na maeneo yanayoendelezwa na Sekta binafsi;
(b) Kuweka alama na kuimarisha ulinzi katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi yaliyokwishalipiwa fidia ili yasivamiwe;
(c) Kuhamasisha uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi SEZ;
(d) Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi iliyo chini ya SEZ - (Monitoring and Evaluation);
(e) Kupitia Sheria zinazosimamia Mamlaka ya EPZ ili kuendana na wakati;
(f) Kuboresha mifumo ya utoaji huduma kwa kutumia TEHAMA; na
(g) Kuimarisha Rasilimali Watu katika Mamlaka ya EPZ.

### ***6.2.2. Taasisi za Utafiti, Maendeleo ya Teknolojia na Mafunzo***

#### ***i) Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)***

241. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) itatekeleza malengo yafuatayo:

(a) Kuendeleza Mitaa ya Viwanda ya SIDO na kutengeneza Mfumo Unganishi wa shughuli za TEHAMA za Shirika;

(b) Kuhawilisha teknolojia kwa Kuimarisha vituo vya uendelezaji teknolojia (TDCs) na Vituo vya mafunzo na uzalishaji (TPC) vya SIDO;

Kutunisha Mtaji wa Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi (NEDF); na

(c) Kuanzisha kituo kimoja cha kutengeneza vifungashio na kununua kwa wingi na kuimarisha usambazaji wa vifungashio kwa wajasiriamali mikoa yote.

### *ii) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)*

242. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kutoa huduma za kitaalam viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira pia zinazolenga matumizi bora ya nishati;

(b) Kuendelea na mchakato wa kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Ngozi jinsi ya kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuhifadhi na

kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama 'Leather boards';

(c) Kuendelea na kukamilisha mchakato wa kuhakiki (Accreditation) na kuboresha maabara ya chakula na mazingira ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;
(d) Kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuleta teknolojia mpya za uzalishaji;
(e) Kuendelea kukamilisha marejeo ya Sheria ya Bunge Na.5 ya mwaka 1979 iliyoanzisha TIRDO kwa kufuatilia ripoti ya mapitio ya Sheria iliyokwishawasilishwa Wizara mama na hatimaye kupelekwa Bungeni, na
(f) Kukamilisha Jengo la Utawala (Complete and furnish TIRDO administration block for Industrial Clinic, ICT and Information Centre).

### *iii) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)*

243. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya uchunguzi wa namna bora ya kudhibiti kinyesi cha kuku wanaofugwa kwenye viota (cage) katika eneo finyu

kwenye miji na maeneo yanayozunguka miji ili kutunza na kuboresha usafi wa mazingira;

(b) Kubuni na kuunda teknolojia ya kutenganisha maganda na kiini cha mbegu ya chikichi ambayo inahamishika;

(c) Kuunda teknolojia ya Kipandio kinachofaa kupanda mbegu za ufuta, alizeti, pamba na karanga ili kuchangia kuongeza uzalishaji wa mazao yenye kutoa mafuta ya kula nchini;

(d) Kufanya usanifu wa teknolojia ili kufikia hatua bora kabisa (design optimization) na kuziingiza kwenye soko la wadau;

(e) Kufanya tathmini ya mahitaji ya teknolojia katika hali ya uchimbaji madini kwa wachimbaji wadogo;

(f) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Wajasiriamami wadogo 5 wanaojishughulisha na ubunifu na utengenezaji wa zana za kilimo na teknolojia za vijijini;

(g) Kuanzisha Vituo vya Ukaguzi na Majaribio katika maeneo matatu (3) muhimu ya Bandari na mipakani ambayo ni Bandari ya Dar es Salaam, Horohoro mkoani Tanga, naTunduma mkoani Songwe;

(h) Kununua vifaa, mitambo, machine na magari ya kusaidia kufanikisha kazi za ukaguzi na majaribio ya Zana za Kilimo na teknolojia za vijijini;

(i) Kujenga ufahamu na kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Majaribio na Ukaguzi wa zana za Kilimo na teknolojia za vijijini; na
(j) Kujenga uwezo wa rasilimali watu kwenye Kada ya utafiti na wafanyakazi wengine wasio watafiti kwa kuwapa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

***iv) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO)***

244. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO) litatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea na uboreshaji wa karakana na ofisi ya usanifu pamoja na miundombinu ya Taasisi kwa ujumla;
(b) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Taasisi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kuboresha utendaji kazi;
(c) Kuendeleza ubunifu na kutengeneza chasili cha mtambo wa kuchakata na kukausha mazao ya kilimo (Muhogo) na kukausha korosho pamoja na kubangua (drying and scooping) ili kuongeza thamani;
(d) Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo mdogo wa kuchakata miwa na kutengeneza sukari (Mini/small scale sugar processing technology);
(e) Kuendeleza ubunifu na maboresho katika

utengenezaji wa mtambo wa kukamua na kusindika mafuta ya mbegu za alizeti;

(f) Kusanifu na kuendeleza chasili cha mtambo wa kuchakata michikichi ili kupata mafuta ya kula pamoja na mazao yake mbalimbali;

(g) Kuendeleza ubunifu na maboresho ya kutengeneza mtambo wa kuteketeza taka ngumu za hospitali (Existing biomedical solid waste incinerator) ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi pamoja na kuweza kutumika katika kuteketeza/kuchoma damu zisizo salama na madawa ya hospitali yaliyokwisha muda wake kwa kiwango cha nyuzi joto 1500 – 2000 (Ni maombi ya MSD kusanifu "incinerator" hiyo);

(h) Kubuni na kuendeleza chasili cha jokofu la ngazi tatu la kuhifadhi maiti katika hospitali;

(i) Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo wa kuchakata zao la mkonge;

(j) Kuhawilisha teknolojia na kuhamasisha utengenezaji kibiashara wa mitambo iliyobuniwa na Taasisi ukiwemo mtambo wa kusindika mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za mchikichi; na

(k) Kujitangaza ili kujenga uelewa kwa umma kuhusu shughuli zinazofanywa na Taasisi ya TEMDO kwa kushiriki kwenye maonesho angalau manne ya teknolojia/biashara (kama vile DITF, Nane nane, Maonesho ya kanda ya SIDO, n.k).

### *v) Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)*

245. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kuendeleza rasirimali watu hasa katika hatua ya shahada za Uzamivu;
(b) Kufanya upembuzi yakinifu katika kuboresha makazi ya watumishi katika eneo la Oysterbay Dar es Salaam;
(c) Kuimarisha na kuboresha mifumo ya TEHAMA;
(d) Kufanya ukarabati mkubwa wa minudombinu ya kufundishia na kujifunzia, Kampasi ya Dar es salaam na Dodoma; na
(e) Ujenzi wa Kampasi ya Mbeya.

## *6.2.3. Taasisi za Ushindani na Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa na Huduma*

### *i) Shirika la Viwango Tanzania (TBS)*

246. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutayarisha viwango 500 vya kitaifa katika sekta ndogo, ambavyo kati ya hivyo 260 ni

vya uhandisi (Engineering) na 240 ni vya usindikaji (Process Technology);

(b) Kutoa leseni ya ubora kwa bidhaa 500 kutoka katika sekta mbalimbali zikiwemo bidhaa za wajasiriamali wadogo (SMEs);

(c) Kusajili na Kutoa vibali 5,900 vya chakula na maeneo ya uzalishaji;

(d) Kusajili na Kutoa vibali 5,400 vya vipodozi na maeneo ya uzalishaji;

(e) Kukagua ubora wa bidhaa 39,000 zitokazo nchi za nje kabla ya kuingia nchini (Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards- PVoC (CoCs));

(f) Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa leseni za ukaguzi 43,000 za magari yaliyotumika (used motor vehicles) yanayoingizwa nchini;

(g) Kutoa mafunzo na semina 120 kuhusu viwango na udhibiti wa ubora (Quality Assurance Training) kwa wadau mbalimbali;

(h) Kupima sampuli 25,000 za bidhaa mbalimbali;

(i) Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 8,000;

(j) Kuanzisha ofisi mbili za mipakani; na

(k) Kuanza ujenzi wa Viwango House Dodoma.

### *ii) Wakala wa Vipimo (WMA)*

247. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo

(WMA) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia, kuhakiki na kukagua vipimo vyote vitumikavyo na viingiavyo nchini kwa lengo la kumlinda mlaji;
(b) Kuendelea na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya mipakani, bandarini na viwandani kwa lengo la kuhakiki usahihi wa kiasi/ idadi iliyotamkwa (decraled quantity);
(c) Kununua vitendea kazi yakiwemo magari Mawili na vitendea kazi vya kitaalam;
(d) Kuongeza idadi ya watumishi 300 (Maafisa Vipimo 200, Maafisa Vipimo wasaidizi 50 na Madereva 50);
(e) Kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo; na
(f) Kuwajengea uwezo (*Capacity building*) watumishi wa Wakala wa Vipimo kwa kuwapeleka mafunzo ndani na nje ya nchi ili kuongeza elimu na ujuzi.

### ***iii) Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)***

248. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya maboresho makubwa ya Mifumo a ya mitandao ya ORS na NBP ili kuwa rafiki

zaidi kwa watumiaji na kutoa huduma bora na kuleta tija;

(b) Kuendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Biashara nchini na kuweka taratibu za ushirikiano katika utoaji huduma na Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa Biashara ili kuweza kuwahudumia wananchi katika maeneo yao kwa urahisi;

(c) Kukamilisha mapitio ya sheria zote zinazosimamiwa na Wakala ikiwa ni pamoja na kuanzisha Daftari la kuwatambua Wanufaika wa mwisho wa Makampuni (Beneficial Ownership Register);

(d) Kuendelea kuelemisha umma juu ya umuhimu wa kufanya sajili mbalimbali za kibiashara zinazofanywa na Wakala na urasimishaji wa Biashara kwa ujumla katika ngazi za Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na Maafisa Biashara kote nchini; na

(e) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi pamoja na mafunzo kwa watumishi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi kwa wateja.

***iv) Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)***

249. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imepanga

kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kujenga uwezo wa Bodi kuwezesha usimamizi wa majukumu yake kikamilifu kwa kuomba muundo mpya, ajira zaidi za watumishi, vitendea kazi na kubuni vyanzo vya mapato;
(b) Kushirikiana na wadau mbalimbali kuwezesha mazao yanayohifadhiwa kupitia mfumo wa stakabadhi kuuzwa kupitia soko la mazao na bidhaa (commodity exchange market) ili kuongeza ushindani, kupunguza gharama za uendeshaji na urasimu katika kuwalipa wakulima;
(c) Kuimarisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi kwa mazao ya nafaka hususan mahindi na mpunga ili kufanikisha biashara ya mazao haya kwenda nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki/SADC;
(d) Kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika maeneo yanayozalisha mazao ya chai, pamba, ufuta, dengu, mbaazi, soya, mahindi na mpunga katika mikoa ya Mbeya, Dodoma, Pwani, Lindi, Ruvuma, Iringa, Njombe, Rukwa, Sumbawanga, Songwe, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Tabora na Mara;
(e) Kuendelea kuimarisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi za ghala kwa

mazao ya korosho, ufuta na kahawa kwa kukamilisha viwango vya mazao hayo, na kuboresha mfumo wa mauzo;

(f) Kuanzisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi kwa kuwezesha mazao ya chai, pamba, dengu na mbaazi kutumika katika mfumo huu; na

(g) Kuhamasisha wahisani wa maendeleo, sekta binafsi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kujenga ghala zinazofaa kwa matumizi ya mfumo wa stakabadhi za ghala.

***v) Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA)***

250. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha na kutumia kwa mfumo wa kieletroniki ili kurahisisha zoezi la usajili wa wabunifu wa hakimiliki na hakishiriki na kazi zao;

(b) Kushiriki katika marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7/1999 kupitia Sheria ya Mazingira ya Ufanyaji Biashara (Ease of doing business) na utekelezaji wa marekebisho ya Sheria hiyo;

(c) Kutoa elimu kwa umma kuhusiana na mfumo wa usajili na masuala ya Hakimiliki na Hakishiriki;

(d) Kukamilisha Kanuni za ukaguzi na kufanya ukaguzi wa kazi zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki (anti piracy raids) katika utekelezaji wa marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki;

(e) Kukamilisha na kuanza kutumika kwa Kanuni za *Resale rights* kwa kazi za sanaa za ufundi; na

(f) Kushughulikia migogoro na kesi za Hakimiliki na Hakishiriki ndani na nje ya Tanzania na kukuza ushirikiano na usimamizi wa migogoro hii kwa ushirikiano na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (World Intellectual Property Organization – WIPO).

**vi) *Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE)***

251. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha upatikanaji wa Masoko na kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania katika masoko ya nje kwa kuimarisha

inteligensia ya biashara, kuanzisha madawati ya biashara ubalozini katika nchi za kimkakati na kutangaza bidhaa kupitia Maonesho, misafara na mikutano ya biashara;

(b) Kuimarisha sekta ndogo ya biashara (SMEs) ili iweze kujiendesha kiushindani kwa kutoa mafunzo, kuimarisha na kuanzisha vikundi vya kibiashara na kuendeleza bidhaa zenye fursa katika masoko ya nje;

(c) Kuimarisha biashara Zanzibar kwa kutafuta masoko yenye tija ya bidhaa za kimakakati (viungo, chumvi, dagaa na mwani) na kujenga uwezo wa wazalishaji kuwa na ushindani;

(d) Kuimarisha biashara za mipakani kwa kuimarisha mfumo shirikishi wa upokeaji malalamiko ya kero za biashara mipakani, kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara, na kuimarisha Kamati za Pamoja na Vyama vya wafanyabiashara za Mpakani;

(e) Kusimamia uendeshaji wa Maonesho nchini kwa kukamilisha uandaaji wa kanuni za kusimamia Maonesho nchini; kudhiti uratibu wa maonesho kwa kutoa vibali vya kuandaa maonesho, kusimamia ratiba ya maonesho na kusimamia ubora wake;

(f) Kushiriki katika utekelezajia wa BLUEPRINT kwa kuandaa mfumo wa

kubaini vikwazo na kero za ufanyaji biashara nchi na kuratibu uendeshaji wa Klinik ya Biashara ya Biashara; na

(g) Kuimarisha Uwezo wa Taasisi kujiendesha kiushindani kwa kuimarisha vyanzo vya mapato.

### *vii) Tume ya Ushindani (FCC)*

252. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kuboresha hali ya ushindani katika soko (Competition Protection and Promotion improved) kupitia;

(b) Kumlinda mlaji dhidi ya mienendo hadaifu (Consumer Protection Enhanced) kupitia; na

(c) Kuongeza ufanisi katika kutoa huduma (Service delivery capacity improved) kupitia.

### *viii) Baraza la Ushindani (FCT)*

253. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Baraza la Ushindani (FCT) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri ya rufaa yanayowasilishwa

katika Baraza ambapo lengo letu ni kutoa maamuzi ya mashauri 65 kwa mwaka 2020/2021;

(b) Kuimarisha uwezo wa kutekeleza majukumu ya Baraza. Hii ikiwa pamoja na uboreshaji wa mifumo ya Baraza (ikiwemo: *case management sysytem*; na *information management system*); na Mafunzo ilikuongeza kasi ya usikilizwaji wa mashauri yanayowasilishwa katika Baraza;

(c) Kuendelea kufanya utafiti wa kisheria na kiuchumi katika ushindani na udhibiti kwa ajili ya kusaidia katika uendeshaji wa mashauri ya Baraza;

(d) Kuongeza uelewa kwa Wadau wengi zaidi na Jamii kwa ujumla juu ya shughuli za Baraza na haki katika ushindani wa soko;

(e) Kuboresha vitendea kazi vya Baraza; na

(f) Kushughulikia masuala Mtambuka.

## 7. MAKADIRIO YA MAKUSANYO NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

### 7.1. *Makusanyo ya Serikali*

254. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2020/2021, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya Shilingi 15,000,000 kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na

makusanyo mengine. Kati ya fedha hizo, Shilingi 9,000,000 zitakusanywa katika Fungu 44 na Shilingi 6,000,000 zitakusanywa katika Fungu 60.

### 7.2. *Maombi ya Fedha*

255. ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa mwaka 2020/2021, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya Shilingi 81,366,902,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 51,679,016,000 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 29,687,886,000 ni za Matumizi ya Maendeleo. Aidha, katika Bajeti hiyo, Shilingi 57,414,395,000 ni za Fungu 44 na Shilingi 23,952,507,000 ni za Fungu 60.

## 8. **SHUKRANI**

256. ***Mheshimiwa Spika;*** Ujenzi wa uchumi wa viwanda ni shirikishi na jumuishi, hivyo huhitaji ushiriki wa wadau mbalimbali. Kwa kutambua umuhimu huo, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati washirika wetu wa maendeleo, zikiwemo nchi rafiki ambazo ni Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, tunayashukuru Mashirika ya Kimataifa ikiwa ni

pamoja na: ARIPO, Benki ya Dunia, CFC, DANIDA, DFID, EU, FAO, IFAD, JICA, Jumuiya ya Madola, KOICA, SIDA, Taasisi za Umoja wa Mataifa (UNCTAD, UNDP, UNIDO, UNWOMEN), USAID, WIPO, FSDT, TMEA, SADC na WTO. Vilevile, nashukuru taasisi zote, Sekta Binafsi, taasisi zisizo za kiserikali (CBOs & FBOs) kwa kuwa sehemu muhimu ya ujenzi wa uchumi wetu. Kama nchi, tunaendelea kutegemea ushirikiano wenye tija katika kufikia malengo endelevu ya jamii nzima ya Watanzania.

257. ***Mheshimiwa Spika;*** Naomba nihitimishe kwa kuwashukuru tena Watanzania na hasa Wazalendo wa nchi yetu ya Tanzania kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na hivyo kuwa kichocheo cha kukua kwa sekta nyingine za uchumi. Ni dhahiri kuwa Taifa kwa kipindi hiki kinahitaji kuendeleza ari hiyo katika kupambana na majanga mbalimbali ikiwemo ugonjwa wa mafua makali wa CORONA. Kwa pamoja tuungane kujikinga na kulindana ili Taifa libaki salama na likiwa na nguvukazi ya kutegemewa.

## 9. HITIMISHO

258. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara ninayoisimamia imeazimia kuendeleza maamuzi makini na yenye mashiko ya Serikali ya Awamu

ya Tano ya kujenga uchumi wa viwanda wenye mafanikio ambayo yanajitafsiri katika ubora wa maisha ya kila mwananchi na Taifa kwa ujumla. Hivyo, Sera, Sheria na Mikakati iliyopo itaendelea kuboreshwa ili kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kuchochea mbinu za utekelezaji ili kufikiwa kwa malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. Ni dhahiri kuwa jitihada hizo pamoja na utekelezaji wa *Blueprint* utatutoa hapa tulipo na kutupaisha katika maendeleo na kufikia lengo la uchumi wa kati kama ilivyoazimiwa na Dira ya Taifa ya 2025. Ni dhahiri kuwa tunahitaji ushiriki usio na shaka wa kila Mtanzania, wadau wa sekta na washirika wa maendeleo. Inawezekana, endapo kila mmoja wetu atachukua nafasi yake na kujituma ipasavyo.

## 10. MAOMBI RASMI YA FEDHA

259. ***Mheshimiwa Spika;*** Naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 15,000,000 na matumizi ya jumla ya Shilingi 81,366,902,000 kwa mwaka 2020/2021.

## 11. **MWISHO**

260. ***Mheshimiwa Spika;*** Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara yenye anuani ifuatayo: www.mit.go.tz.

261. ***Mheshimiwa Spika;*** Naomba kutoa hoja.

**_KIAMBATISHO Na. 1_**

***Mwenendo wa Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa***

| **Mwaka** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Asilimia** | 7.86 | 7.81 | 7.67 | 8.05 | *8.5* |

**Chanzo:** *Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS)*

**_KIAMBATISHO Na. 2_**

***Ukuaji wa Sekta ya Viwanda***

| **Mwaka** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Asilimia** | 7.1 | 10.8 | 8.2 | *8.3* | *5.8* |

***Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS)***

**Kiambatisho Na. 3**

***Idadi ya Ghala yaliyokusanya Mazao kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala Msimu wa 2019/2020***

| Na. | Zao | Mkoa | Idadi ya Ghala | Kiasi (Kg) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Korosho | Ruvuma, Pwani, Lindi na Mtwara. | 27 | 219,889,211 |
| 2. | Dengu | Manyara. | 1 | 80,804 |
| 3. | Kakao | Mbeya. | 2 | 7,126,355 |
| 4. | Choroko | Shinyanga, Mwanza na Tabora. | 5 | 396,959 |
| 5. | kahawa | Mbeya, Songwe, Kilimanjaro na Ruvuma. | 4 | 3,131,094 |
| 6. | Mbaazi | Ruvuma. | 2 | 775,543 |
| 7. | Ufuta | Ruvuma, Dodoma na Manyara. | 6 | 5,926,726 |
| 8. | Soya | Ruvuma. | 4 | 2,892,004 |
| | **Jumla** | | **51** | **240,218,696** |

***Chanzo: Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, 2020***

**KIAMBATISHO Na. 4**

**VIWANDA VYA KUTENGENEZA DAWA VIFAA NA VIFAA TIBA NCHINI**

| NA | JINA LA KIWANDA | MKOA |
|---|---|---|
| 1 | Keko Pharmaceutical Industries (1997) Limited, | Dar es Salaam |
| 2 | Mansoor Daya Chemicals Limited, | Dar es Salaam |
| 3 | A.A Pharmaceuticals Limited | Dar es Salaam |
| 4 | Msagara Investment Ltd | Dar es salaam |
| 5 | Afya Laboratories Limited, | Dar es Salaam |
| 6 | Shelys Pharmaceutical Limited, | Dar es Salaam |
| 7 | Tanzania Pharmaceutical Industries Limited, | Arusha |
| 8 | Prince Pharmaceuticals Ltd | Mwanza |
| 9 | Zenufa Laboratories Limited, | Dar es Salaam |
| 10 | Sri Balaj Ltd | Dar es salaam |
| 11 | S.G Star Pharmaceuticals Ltd | Dar es salaam |
| 12 | Tanzania Vaccines Institute | Pwani |
| 13 | Jeffery Medical Device Company | Dar es salaam |
| 14 | TPI ARVs Ltd | Arusha |

*KIAMBATISHO NA 5*

**VIWANDA VINAVYOTENGENEZA SANITIZER (VITAKASA MIKONO, BARAKOA NA VIFAA MAALUM KWA WATOA HUDUMAZA AFYA )**

| Na. | Jina La kiwanda | Bidhaa | Mkoa |
|---|---|---|---|
| | Mansoor Daya Chemicals Limited | Vitasa Mikono | Dar es Salaam |
| 2. | Shelys Pharmaceutical Limited | Vitasa Mikono | Dar es Salaam |
| 3. | A.A Pharmaceuticals Limited | Vitasa Mikono | Dar es Salaam |
| 4. | Sri Balaj Ltd | Vitasa Mikono | Dar es Salaam |
| 5. | Keko Pharmaceutical Industries (1997) Limited | Vitasa Mikono | Dar es Salaam |
| 6. | Sterling Surfactants Limited | Vitasa Mikono | Dar es Salaam |
| 7. | Natural Products Limited | Vitasa Mikono | Dar es Salaam |
| 8. | Chemi & Cotex | Vitasa Mikono | Dar es Salaam |
| 9. | Afrikana Ltd | Vitasa Mikono | Dar es Salaam |
| 10 | Pristine Manufacturer Company | Barakoa | Dar es Salaam |
| 11 | Fiverstar Ltd | Barakoa | Dar es Salaam |
| 12 | Hospital ya Taifa ya Rufaa Muhimbili | Mavazi maalum kwa ajili ya Wahudumu wa afya | Dar es Salaam |

*Kiambatisho Na. 6*

## 4. VIWANDA VILIVYOANZA UJENZI NA HATUA WALIYOFIKIA

| Na. | Jina la Kiwanda | Mahali kilipo | | Aina ya dawa zinazorajiwa kutengenezwa | Hatua ya Ujenzi iliyofikiwa | Changamoto |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mkoa | Wilaya/ Eneo | | | |
| 1 | Kairuki Pharmaceuticals Industry Ltd (KPIL) | Pwani | Kitalu Na. 192, eneo la viwanda Zegereni, Mji wa Kibaha, | Dawa za binadamu za sindano za ujazo mkubwa *(large volume parenterals/IV fluids)* | • Ujenzi umekamilika kwa asilimia 75<br>• Majengo ya kuzalisha dawa, ghala la kuhifadhia malighafi, dawa na utawala yameezekwa<br>• Ujenzi wa kutenganisha vyumba katika majengo unaendelea<br>• Baadhi ya mashine zimenunuliwa na zinatarajiwa kuwasili nchini mwezi April, 2020 | • Barabara ya kwenda eneo la Zegereni kutoka barabara kuu ya Morogoro ni mbovu na haipitiki kirahisi hususan wakati wa mvua, hii imesababisha usafirishaji wa mashine na vifaa vya ujenzi kuwa mugumu<br>• Kutokuwepo kwa umeme wa uhakika kutoka TANESCO, kwani hadi sasa *transformer* halijasimikwa kwa ajili ya kutoa huduma ya umeme katika viwanda vinavyojengwa eneo la Zegereni<br>• Kutokuwepo kwa gesi asilia katika maeneo ya ujenzi ili kupunguza gharama za umeme |
| 2 | Biotec Laboratories Ltd | Pwani | Kitalu Na. 60 & 62, eneo la Lulanzi, Mji wa Kibaha | Dawa za maji ( *Oral liquids)* na unga ( *Powder )* za mifugo | • Ujenzi umekamilika kwa asilimia 90<br>• Usimikaji wa mifumo ya hewa (*HVAC*) na umeme unaendelea<br>• Baadhi ya mashine kama vile *mixers*,zimesimi kwa<br>• Ukarabati wa baadhi ya maeneo kama vile *sampling area*, sakafu na kuta unaendelea | • Kutokuwepo kwa gesi asilia katika maeneo ya ujenzi ili kupunguza gharama za umeme |
| 3 | VistaPharma Ltd | Pwani | Kitalu Na. 4, Eneo la viwanda, Zegereni, Mji wa Kibaha, | Dawa za binadamu za maji *(Oral liquids)* na vidonge *(Tablets)* | • Ujenzi umekamilika kwa asilimia 70<br>• Ujenzi wa sakafu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2020<br>• Ununuzi wa mashine umefanyika na zinatarajiwa kuwasili nchini mwishoni mwa mwezi Aprili, 2020 | • Barabara ya kwenda eneo la Zegereni kutoka barabara kuu ya Morogoro ni mbovu na haipitiki kirahisi hususan wakati wa mvua, hii imesababisha usafirishaji wa mashine na vifaa vya ujenzi kuwa mugumu<br>• Kutokuwepo kwa umeme wa uhakika kutoka TANESCO, kwani hadi sasa *transformer* halijasimikwa kwa ajili ya kutoa huduma ya umeme katika viwanda vinavyojengwa eneo la Zegereni<br>• Kutokuwepo kwa gesi asilia katika maeneo ya ujenzi ili kupunguza gharama za umeme<br>• Kuwepo kwa hali ya uchavuzi wa mazingira kutokana na moshi |

| Na. | Jina la Kiwanda | Mahali kilipo | | Aina ya dawa zinazorajiwa kutengenezwa | Hatua ya Ujenzi iliyofikiwa | Changamoto |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mkoa | Wilaya/ Eneo | | | |
| | | | | | | unaotoka katika kiwanda kimojawapo kinachotengeneza nondo ambacho kipo karibu na kiwanda hiki |
| 4 | Hester Biosciences Africa Ltd | Pwani | Kitalu Na. 11&12, Tamco Industrial Estate – Kibaha Mji wa Kibaha | Dawa za chanjo za mifugo *(Veterinary Vaccines)* | • Ujenzi umekamilika kwa asilimia 70<br>• Uzimikaji wa mifumo ya hewa (HVAC) unaendelea<br>• Baadhi ya watalaam kama vile, *mechanical engeneers, microbiologist* wameajiriwa na kupata mafunzo nchini india<br>• Kinatarajia mwezi Juni, 2020 kutoa toleo la kwanza la dawa chini ya utaratibu wa *toll manufacturing* | • Maji ya mvua hukusanyika ndani ya eneo la kiwanda kutoka kwenye barabara |
| 5 | Afrikana Pharmaceuticals Ltd | Pwani | Kisemvule, Mkuranga | Dawa za kupaka *(topical formulations)* kwa matumizi ya binadamu | • Ujenzi wa kiwanda cha dawa bado kuanza, kinasubiri fedha kutoka kwa wabia<br>• Kwa sasa kinazalisha bidhaa aina ya vipodozi na *antiseptics* | • Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda |
| 6 | Alfa Pharmaceuticals Ltd | Dar es Salaam | Kitalu Na. 14, eneo la viwanda-Mbagala, Temeke | Kikikamilika kitatengeneza dawa za binadamu za sindano za ujazo mkubwa *(large volume parenterals/IV fluids)* | • Ujenzi umekamilika kwa asilimia 90<br>• Ununuzi wa baadhi ya mashine za uzalishaji dawa umefanyika na tayari zimewasili kiwandani ili kuanza kusimikwa<br>• Uzalishaji unatarajiwa kuanza katikati ywa mwaka 2020 | • Barabara kwenda kiwandani kutoka barabara kuu ya Mbagala ni mbovu, hivyo kusababisha ugumu wa usafirishaji wa vifaa vya ujenzi |
| 7 | Afravet/Novel Vaccines and Biological Company Ltd (NOVABI) | Morogoro | Kitalu Na. 91-96, Ploti A, Kihonda, Manispa a ya Morogoro | Chanjo za Mifugo *(Veterinary Vaccines)* | • Ukarabati wa kiwanda unaendelea ili kukidhi matakwa na GMP | • Matakwa ya GMP hayajaweza kufikiwa kwa kiwango cha kuridhisha kwa kuwa jengo lilijengwa hapo awali kama maabara ya kupima chanjo za mifugo |
| 8 | Farm Access Limited | Arusha | Ngaramtoni Ilkiushin, Arumeru | Kitatengeneza dawa za mifugo za maji *(Oral Liquids )* na unga *(powder)* | • Ukarabati wa jengo na usimikaji wa mashine za uzalishaji umefanyika kwa | • Kutokuwa na *transformer* kutoka TANESCO kwa ajili ya shughuli za kiwanda |

| Na. | Jina la Kiwanda | Mahali kilipo | | Aina ya dawa zinazorajiwa kutengenezwa | Hatua ya Ujenzi iliyofikiwa | Changamoto |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mkoa | Wilaya/ Eneo | | | |
| | | | | | asilimia 100<br>• Ujenzi wa maabara ya microbiolojia kwa kutenganisha vyumba mahususi unaendelea kufanyika<br>• Baadhi ya wafanyakazi wameajiriwa<br>• Kiwanda tayari kimepewa hati ya usajili wa majengo kutoka TMDA<br>• Baadhi ya nyaraka muhimu zinaandaliwa kama vile taratibu sanifu za uzalishaji ( *SOPs*), *dossier* kwa ajili ya kuomba usajili wa bidhaa na kuanza uzalishaji | |
| 9 | Cure Afya Pharmaceuticals Ltd | Dar es Salaam | Kitalu Na. 69, Ploti A, Eneo la Kimbiji, Manispaa Kigamboni | Dawa za binadamu za sindano za ujazo mkubwa *(large volume parenterals/IV fluids)* | • Ujenzi wa sakafu kwa ajili ya kusimika kiwanda umeanza mwezi Januari , 2020<br>• Kiwanda kinategemewa kukamilika kujengwa mwaka 2021 | • Kipo katika hatua za awali za ujenzi, changamoto bado kujulikana |
| 10 | Emedics Pharmaceuticals Ltd | Pwani | Kerege, Bagamoyo | Dawa za binadamu za kupaka(*External preparations*), Vidonge, Krimu na *Ointments* | • Ujenzi umekamilika kwa asilimia 70<br>• Baadhi ya Mashine za kuzalishia dawa zimenunuliwa, zinasubiri kukamilisha taratibu za forodha kuingizwa nchini | • Kukosekana kwa watalaam wenye kuchora michoro yenye viwango vya GMP |

| Na. | Jina la Kiwanda | Mahali kilipo | | Aina ya dawa zinazorajiwa kutengenezwa | Hatua ya Ujenzi iliyofikiwa | Changamoto |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mkoa | Wilaya/ Eneo | | | |
| 11 | Vine Vision Infusion Ltd | Arusha | Kitalu Na. 1053 Moshomo, Manispaa ya Arusha | Dawa za binadamu za Macho | • Ujenzi umekamilika kwa asilimia 60<br>• Baadhi ya Mashine za kuzalishia dawa zimenunuliwa, zinasubiri taratibu za forodha kuingizwa nchini | • Kukosekana kwa watalaam wa kuchora michoro yenye viwango vya GMP |

***Kiambatisho Na. 7***

## *Biashara kati ya Tanzania na nchi mbalimbali kwa mwaka 2013 – 2019 (Dola za Marekani '000,000')*

*Jedwali Na1:* Biashara kati ya Tanzania na Nchi Nyingine (Preferential Markets) kwa mwaka 2008 – 2019 (Dola za Kimarekani '000,000)

| Na | Nchi | Maelezo | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **China** | Bidhaa zilizouzwa | 223.5 | 363.9 | 634.2 | 659.2 | 520.4 | 307.8 | 683.9 | 645.9 | 355.9 | 142.3 | 144.28 | 233.6 |
| | | Bidhaa zilizoagizwa | 711.8 | 678.1 | 846.8 | 787.6 | 1,145.40 | 1,444.20 | 1,571.10 | 2,147.60 | 1,630.20 | 1,408.10 | 1762.78 | 1,987.60 |
| | | **Jumla** | **935.3** | **1,042.00** | **,481.0** | **1,446.80** | **1,665.80** | **1,752.00** | **2,255.00** | **2,793.50** | **1,986.10** | **1,550.40** | **1,907.06** | **2,221.20** |
| | | **Urari** | **-488.3** | **-314.2** | **-212.6** | **-128.4** | **-625** | **-1136.4** | **-887.2** | **-1501.7** | **-1274.3** | **-1265.8** | **- 1618.50** | **-1754.00** |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| 2 | **India** | Bidhaa zilizouzwa | 171.8 | 183.8 | 218.5 | 202.7 | 476.5 | 748.2 | 1,254.50 | 1,320.30 | 706.4 | 977.6 | 734.27 | 867.70 |
| | | Bidhaa zilizoagizwa | 891.2 | 757.3 | 864.6 | 784.5 | 867.4 | 2,088.20 | 1,848.60 | 1,458.30 | 1,421.60 | 1,077.60 | 1218.07 | 1,258.40 |
| | | **Jumla** | **1,063.00** | **941.1** | **1,083.10** | **987.2** | **1,343.90** | **2,836.40** | **3,103.10** | **2,778.60** | **2,128.00** | **2,055.20** | **1952.34** | **2126.10** |
| | | **Urari** | **-719.4** | **-573.5** | **-646.1** | **-581.8** | **-390.9** | **-1340** | **-594.1** | **-138** | **-715.2** | **-100** | **-483.81** | **-390.70** |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| 3 | **Japan** | Bidhaa zilizouzwa | 136.9 | 164.7 | 209.7 | 346.8 | 296.5 | 220 | 247.8 | 263.4 | 139.2 | 75.7 | 66.72 | 64.1 |
| | | Bidhaa zilizoagizwa | 711.8 | 413.6 | 548.8 | 502.9 | 510.5 | 466.7 | 559.3 | 458.6 | 369.2 | 365.2 | 398.13 | 485.1 |
| | | **Jumla** | **848.7** | **578.3** | **758.5** | **849.7** | **807** | **686.7** | **807.1** | **722** | **508.4** | **440.9** | 464.85 | 549.20 |
| | | **Urari** | **-574.9** | **-248.9** | **-339.1** | **-156.1** | **-214** | **-246.7** | **-311.5** | **-195.2** | **-230** | **-289.5** | -331.41 | -421.00 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

# *KIAMBATISHO NA 8*

## *Biashara kati ya Tanzania na Jumuiya mbalimbali kwa mwaka 2009 - 2019 (Dola za Kimarekani '000,000)*

*Biashara kati ya Tanzania na Jumuiya mbalimbali kwa mwaka 2009 - 2019 (Dola za Kimarekani '000,000)*

| Na | Jumuiya | Maelezo | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ulaya | Bidhaa zilizouzwa | 440.00 | 464.00 | 553.50 | 745.40 | 898.40 | 791.70 | 708.70 | 236.50 | 441.40 | 497.82 | 399.30 |
| | | Bidhaa zilizoagizwa | 1,076.60 | 1,111.40 | 1,074.40 | 1,536.90 | 2,759.40 | 2,895.00 | 1,159.80 | 557.70 | 936.10 | 1,015.76 | 909.01 |
| | | **Jumla** | **1,516.60** | **1,575.40** | **1,627.90** | **2,282.30** | **3,657.80** | **3,686.70** | **1,868.50** | **794.20** | **1,377.50** | **1,513.57** | **1,308.31** |
| | | **Urari** | **(636.60)** | **(647.40)** | **(520.90)** | **(791.50)** | **(1,861.00 )** | **(2,103.30)** | **(451.10)** | **(321.20)** | **(494.70)** | **(517.94)** | **(509.71)** |
| 2 | Africa Mashariki (EAC) | Bidhaa zilizouzwa | 263.80 | 450.10 | 352.40 | 515.30 | 419.10 | 598.10 | 1,062.40 | 437.70 | 349.60 | 447.50 | 674.40 |
| | | Bidhaa zilizoagizwa | 310.50 | 285.20 | 263.80 | 668.40 | 394.70 | 706.00 | 322.80 | 298.90 | 220.40 | 302.93 | 329.10 |
| | | **Jumla** | **574.30** | **735.30** | **616.20** | **1,183.70** | **813.80** | **1,304.50** | **1,385.20** | **736.60** | **570.00** | **750.43** | **1,003.50** |
| | | **Urari** | **(46.70)** | **164.90** | **88.60** | **(153.10)** | **24.40** | **(108.30)** | **739.60** | **138.80** | **129.20** | **144.57** | **345.30** |
| 3 | Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC) | Bidhaa zilizouzwa | 374.20 | 625.10 | 1,158.80 | 1,421.90 | 1,243.55 | 1,235.90 | 1,357.70 | 1,017.90 | 877.80 | 999.34 | 1,330.90 |
| | | Bidhaa zilizoagizwa | 733.20 | 827.70 | 881.30 | 1,093.10 | 835.90 | 773.00 | 771.20 | 612.40 | 600.64 | 604.32 | 155.10 |
| | | **Jumla** | **1,107.40** | **1,452.80** | **2,040.10** | **2,515.00** | **2,079.45** | **2,008.90** | **2,128.90** | **1,630.30** | **1,478.44** | **1,603.66** | **1,486.00** |
| | | **Urari** | **-359.00** | **-202.60** | **277.50** | **328.80** | **407.65** | **462.90** | **586.50** | **405.50** | **277.16** | **395.03** | **1,175.80** |
| 4 | Afrika (CFTA) | Bidhaa zilizouzwa | 646.15 | 1,205.83 | 1,517.78 | 2,113.14 | 2,420.00 | 1,620.33 | 1,407.25 | 1,262.49 | 1,419.84 | 1,485.05 | 1,898.50 |
| | | Bidhaa zilizoagizwa | 1,174.79 | 1,204.19 | 1,718.84 | 1,836.28 | 1,451.00 | 1,482.65 | 1,011.79 | 984.64 | 895.88 | 989.01 | 537.04 |
| | | **Jumla** | 1,820.94 | 2,410.02 | 3,236.62 | 3,949.42 | 3,871.00 | 3,102.98 | 2,419.03 | 2,247.13 | 2,315.72 | 2,474.06 | 2,435.54 |
| | | **Urari** | -528.64 | 1.64 | (201.06) | 276.86 | 969.00 | 137.68 | 395.46 | 277.85 | 523.96 | 496.04 | 1,361.46 |
| 5 | Tripitite (EAC, SADC, COMESA) | Bidhaa zilizouzwa | 859.66 | 1,405.03 | 1,830.99 | 2,350.03 | 2,082.65 | 2,441.01 | 2,986.19 | 1,983.47 | 1,900.15 | 2,160.15 | 2,022.90 |
| | | Bidhaa zilizoagizwa | 1,149.18 | 1,245.50 | 1,346.19 | 1,916.76 | 1,395.60 | 2,333.21 | 1,528.96 | 1,375.70 | 1,217.00 | 1,385.62 | 515.40 |
| | | **Jumla** | **2,008.84** | **2,650.53** | **3,177.18** | **4,266.79** | **3,478.25** | **4,774.22** | **4,515.15** | **3,359.17** | **3,117.16** | **3,545.76** | **2,538.30** |
| | | **Urari** | **-289.53** | **159.53** | **484.80** | **433.27** | **687.05** | **107.80** | **1,457.23** | **607.77** | **683.15** | **774.53** | **1,507.50** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**_KIAMBATISHO NA. 9a_**

***Wastani wa Bei ya Mazao Makuu ya Chakula kwa mwezi Desemba 2019- Machi, 2020. Bei TZS/100Kg***

| Bidhaa | 2019-Des | 2020-Jan | 2020-Feb | 2020-Machi | Tofauti (Des Vs Machi) |
|---|---|---|---|---|---|
| Maharage | 219,079 | 214,873 | 210,208 | 179,410 | ▼18.1% |
| Uwele | 101,850 | 116,599 | 114,747 | 117,461 | ▲15.3% |
| Ulezi | 131,235 | 129,072 | 124,895 | 128,463 | ▼2.1% |
| Viazi Mviringo | 71,000 | 72,766 | 73,993 | 71,000 | ►0.0% |
| Mahindi | 91,266 | 92,293 | 85,038 | 65,217 | ▼28.5% |
| Mchele | 189,342 | 187,736 | 190,898 | 183,859 | ▼2.9% |
| Mtama | 105,406 | 110,677 | 116,055 | 114,062 | ▲8.2% |
| Ngano | 120,818 | 117,535 | 123,297 | 121,117 | ▲0.2% |

***Chanzo**: Wizara ya Viwanda na Biashara.*

**KIAMBATISHO NA 9b**

***Mwenendo wa Bei za baadhi ya bidhaa za viwandani mwezi Aprili, 2019 na mwezi Aprili, 2020 kwa tarehe 16/04/2020.***

**APRILI, 2019**

| NA | MKOA/ | SARUJI | NONDO (TZS/PC) | | | | BATI (TZS/PC) | | | SUKARI | | MAFUTA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MJI | 50KG | 8mm | 10mm | 12mm | 16mm | 32G | 30G | 28G | 50KG | 1KG | ALZT 1 Lt |
| 2 | Mtwara | 12,500 | 12,000 | 16,000 | 19,750 | 42,000 | 14,750 | 18,500 | 27,000 | 125,000 | 2,800 | 4,750 |
| 3 | Daes salaam | 14,000 | 12,000 | 15,000 | 19,500 | 34,000 | 15,375 | 18,000 | 24,750 | 112,000 | 2,750 | 4,600 |
| 4 | Musoma | 21,000 | 10,500 | 15,000 | 20,000 | 35,000 | 16,000 | 21,000 | 22,500 | 116,000 | 2,700 | 4,500 |
| 5 | Mwanza | 18,000 | 15,000 | 15,500 | 20,000 | 34,500 | 14,500 | 18,000 | 27,500 | 120,000 | 2,700 | 4,500 |
| 6 | Tanga | 12,500 | 12,000 | 15,000 | 19,200 | 34,500 | 16,000 | 19,250 | 26,000 | 110,000 | 2,600 | 4,500 |
| 7 | Arusha | 15,000 | 12,500 | 15,000 | 19,750 | 32,000 | 15,000 | 19,500 | 26,000 | 110,000 | 2,500 | 3,500 |
| 8 | Rukwa | 16,500 | 15,000 | 16,000 | 21,750 | 38,500 | 14,500 | 17,500 | 26,000 | 115,000 | 2,600 | 4,750 |
| 9 | Morogoro | 13,200 | 12,000 | 15,500 | 20,000 | 36,000 | 16,000 | 18,000 | 26,000 | 100,000 | 2,500 | 4,600 |
| 10 | Lindi | 13,000 | 10,000 | 14,000 | 23,000 | 39,500 | 15,500 | 19,500 | 29,500 | 125,000 | 2,800 | 4,600 |
| 11 | Kigoma | 17,000 | 10,000 | 15,000 | 19,500 | 37,000 | 14,750 | 15,526 | 21,071 | 116,000 | 2,600 | 4,600 |
| 12 | Moshi | 13,650 | 11,500 | 14,600 | 19,700 | 37,500 | 14,900 | 18,600 | 25,000 | 110,000 | 2,700 | 4,500 |
| 13 | Bukoba | 18,250 | 12,500 | 16,500 | 21,500 | 38,000 | 17,000 | 19,500 | 28,500 | 112,000 | 2,500 | 4,600 |
| 14 | Ruvuma | 14,500 | 13,000 | 16,000 | 21,000 | 37,000 | 15,000 | 19,000 | 22,500 | 114,000 | 2,600 | 3,800 |
| 15 | Dodoma | 14,500 | 12,000 | 16,000 | 21,000 | 36,500 | 16,000 | 20,000 | 26,000 | 115,000 | 2,700 | 3,500 |

**APRILI 2020* Due to 16th April,2020**

| NA | MKOA/ | SARUJI | NONDO (TZS/PC) | | | | BATI (TZS/PC) | | | SUKARI | | MAFUTA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MJI | 50KG | 8mm | 10mm | 12mm | 16mm | 32G | 30G | 28G | 50KG | 1KG | ALZT 1LT |
| 2 | Mtwara | 12,750 | 12,000 | 16,000 | 22,000 | 42,500 | 15,500 | 17,500 | 27,500 | 158,000 | 3,500 | 4,750 |
| 3 | Daes salaam | 14,120 | 12,000 | 15,000 | 19,500 | 34,600 | 15,750 | 18,250 | 25,000 | 175,000 | 3,600 | 4,600 |
| 4 | Musoma | 21,000 | 10,500 | 15,500 | 20,000 | 35,000 | 16,000 | 19,000 | 22,500 | 155,500 | 3,000 | 4,500 |
| 5 | Mwanza | 18,250 | 15,000 | 15,500 | 20,000 | 35,000 | 14,500 | 18,000 | 27,500 | 158,000 | 3,500 | 5,000 |
| 6 | Tanga | 13,233 | 12,000 | 15,000 | 17,500 | 32,000 | 16,000 | 19,500 | 26,000 | 160,000 | 3,200 | 4,500 |
| 7 | Arusha | 14,667 | 12,500 | 16,000 | 19,750 | 32,000 | 15,000 | 17,500 | 26,000 | 150,000 | 3,000 | 3,500 |
| 8 | Rukwa | 16,800 | 15,000 | 15,500 | 22,000 | 22,000 | 14,500 | 18,000 | 26,000 | 158,000 | 3,000 | 4,750 |
| 9 | Morogoro | 18,500 | 12,000 | 15,000 | 20,500 | 36,000 | 16,000 | 19,500 | 26,000 | 150,000 | 3,200 | 4,600 |
| 10 | Lindi | 13,875 | 10,000 | 14,000 | 23,000 | 39,500 | 15,500 | 17,250 | 29,500 | 158,000 | 3,550 | 4,600 |
| 11 | Kigoma | 17,000 | 10,000 | 15,000 | 19,500 | 37,000 | 14,000 | 15,526 | 27,500 | 160,000 | 3,900 | 4,600 |
| 12 | Moshi | 13,650 | 11,500 | 14,600 | 19,700 | 37,500 | 14,900 | 19,100 | 25,500 | 160,000 | 3,800 | 4,600 |
| 13 | Bukoba | 19,667 | 12,500 | 16,500 | 21,500 | 38,000 | 17,000 | 19,500 | 28,000 | 130,000 | 2,800 | 4,600 |
| 14 | Ruvuma | 14,500 | 13,000 | 16,000 | 21,000 | 37,000 | 15,000 | 19,000 | 30,000 | 158,000 | 3,200 | 4,600 |
| 15 | Dodoma | 15,500 | 11,250 | 15,250 | 23,000 | 38,250 | 16,000 | 21,000 | 26,000 | 159,000 | 3,700 | 3,750 |

***Chanzo**: Wizara ya Viwanda na Biashara.*

## *Mwenendo wa Wastani wa Bei ya Mazao Makuu kwa Mwezi kwa kipindi cha Mwaka 2015 – 2019* (TZS/100KG)

| Month | Beans | Bulrush Millet | Finger Millet | Irish potatoes | Maize | Rice | Sorghum | Wheat |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2019-12 | 219,079 | 101,850 | 131,235 | 71,408 | 91,266 | 189,342 | 105,406 | 120,818 |
| 2019-11 | 208,250 | 99,498 | 140,666 | 72,910 | 84,859 | 184,696 | 108,940 | 130,273 |
| 2019-10 | 176,953 | 99,423 | 127,784 | 72,640 | 80,967 | 181,334 | 93,745 | 130,501 |
| 2019-09 | 167,866 | 100,499 | 125,250 | 72,864 | 74,524 | 169,732 | 91,400 | 121,405 |
| 2019-08 | 158,436 | 101,040 | 125,350 | 69,000 | 67,075 | 160,016 | 88,965 | 124,596 |
| 2019-07 | 160,044 | 98,682 | 131,819 | 72,507 | 61,341 | 162,418 | 79,283 | 122,215 |
| 2019-06 | 162,802 | 89,264 | 134,246 | 74,578 | 59,851 | 164,936 | 81,557 | 123,918 |
| 2019-05 | 163,601 | 85,238 | 133,556 | 70,749 | 59,160 | 167,412 | 76,934 | 131,838 |
| 2019-04 | 159,606 | 85,913 | 136,583 | 69,039 | 54,027 | 166,172 | 76,864 | 126,679 |
| 2019-03 | 165,352 | 73,210 | 134,727 | 68,302 | 52,987 | 168,520 | 75,677 | 119,357 |
| 2019-02 | 164,745 | 71,397 | 138,659 | 75,329 | 50,812 | 167,567 | 73,619 | 123,460 |
| 2019-01 | 159,310 | 80,272 | 138,567 | 82,434 | 48,903 | 158,447 | 76,493 | 120,112 |
| 2018-12 | 153,503 | 81,047 | 138,570 | 87,113 | 46,853 | 151,545 | 77,980 | 114,185 |
| 2018-11 | 161,304 | 72,833 | 135,048 | 89,843 | 42,374 | 153,717 | 71,833 | 122,067 |
| 2018-10 | 158,584 | 75,120 | 131,695 | 81,940 | 37,671 | 152,289 | 75,565 | 114,202 |
| 2018-09 | 156,677 | 76,639 | 126,453 | 80,835 | 39,692 | 148,305 | 76,575 | 112,076 |
| 2018-08 | 157,335 | 78,008 | 129,635 | 79,410 | 40,593 | 148,418 | 77,664 | 113,379 |
| 2018-07 | 163,693 | 80,061 | 136,446 | 78,648 | 40,967 | 152,567 | 68,635 | 114,983 |
| 2018-06 | 168,613 | 80,981 | 143,013 | 73,222 | 43,002 | 161,450 | 84,519 | 119,479 |
| 2018-05 | 174,845 | 84,991 | 147,488 | 68,918 | 44,168 | 170,758 | 90,255 | 121,170 |
| 2018-04 | 167,111 | 77,608 | 150,188 | 70,282 | 45,953 | 202,700 | 91,804 | 127,625 |
| 2018-03 | 168,479 | 77,847 | 148,837 | 67,291 | 46,094 | 198,401 | 79,712 | 120,059 |
| 2018-02 | 178,101 | 74,301 | 147,027 | 72,530 | 49,167 | 195,813 | 72,606 | 109,014 |
| 2018-01 | 178,824 | 89,231 | 154,335 | 76,789 | 49,807 | 193,578 | 76,436 | 106,666 |
| 2017-12 | 177,679 | 73,034 | 146,816 | 71,932 | 59,674 | 191,989 | 60,500 | 114,283 |
| 2017-11 | 182,822 | 86,350 | 146,649 | 69,032 | 53,215 | 185,166 | 76,360 | 121,193 |

| Month | Beans | Bulrush Millet | Finger Millet | Irish potatoes | Maize | Rice | Sorghum | Wheat |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2017-10 | 168,419 | 83,698 | 142,777 | 67,106 | 54,539 | 187,624 | 86,874 | 110,315 |
| 2017-09 | 172,795 | 93,959 | 148,020 | 68,494 | 56,401 | 179,845 | 88,864 | 120,895 |
| 2017-08 | 168,027 | 106,846 | 141,276 | 70,653 | 57,629 | 170,855 | 95,879 | 123,450 |
| 2017-07 | 165,057 | 122,902 | 154,038 | 77,478 | 69,693 | 170,895 | 101,856 | 122,964 |
| 2017-06 | 171,701 | 134,248 | 161,075 | 82,145 | 81,938 | 175,283 | 117,939 | 131,075 |
| 2017-05 | 176,695 | 127,051 | 168,803 | 84,572 | 94,915 | 177,830 | 123,913 | 137,357 |
| 2017-04 | 183,052 | 126,142 | 167,438 | 81,394 | 106,511 | 177,685 | 132,802 | 135,750 |
| 2017-03 | 180,705 | 123,345 | 154,341 | 78,960 | 103,143 | 171,760 | 117,288 | 131,761 |
| 2017-02 | 178,677 | 116,809 | 141,234 | 86,204 | 105,697 | 177,881 | 107,887 | 127,865 |
| 2017-01 | 175,602 | 98,990 | 131,320 | 83,468 | 93,356 | 162,745 | 94,900 | 119,921 |
| 2016-12 | 171,743 | 89,819 | 120,913 | 79,426 | 85,160 | 152,274 | 104,545 | 123,196 |
| 2016-11 | 169,726 | 90,024 | 117,957 | 81,386 | 72,620 | 147,787 | 102,691 | 124,402 |
| 2016-10 | 164,656 | 91,412 | 113,624 | 81,764 | 64,054 | 145,466 | 96,778 | 122,983 |
| 2016-09 | 151,357 | 88,208 | 108,533 | 80,882 | 56,984 | 138,551 | 84,896 | 122,000 |
| 2016-08 | 149,699 | 88,649 | 108,799 | 82,074 | 55,855 | 139,596 | 89,886 | 125,018 |
| 2016-07 | 149,624 | 92,773 | 111,314 | 87,146 | 57,203 | 147,777 | 89,209 | 127,237 |
| 2016-06 | 149,125 | 93,663 | 110,698 | 89,686 | 53,985 | 148,129 | 97,811 | 121,220 |
| 2016-05 | 150,408 | 93,105 | 110,653 | 91,934 | 55,357 | 158,951 | 93,837 | 122,584 |
| 2016-04 | 151,563 | 91,862 | 111,593 | 86,147 | 57,945 | 174,746 | 93,466 | 124,882 |
| 2016-03 | 159,081 | 92,322 | 112,303 | 77,518 | 64,296 | 179,597 | 92,505 | 124,570 |
| 2016-02 | 171,738 | 90,521 | 112,004 | 79,235 | 67,316 | 184,137 | 92,338 | 126,991 |
| 2016-01 | 172,949 | 89,809 | 112,154 | 80,884 | 67,507 | 179,698 | 85,114 | 124,069 |
| 2015-12 | 172,852 | 86,401 | 110,718 | 82,791 | 65,104 | 176,237 | 81,638 | 119,257 |
| 2015-11 | 174,853 | 80,932 | 114,293 | 90,552 | 63,404 | 176,644 | 75,479 | 115,667 |
| 2015-10 | 164,537 | 80,234 | 112,296 | 79,483 | 58,009 | 170,589 | 76,586 | 116,745 |
| 2015-09 | 158,241 | 81,448 | 116,375 | 74,098 | 56,840 | 162,029 | 74,573 | 113,679 |
| 2015-08 | 158,530 | 83,905 | 113,928 | 72,421 | 56,358 | 158,069 | 77,661 | 117,225 |
| 2015-07 | 158,313 | 88,804 | 115,293 | 73,360 | 52,154 | 153,402 | 77,965 | 119,802 |
| 2015-06 | 163,723 | 77,380 | 109,083 | 79,275 | 47,670 | 155,360 | 72,115 | 122,578 |

| Month | Beans | Bulrush Millet | Finger Millet | Irish potatoes | Maize | Rice | Sorghum | Wheat |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2015-05 | 156,789 | 74,983 | 112,252 | 77,508 | 47,163 | 162,702 | 69,222 | 123,703 |
| 2015-04 | 151,733 | 70,927 | 112,992 | 71,897 | 47,708 | 166,902 | 65,779 | 121,971 |
| 2015-03 | 149,534 | 68,559 | 109,471 | 68,249 | 39,940 | 161,422 | 63,548 | 117,244 |
| 2015-02 | 150,829 | 61,364 | 107,185 | 69,767 | 37,452 | 150,296 | 61,932 | 106,643 |
| 2015-01 | 153,493 | 64,366 | 107,543 | 72,970 | 38,328 | 145,661 | 63,118 | 114,442 |

***KIAMBATISHO Na. 9d***

Wastani wa Bei za Mazao Makuu ya Chakula mwaka 2010 - 2020* mwezi Machi, Shilingi kwa Gunia la Kilo 100

| **Mazao** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020*** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Maharage | 160,144 | 159,561 | 175,103 | 165,589 | 185,183 | 203,027 |
| Uwele | 77,102 | 91,943 | 107,781 | 79,056 | 99,767 | 116,218 |
| Ulezi | 112,598 | 112,881 | 150,316 | 140,728 | 130,849 | 129,082 |
| Viazi Mviringo | 76,377 | 83,313 | 76,786 | 77,235 | 72,116 | 72,430 |
| Mahindi | 51,321 | 63,367 | 78,059 | 43,862 | 75,280 | 79,885 |
| Mchele | 162,039 | 158,434 | 177,463 | 169,128 | 173,535 | 187,560 |
| Mtama | 70,557 | 95,343 | 100,422 | 78,632 | 93,946 | 113,901 |
| Ngano | 119,174 | 124,779 | 124,736 | 116,242 | 126,563 | 121,255 |

*Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara.*

*2020*- Jan – Machi, 2020*



*Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Innocent L. Bashungwa (Mb), kushoto ni Katibu Mkuu Prof. Riziki Shemdoe, wakisikiliza maelezo kuhusu uzalishaji wa nyaya za umeme kwenye Kiwanda cha Tropical Industries kilichopo Mikocheni Jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Innocent L. Bashungwa (Mb), akiwa na mmoja wa wajasiriamali wa bidhaa za ngozi kwenye Maonesho ya Sabasaba ya mwaka 2019.*



*Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Innocent L. Bashungwa (Mb), akiangalia nguo zinazozalishwa na Kiwanda cha Mazava.*





*Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara Mhandisi Stella M. Manyanya (Mb), akiwa na wafanyakazi wa Kiwanda cha kutengeneza pipi cha Ivori kilichopo mkoani Iringa.*